# BUNGE LA TANZANIA

# MAJADILIANO YA BUNGE

## MKUTANO WA KUMI NA TANO

### Kikao cha Thelathini na Nne – Tarehe 27 Mei, 2024

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

## D U A

*Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alisoma Dua*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tuketi.

Katibu.

**NDG. EMMANUEL MPANDA - KATIBU MEZANI:**

## HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati ifuatayo iliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE (MHE. BALOZI MBAROUK NASSOR MBAROUK):**

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa mwaka wa fedha 2024/2025.

**SPIKA:** Ahsante sana.

Katibu.

**NDG. EMMANUEL MPANDA - KATIBU MEZANI:**

**MASWALI NA MAJIBU**

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, maswali, tutaanza na Ofisi ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Khadija Shaaban Taya, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 439

**Kuwekwa Maeneo Maalum ya Watu Wenye Ualbino katika Mikutano ya Hadhara**

**MHE. KHADIJA S. TAYA** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itahakikisha kunakuwa na maeneo maalum ya Watu wenye Ualbino kwenye mikutano ya hadhara ili wasikae juani?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Ummy Nderiananga, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE NA URATIBU (MHE. UMMY H. NDERIANANGA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, Sera ya Taifa ya Maendeleo na Huduma kwa Watu Wenye Ulemavu ya 2004, kupitia matamko yake namba 3, Kifungu cha 11 - Uondoaji Vikwazo vya Ufikivu, 3:1-Matunzo kwa Watu wenye Ulemavu, 3(13) kuhusu Marekebisho na 3(14) - Mchangamano, imeonesha namna ambayo watu wenye ulemavu wakiwemo wenye Ualbino wanavyostahili kushiriki na kushirikishwa katika shughuli za kijamii na kisiasa. Aidha, Sheria ya Watu wenye Ulemavu, Sura Na.183, Sehemu ya Nne, Kifungu cha 15(1) na Sehemu ya Tisa, Kifungu cha 51 zinabainisha juu ya ushiriki wa watu wenye ulemavu katika shughuli za kijamii na kisiasa.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia nyaraka hizi muhimu, Serikali inatoa wito kwa viongozi wote wa Serikali na Taasisi zake pamoja na Taasisi na wadau wa huduma za kijamii kuhakikisha

kuwa wakati wa utoaji wa huduma, suala la ufikivu na usalama kwa watu wenye Ualbino linazingatiwa. Aidha, Serikali inaendelea kutoa wito kwa watu wenye Ualbino kutambua mahitaji na haki zao kiafya na kujiepusha na mazingira yanayoweza kuhatarisha afya zao. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Khadija Shaaban Taya, swali la nyongeza.

**MHE. KHADIJA S. TAYA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali, pamoja na majibu hayo nina maswali mawili ya nyongeza.

Swali la kwanza, kwa kuwa tatizo hilo bado lipo na linajitokeza. Je, ni kwa kiasi gani watendaji wanaufahamu wa sera hii ambayo Mheshimiwa Naibu Waziri umeisema?

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili; je, sasa Serikali haioni haja ya kutoa mwongozo tena mara nyingine kwa watendaji wanaohusika na masuala ya sherehe za Serikali?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE NA URATIBU (MHE. UMMY H. NDERIANANGA):** Mheshimiwa Spika, naomba nimshukuru Mheshimiwa Keysha, kama nilivyojibu jibu la msingi tuna sera na sheria. Nitoe rai kwa wale wanaoandaa shughuli za Serikali na sisi Ofisi ya Waziri Mkuu chini ya Waziri wetu Mheshimiwa Jenista, tumekuwa tukifanya jambo hili kwa pamoja. Maadhimisho mbalimbali ya sherehe tuna kitengo cha sherehe waendelee kuweka nafasi hizi za watu wenye Ualbino na watu wengine kwa sababu tunaweka masuala ya tenti kuweka vizuri ili waweze kukaa. Tuna mkakati gani? Tunaendelea kushirikiana na Chama cha Watu Wenye Ualbino Tanzania *(TAS)* pamoja na wadau wengine wanaofanya kazi kwenye eneo la watu wenye ulemavu kujengea elewa jamii ili kufahamu haki za watu wenye ulemavu na sera.

Mheshimiwa Spika, pia tuko kwenye marekebisho ya Sera ya Taifa ya Watu Wenye Ulemavu ambayo pia nayo inagusa kundi la watu wenye Ualbino. Kwa hiyo nimtoe mashaka Mheshimiwa Khadija Shaaban Taya maarufu kama Keysha kwamba mambo yanaenda vizuri Serikali ya Awamu ya Sita, Mheshimiwa Rais, Daktari Samia tunaendelea kuwajali watu wenye ulemavu na watu wenye Ualbino. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea na Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Mariam Madalu Nyoka, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 440

**Ujenzi wa Barabara ya Nandembo Nampungu – Tunduru**

**MHE. MARIAM M. NYOKA** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga Barabara ya Nandembo - Kitula hadi Nampungu - Tunduru kwa kiwango cha lami?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Zainab Katimba.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, Barabara ya Nandembo - Nampungu ina urefu wa kilometa 28.81 ambapo katika mwaka 2021/2022, yalifanyika matengenezo ya tabaka la changarawe kilometa 27.3 na kilometa 1.51, tabaka la udongo kwa gharama ya shilingi milioni 241. Aidha, Serikali imepanga kufanya usanifu wa Barabara ya Nandembo – Nampungu kwa ajili ya ujenzi kwa kiwango cha lami kadri ya upatikanaji wa fedha.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kuhudumia barabara za Mji Tunduru kwa kuzijenga, kuzifanyia matengenezo na kuzikarabati kulingana na upatikana wa fedha.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mariam Madalu Nyoka, swali la nyongeza.

**MHE. MARIAM M. NYOKA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru naomba niulize maswali mawili ya nyongeza.

Swali la kwanza; Barabara ya kutoka Kangomba – Ipanje - Kidodoma- Legezamwendo hadi Machemba lini itatengenezwa ili iweze kupitika muda wote? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili; Serikali ina mpango gani wa kutengeneza Barabara ya kutoka Pacha ya Mwongozo kupita Mchuruka hadi Cheleweni ili nayo iweze kupitika muda wote?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Spika, nimpongeze Mheshimiwa Mbunge amekuwa akifanya kazi kubwa sana ya kufuatilia maendeleo ya miundombinu ya barabara katika Mkoa wa Ruvuma.

Mheshimiwa Spika, kuhusu swali lake la kwanza, Barabara ya Kangomba – Ipanje – Kidodoma - Legezamwendo hadi Machemba yenye urefu wa kilometa 85 tayari Serikali imekuwa ikitenga fedha katika kila mwaka wa fedha kuhakikisha barabara hiyo inapitika kwa misimu yote. Katika mwaka 2022/2023 shilingi milioni 250 zilitolewa kwa ajili ya kuchonga na kuweka kifusi kwenye barabara hiyo lakini mwaka 2023/2024 shilingi milioni 350 zimetengwa kwa ajili ya kuchonga na kuweka kifusi pia kuweka makalvati manne.

Mheshimiwa Spika, pia katika Mwaka wa Fedha 2024/2025, shilingi milioni 270 zimetengwa kwa ajili ya kurekebisha maeneo

korofi yaliyobaki ambayo yana urefu wa kilometa 20. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge baada ya marekebisho haya ya mwaka wa fedha 2024/2025, barabara hii itakuwa imekamilika na itakuwa inapitika mwaka mzima.

Mheshimiwa Spika, kuhusu swali lake la pili kuhusu Barabara ya Mwongozo – Mchuruka - Cheleweni katika Mwaka wa Fedha 2023/2024, shilingi milioni 61.32 zimetolewa kwa ajili ya kurekebisha sehemu korofi yenye urefu wa kilometa 9.41. Katika mwaka wa bajeti 2024/2025 shilingi milioni 18 zimetengwa kwa ajili ya ujenzi wa makalvati matatu kwenye maeneo korofi. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge Serikali itaendelea kutenga fedha kuhakikisha inaboresha na inakarabati miundombinu ya barabara katika majimbo yote ya Mkoa wa Ruvuma. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Mwita Mwikabe Waitara, swali la nyongeza.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Serikali iliahidi kujenga kilometa mbili za lami kwa kila makao makuu ya halmashauri mpya na Mheshimiwa Bashungwa akiwa Waziri wa TAMISEMI aliwaahidi Wananchi wa Nyamwaga barabara ya kilometa mbili kwa kiwango cha lami...

**SPIKA:** Swali.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Spika, naomba kujua ni lini ahadi hiyo ya Mheshimiwa Waziri itatekelezwa katika Mji wa Nyamwaga? Ahsante

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Spika, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali ina dhamira ya dhati ya kuhakikisha kwamba inaboresha miundombinu na hasa kwenye barabara zetu hizi za wilaya. Nimhakikishie Serikali itahakikisha inatafuta pesa kuhakikisha inajenga barabara aliyoitaja.

**SPIKA:** Mheshimiwa Boniphace Nyangidu Butondo, Mbunge wa Kishapu, sasa aulize swali lake.

Na. 441

**Fedha kwa Ajili ya Ujenzi wa Barabara – Mji wa Mhunze Kishapu**

**MHE. BONIPHACE N. BUTONDO** aliuliza:-

Je, lini fedha za kukamilisha ujenzi wa Barabara ya Mji wa Mhunze Wilayani Kishapu kwa kiwango cha lami zitatolewa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA)** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea kuzifanyia usanifu barabara zote kuu na muhimu za Mji wa Mhunze kutoka tabaka la udongo na changarawe kwenda tabaka la lami ambapo kilometa mbili za Barabara za *DED - DC* kilometa moja na Madukani kilometa moja zimejengwa kwa tabaka la lami kwa gharama ya shilingi bilioni 1.07. Aidha, katika mwaka 2024/2025, Serikali imetenga bajeti ya shilingi milioni 680 kwa ajili ya ujenzi wa tabaka la lami kilometa moja Barabara ya Madukani.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kutenga fedha kila mwaka mpaka kukamilisha barabara muhimu za Mji wa Mhunze Wilayani Kishapu kwa kiwango cha lami.

**SPIKA:** Mheshimiwa Boniphace Butondo, swali la nyongeza.

**MHE. BONIPHACE N. BUTONDO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali. Naomba niulize maswali maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; mwaka 2015 aliyekuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Hayati Magufuli aliahidi kilometa nne katika Mji wa Mhunze na mpaka sasa kilometa moja imetekelezwa katika ujenzi. Serikali inasema nini juu ya kilometa tatu zilizobaki kwa ajili ya kuzitekeleza?

Mheshimiwa Spika, swali la pili; tumekuwa tukipokea fedha za mfuko wa jimbo, tozo na *road fund* katika usawa sahihi kwa pamoja kwa maana ya kwamba, zimekuwa zikitolewa katika kila halmashauri kwa usawa lakini kiukweli mitandao ya barabara inatofautiana wilaya hadi wilaya. Kwa nini Serikali isije na *formula* mpya ya kutoa mgao wa fedha kulingana na ukubwa wa mtandao wa barabara katika kila wilaya? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mbunge amekuwa akifanya kazi kubwa sana ya kuwatumikia wananchi wake.

Kuhusiana na swali la kwanza, naomba nimfahamishe Mheshimiwa Mbunge kwamba kipaumbele cha Serikali ni kuhakikisha ahadi za Viongozi Wakuu zinatekelezwa. Kama alivyosema yeye mwenyewe tayari katika barabara hii ya Mji wa Mhunze ambayo iliahidiwa kilometa nne tayari kilometa moja imeshajengwa kwa lami. Nimhakikishie katika Mwaka wa Fedha 2024/2025 shilingi milioni 688 zimetengwa kwa ajili ya kujenga barabara hii kwa kiwango cha lami lakini na kuweka taa. Kwa hiyo, nikuhakikishie ahadi ile iliyotolewa na Hayati Magufuli ya kilometa nne inaendelea kutekelezwa.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na swali lake la pili; kusema kweli Mheshimiwa Mbunge hoja yako ni ya msingi na Serikali imelitambua hilo na tayari Serikali inafanya mchakato ili kutengeneza *formula* mpya ambayo itazingatia mambo kadha wa kadha ikiwemo urefu wa mtandao wa barabara katika jimbo husika katika mgao wa fedha hizi kwa ajili ya kuboresha miundombinu katika kila jimbo. Kwa hiyo, nimhakikishie Mbunge, hoja yake ni ya msingi Serikali inaendelea nayo na katika Mwaka wa Fedha 2024/2025, utaratibu mpya wa kutoa fedha hizi utaanza kutumika.

**SPIKA:** Haya ahsante sana. Mheshimiwa Grace Tendega, swali la nyongeza.

**MHE. GRACE V. TENDEGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, Barabara ya Jimbo la Kilolo kutoka Mtandika hadi Nyanzwa kilometa 40 ni mbovu mno na ni muhimu kwa uchumi. Je, lini itajengwa hata kwa kiwango cha changarawe?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Spika, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali inakusudia kutafuta fedha na kuhakikisha kwamba barabara hiyo inajengwa ili iweze kuwa na manufaa kwa ajili ya wananchi.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Kimei, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. CHARLES S. KIMEI:** Mheshimiwa Spika, je, ni lini Serikali itajenga barabara za lami angalau hata kilometa mbili kwenye Mji mdogo wa Himo? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Spika, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, Serikali inatafuta fedha na itahakikisha kwamba inakuja kujenga barabara hiyo aliyoitaja Mheshimiwa Mbunge.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora, Mheshimiwa Neema William, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

**MHE. NEEMA W. MGAYA:** Mheshimiwa Spika, ahsante, naomba sasa swali langu liweze kupatiwa majibu.

**SPIKA:** Mheshimiwa Neema swali lako ni namba 442.

**MHE. NEEMA W. MGAYA:** Mheshimiwa Spika, naomba swali langu namba 442 lipatiwe majibu ya Serikali.

Na. 442

**Serikali Kulipa Madeni ya Watumishi**

**MHE. NEEMA W. MGAYA** aliuliza:-

Je, lini Serikali itamaliza kulipa madeni ya muda mrefu ya watumishi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Neema William Mgaya, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kuchukua hatua mbalimbali katika kudhibiti uzalishaji wa madeni ya watumishi ikiwemo malimbikizo ya mishahara kwa kujenga Mfumo Mpya wa Taarifa za Kiutumishi na Mishahara *(HCMIS)* ulioanza kutumika mwezi Mei, 2021 ambao umeweza kudhibiti uzalishaji wa malimbikizo mapya ya mishahara.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hatua hiyo, kuanzia Mwezi Mei, 2021 hadi sasa Serikali imelipa madai ya malimbikizo ya mishahara kwa watumishi 132,611 yenye thamani ya shilingi bilioni 219.7. Aidha, Serikali inatoa wito kwa waajiri wote nchini kuhakiki na kuwasilisha taarifa za madeni ya watumishi kwa ajili ya taratibu za uhakiki na malipo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Neema Mgaya, swali la nyongeza.

**MHE. NEEMA W. MGAYA:** Mheshimiwa Spika, naipongeza Serikali ya Awamu ya Sita ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuweza kuanza kulipa madeni. Swali la kwanza; nataka kujua wamejipanga vipi kuhakikisha kwamba wanamaliza madeni yote na mpaka lini watakuwa wameweza kumaliza madeni hayo?

Mheshimiwa Spika, swali la pili; walimu wanalipwa madeni yao kupitia halmashauri. Je, Wizara ya Fedha imejipanga vipi kuhakikisha kwamba inapeleka fedha Hazina ili ziweze kufika kwenye halmashauri zetu kwa wakati? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Spika, juu ya Serikali imejipanga lini kumaliza madeni? Nataka nilihakikishie Bunge lako kwamba Serikali kwa mujibu wa taarifa na taratibu ambazo tumejipangia tunataka tuhakikishe kwamba madeni ya hawa walimu ikiwezekana hata leo yaishe yote. Sisi kwetu kinachotukwamisha ni wale waajiri ambao hawaleti taarifa kwa wakati na ndiyo maana najibu swali la msingi nilisisitiza kwamba Serikali inatoa wito kwa waajiri wote nchini, kuhakiki na kuwasilisha taarifa za madeni ya watumishi wa umma ili Serikali iweze kuwalipa.

Mheshimiwa Spika, nataka kukushukuru wewe na Bunge lako kwa sababu kila tunapoleta maombi ya bajeti kwa ajili ya malipo ya malimbikizo ya madeni yanayotokana na kazi za kiutumishi mmekuwa mnatupitishia na hivyo kutuwezesha kuweza kulipa.

Mheshimiwa Spika, narudia tena Wabunge wenzangu tuendelee kuwambusha waajiri hasa wakurugenzi katika halmashauri zetu kuendelea kuwasilisha taarifa zinazohusu madeni ya watumishi ili kutatua kilio hiki cha watumishi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu swali la pili juu ya Wizara ya Fedha imejipangaje. Wizara ya Fedha imekuwa inaleta fedha kwa wakati na kila tunaposema kwamba tunahitaji kulipa imekuwa

inafanya hivyo na ndiyo kupitia mfumo huu wa *HCMIS* fedha zinakuja na madeni katika zile taarifa yanalipwa, ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Oscar Kikoyo, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. OSCAR I. KIKOYO:** Mheshimiwa Spika, swali la nyongeza ni kwamba kuna ndugu zetu Wanajeshi waliyopigana na kulinda Taifa hili hasa kipindi cha mwaka 1978, 1979 kule Uganda, je, ni lini tutawalipa stahiki zao wale ambao wanadai mpaka sasa? *(Makofi)*

**SPIKA:** Hebu rudia swali lako.

**MHE. DKT. OSCAR I. KIKOYO:** Mheshimiwa Spika, kuna ndugu zetu Wanajeshi waliopigana Vita ya Kagera na Uganda, ambao bado wanadai stahiki zao, je, ni lini Serikali itawalipa hao wanajeshi wetu?

**SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge, nadhani hilo nilishawaagiza Serikali wafanye utafiti wa jumla ili watuletee. Kwa hiyo, bado wanaendelea nalo nadhani wakishahitimisha watalileta kwa sababu hao watu tujue kama kipo wanachokidai ama vyote walishalipwa na kama unataka kuuliza tena kama swali la msingi unaruhusiwa, lakini kwa maana ya majibu yake tunasubiri Serikali kwa sababu Bunge lilishatoa maelekezo kwa Serikali kulifanyia utafiti jambo hili ili tujue kama wapo ambao tunawadai au hapana ili majibu watakayoyatoa yawe kwa hao wote wa nchi nzima, kama walishalipwa wote iwe walilipwa wote na kwa muktadha huo ilibidi ajibu Mheshimiwa Waziri wa kutoka Ofisi ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Mbunge, kwa hivyo unaweza kulileta kama swali la msingi. Mheshimiwa Sophia Mwakagenda swali la nyongeza.

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali ya nyongeza. Kada ya Manesi ni kada ambayo inadai madeni mengi sana hasa fedha za ziada

kwa kufanya kazi za ziada. Je, ni lini Serikali itahakikisha manesi hawa wanapata fedha kwa wakati? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Spika, naomba kumjibu Mheshimiwa Mwakagenda kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, sisi ndani ya Ofisi ya Rais, Utumishi tunafanyakazi kwa taarifa, naendelea kusisitiza tena kama nilivyoeleza katika jibu la msingi, madeni yote yanayodaiwa na watumishi wa umma naomba yawasilishwe katika ofisi yetu mapema iwezekanavyo ili tuweze kuyalipa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Tunza Malapo, swali la nyongeza.

**MHE. TUNZA I. MALAPO:** Mheshimiwa Spika, ni lini Serikali itawalipa madeni yao wakufunzi wa vyuo vya ualimu, madeni hayo yameshahakikiwa na yanajulikana lakini bado hawajalipwa. Nakushukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Spika, kama itapendeza Bunge lako naona taarifa za kundi fulani wanadaiwa, mara kundi fulani linadai, mara kundi fulani linadai zimekuwa ni nyingi sana.

Mheshimiwa Spika, naomba sana Waheshimiwa Wabunge pamoja na kazi yetu ya Kibunge ni wakubwa katika maeneo yetu ni viongozi katika maeneo yetu, hebu tutumie nafasi hizi kuleta taarifa hizi pia ndani ya ofisi zetu. Tunayo nafasi kama viongozi ndani ya umma kuzileta taarifa na ofisi yetu mkaidai matokeo ya taarifa hizo, lakini narudia tena kupitia mfumo wa *HCMIS* tumeendelea kukusanya taarifa za madeni zinazodaiwa ndani ya Serikali na tumeendelea kulipa kutokana na uwepo wa fedha zinazotengwa na bajeti ambayo inapitishwa na Bunge lako.

Mheshimiwa Spika, nataka nilihakikishie Bunge lako, Serikali inayoongozwa na Mama Dkt. Samia Suluhu Hassan, Mheshimiwa Rais wetu ipo kwa ajili ya kuhakikisha haki ya watumishi wa umma inapatikana kwa kulipa madeni yao ndani ya muda. Niendelee kusisitiza tena na kutoa wito kwa waajiri, leteni taarifa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, umesema Wabunge wanaweza kupelekewa hizo taarifa za yale madeni, halafu Wabunge wazilete kwako, ama nimeelewa vizuri?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Spika, labda...

**SPIKA:** Maana umesema kama Bunge itatupendeza ili Bunge sasa lifanye maamuzi kuhusu jambo hilo.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Spika, labda inaweza kuwa Kiswahili changu cha Bagamoyo hakijaeleweka, lakini ninachomaanisha kusema ni kwamba sisi kama Wabunge ni viongozi katika umma wetu. Kwa mfano, yapo madeni ya walimu yaliyozungumzwa hapa, walimu hawa tunafanya nao kazi kwenye Halmashauri zetu, sisi tunaye mtu ambaye ndiyo Mkuu wa Utumishi wa Walimu pale ndani ya Halmashauri yetu kwa mfano Mkurugenzi, ambaye taarifa za watumishi wote na madeni yote anayo yeye.

Mheshimiwa Spika, kupitia yeye zile taarifa tukimwomba au tukamwelekeza azilete kwenye Ofisi ya Katibu Mkuu Utumishi, madeni hayo yote yatatambulika, yatalipwa lakini kama tutakuja Bungeni hapa kila mtu anataarifa zake yeye mwenyewe anavyozijua, kwa kweli tunaweza tukajikuta mwisho wa siku tunaweza tusiutendee umma au ikawa kila siku tukija hapa tunasema taarifa mpya.

**SPIKA:** Sawa, umeeleweka Mheshimiwa ila Serikali inao utaratibu ambao nao wa kupokea hizo taarifa kama ulivyosema kutoka kwa Mkurugenzi. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Spika, ni kweli.

**SPIKA:** Taarifa utakazoletewa hapa na Wabunge kwenye jibu lako nimekusikiliza, sehemu ya kwanza ni hiyo ya Wabunge ya pili umesema kulingana na fedha ambazo zinakuwa zipo kulingana na...

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Spika, bajeti.

**SPIKA:** Kulingana na bajeti ambayo tumetenga.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Spika, ni kweli.

**SPIKA:** Kama hivyo ndivyo, maana yake wapo watu ambao huenda wanadai na Wabunge pengine wameshaleta ofisini na hawajalipwa kwa sababu fedha zao hazijatengwa, ama jibu lako ni kwamba watumishi wote wanaodai fedha zao zipo, yaje tu majina yao watalipwa, jibu lako kati ya hayo mawili ni lipi, kwamba bajeti haitoshi ama ipo tulete tu hayo majina? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Spika, upangaji wa bajeti unaendana na maombi yanayoletwa. Kwa mfano, mwaka huu mmetupitishia bajeti inatokana na maombi ambayo yameletwa kwa taarifa zilizokusanywa. Sasa unaposikia taarifa zinakuja kama mpya ndizo ambazo natoa angalizo au maelekezo ya kwamba Wabunge tusaidiane pia kuzungumza na mamlaka za uajiri ambazo sisi tunafanya nazo kazi.

Mheshimiwa Spika, hapa nimekusudia kuzungumza...

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majina yakiletwa fedha zipo?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Spika, fedha zipo zimeshatengwa kwa ajili ya malipo hayo. *(Makofi)*

**SPIKA:** Haya Waheshimiwa Wabunge pelekeni majina fedha zipo, Serikali ipo tayari kwa ajili ya kuwalipa. Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Waheshimiwa Wabunge, jamani naona kuna minong'ono, Mheshimiwa Naibu Waziri kasema mpeleke majina kama mtakuwa hamjalipwa hayo majina mliyopeleka ndiyo mtakuja hapa ndani muulize. Kwa hiyo, maana yake hayo mambo mnayosema kachukueni kwa Wakurugenzi mpelekeeni Mheshimiwa Waziri halafu madeni yalipwe maana naona mnaendelea na minong'ono tena. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Waziri wa Nchi.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE NA URATIBU:** Mheshimiwa Spika, tunapokea maelekezo ya kiti chako lakini niendelee tu...

**SPIKA:** Ngoja Mheshimiwa Waziri niliweke sawa, hili sikukusudia mimi kutoa maelekezo, ndiyo maana nilikuwa namwuliza Mheshimiwa Waziri ajibu na amejibu yeye sasa na nimemwongoza kasema fedha zipo. Kwa hivyo siyo maelekezo ya Bunge, ni Serikali imesema fedha zipo watu walete majina, siyo Bunge limeelekeza kwenye hili, karibu Mheshimiwa. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE NA URATIBU:** Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, naomba kuwaomba Waheshimiwa Wabunge, Serikali kupitia mjadala huu wa leo tutakachoweza kukifanya baada ya kupokea majina hayo ni kufuatilia sasa katika mamlaka husika kuona ni makundi yapi ambayo yamekuwa na changamoto labda za muda mrefu, kwa sababu tunachojua ni kwamba fedha zinaweza kuwa zipo, lakini wakati mwingine waajiri na wasimamizi wa watumishi wamekuwa wakifanya ndivyo sivyo katika kuhakikisha kwamba

madai ya watumishi yanalipwa kwa kuzingatia mifumo na taratibu tulizoziweka.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo tutashirikiana na Wabunge na Serikali itatekeleza majukumu yake ili mradi tu lengo letu ni kuona mwisho wa siku watumishi ambao wamekuwa wakiidai Serikali kwa kuzingatia mifumo na taratibu tulizoziweka wanapatiwa ufumbuzi wa madai yao. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Wizara ya Nishati, Mheshimiwa Jesca David Kishoa, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 443

**Makubaliano ya Mkataba wa *SONGAS***

**MHE. JESCA D. KISHOA** aliuliza:-

Je, makubaliano ya mkataba ujao kati ya *SONGAS* na Serikali yamefikia hatua gani ikiwa mkataba wa awali upo katika mwaka wa mwisho?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati, Mheshimiwa Judith Kapinga, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, Mkataba wa ununuzi wa umeme kati ya *TANESCO* na *SONGAS* unafikia ukomo wake tarehe 31 Julai, 2024. Kwa sasa, Serikali imeunda Timu ya Wataalam (*Government Negociation Team - GNT)* iliyoanza majadiliano mwezi Aprili, 2023 na inatarajia kukamilisha majadiliano haya kabla ya mkataba kuisha. Serikali itahakikisha maslahi ya Taifa yanazingatiwa kabla ya makubaliano yatakayofuata. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Jesca Kishoa, swali la nyongeza.

**MHE. JESCA D. KISHOA:** Mheshimiwa Spika, taarifa za *CAG* pamoja na Kamati za Kudumu za Bunge toka mwaka 2009

zimekuwa zikieleza mapungufu makubwa yaliyopo kwenye mkataba wa *SONGAS*, nataka kujua Serikali ilishachukua hatua gani kwa *GNT* (*Government Negotiation Team)* ya wakati huo ili ya sasa *Government Negotiation Team* isifanye makosa yale.

Mheshimiwa Spika, swali la pili, chanzo cha Tanzania kupata alama ya chini kwenye tathmini ya *EIT* ya mwaka 2023 ni kutokana na mikataba kutowekwa wazi kinyume na sheria ya Tanzania *Extractive Industry Transparency Act* ya Mwaka 2015. Nataka kujua Serikali ni lini mtaleta mkataba huo Bungeni, sisi kama Wabunge tuujadili kabla ya kuusaini. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, nimshukuru Mheshimiwa Mbunge kwa maswali yake mawili ya nyongeza, kwanza kuhusiana na hii timu ya wataalamu. Mwaka jana mwezi Aprili timu ya wataalam iliundwa na walipewa jukumu la kuchambua mikataba yote ya Mradi wa *SONGAS* ikihusisha mikataba ya msingi *(basic agreements)* vilevile mikataba ya fedha *(financial agreements)*.

Mheshimiwa Spika, ilivyofika mwezi Disemba tulianza majadiliano, nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge na Bunge lako hili Tukufu kwamba, timu hii ya wataalamu ambayo imewekwa kwa ajili ya majadiliano ya nyongeza ya mkataba wa mauziano ya umeme kati ya *TANESCO* na *SONGAS* na mikataba mingine ambayo inahusiana. Ni timu ya wataalamu wenye weledi mkubwa sana na imehusisha maeneo yote ya msingi, lengo kuu ni kuhakikisha hatufanyi makosa yoyote tunapoenda kwenye mikataba ya namna hii.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na suala la pili la mikataba kuwa wazi, kwa sababu sasa hivi hatujafahamu kama tutaendelea na mkataba huu ama hatutaendelea na mkataba huo, inaniwia vigumu kusema ni lini tutaleta mkataba huo Bungeni lakini nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, *section* 16 ya Sheria ya *Extractive Industry* ni kweli inataka uwazi kwenye mikataba na leseni za sekta ya uziduwaji na sisi kama Serikali tunahakikisha

mara zote tunaenda kwa mujibu na matakwa ya sheria hizo. Kwa hiyo nimhakikishie kama tutafikia hatua hiyo basi tutawajibika kulingana na sheria. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Yahaya Omary Massare, Mbunge wa Manyoni Magharibi, sasa aulize swali lake.

Na. 444

**Gharama za Kuunganishiwa Umeme**

**MHE. YAHAYA O. MASSARE** aliuliza:-

Je, lini Serikali itarejesha gharama za kuunganishiwa umeme kuwa 177,000?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kulingana na bei za umeme zilizopitishwa na *EWURA*, gharama za kuunganisha umeme wa njia moja katika maeneo ya vijijini ni shilingi 27,000 na mijini shilingi 320,960. Kwa kipindi cha nyuma, kwa miradi ya vijijini *(REA)* ilikuwa inatoza shilingi 27,000 na *TANESCO* shilingi 177,000.

Mheshimiwa Spika, kutokana na malalamiko ya wananchi ya utofauti wa bei kati ya *REA* na *TANESCO* ya kuunganisha umeme vijijini, Serikali iliamuru *TANESCO* kushusha bei ya kuunganisha umeme vijijini na kuwa 27,000 kama *REA* na tofauti ililipwa na Serikali kama ruzuku kwa *TANESCO*. Kwa hali hiyo, bei ya shilingi 177,000 iliyokuwa inatozwa na *TANESCO* vijijini, ilifutwa na kuwa 27,000 kwa vijijini kama ilivyo sasa, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Yahaya Massare, swali la nyongeza.

**MHE. YAHAYA O. MASSARE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, pamoja na majibu mazuri ya Serikali nina maswali madogo mawili ya nyongeza.

Swali la kwanza; umeme ni maisha na sasa watu wanatumia umeme kufanya mambo yao yaende vizuri, sasa lakini kutoka shilingi 320,000 kwa vijiji ambavyo ni vidogo, ambavyo wamevionesha kama ni vijiji mji.

Je, Serikali ipo tayari sasa vile vijiji vidogo vilivyokusanyika pamoja kama vijiji vya Itigi ambavyo ni vijiji saba kwa pamoja, Kijiji cha Mitundu, viwalipe 27,000?

Mheshimiwa Spika, swali la pili; wananchi wanapolipa hizo gharama za kuunganishiwa umeme Serikali inachukua muda mrefu sana. Je, Serikali inasemaje, ni muda gani mahsusi, mtu akishalipia umeme anakuwa anajua kwamba atafungiwa mita? Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, nimshukuru Mheshimiwa Mbunge kwa maswali mawili ya nyongeza.

Swali la kwanza kuhusiana na gharama kwenye maeneo ya vijiji mji, Serikali tumeshaanza kufanya mapitio kwenye maeneo ambayo tunadhani yanatakiwa kupunguziwa gharama kutoka 320,960 hadi shilingi 27,000.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa tumeshaainisha maeneo 1,500 na kwa hiyo nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge hiki Kijiji alichokisema na vijiji vingine vya Itigi pia vimepitiwa. Tutaenda kufanya mapitio zaidi ili kuona kama hicho Kijiji ambacho Mheshimiwa Mbunge amekitaja kinaweza kuingia katika mapitio haya.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na kuunganisha umeme tunaendeleza kuboresha huduma kuhakikisha wananchi wanaunganishiwa umeme kwa wakati. Suala la kuunganisha umeme lina sehemu mbili yaani mwananchi kufanya *wiring* na sisi kisha kupeleka huduma ya kuunganisha umeme. Tuendelee kuwasisitiza wananchi pale ambapo huduma ya umeme inafika kwenye maeneo yao waweze kufanya *wiring* kwa wakati na sisi

tutaendeleza kuboresha huduma ili kuhakikisha huduma ya kuunganisha umeme kwa wananchi inakuwa ya haraka na ya uhakika, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Maji, Mheshimiwa Boniphace Mwita Getere, Mbunge wa Bunda, sasa aulize swali lake.

Na. 445

**Ujenzi wa Mabwawa ya Maji – Bunda**

**MHE. BONIPHACE M. GETERE** aliuliza:-

Je, lini Serikali itakamilisha ujenzi wa Mabwawa ya Maji ya Salama A, Rakana, Mihingo, Tingirima, Kambubu na Nyaburundu – Bunda?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, Mheshimiwa Mhandisi Kundo, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Boniphace Mwita Getere, Mbunge wa Jimbo la Bunda, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali katika Mwaka wa Fedha 2024/2025 imetenga fedha kwa ajili ya kumalizia ujenzi wa bwawa la Mihingo ambapo hadi sasa utekelezaji wake umefikia asilimia 95. Vilevile, Serikali inakarabati Bwawa la Salama A sambamba na kufanya usanifu wa kina wa Bwawa la Tingirima.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Mabwawa ya Kambubu, Nyaburundu na Rakana, katika Mwaka wa Fedha 2024/2025, Serikali itafanya mapitio ya usanifu zilizowahi kufanyika katika mabwawa hayo pamoja na kufanya tathmini ya athari za

kimazingira na kijamii. Lengo ni kujiridhisha na mawanda ya mradi na kulipa fidia kwa waathirika watakaopitiwa na miundombinu ya mradi kabla ya kuanza utekelezaji wake.

Mheshimiwa Spika, mapitio hayo ya usanifu yatasaidia kubainisha kama maeneo hayo yanafaa kujengwa bwawa kati ya moja au mawili makubwa yatakayohudumia vijiji vyote kwa kutumia mitambo iliyonunuliwa na Serikali.

**SPIKA:** Mheshimiwa Boniphace Mwita Getere, swali la nyongeza.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu hayo ya Serikali, nina maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; Bwawa la Mihingo ilikuwa lichimbwe na mkataba wake ulikuwa ni mwaka mmoja, sasa ni miaka mitano toka limeanza kuchimbwa, hali yake bahati nzuri viongozi wote wa Wizara wameshafika pale wameona hali yake. Sasa walisema miezi sita ijayo litakuwa limemalizika na miezi sita imepita. Sasa ni lini watamaliza hilo Bwawa la Mihingo ili kuondoa kero kwa wananchi wa Mihingo?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, Mabwawa ya Rakana, Salama A, Tingirima, Kambubu na Nyaburundu yalishafanyiwa usanifu muda mrefu tu na michoro yote mnayo na kwa kuwa tunayo mitambo Mkoa wa Mara, ni lini sasa watapeleka mitambo kumaliza mabwawa haya? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Bwawa la Mihingo kama ambavyo nimejibu katika majibu ya msingi ni kweli limefikia katika 95% na Serikali imejipanga kwenda kuhakikisha kwamba bwawa hili linaisha.

Mheshimiwa Spika, swali la pili, katika Mabwawa ya Rakana vilevile kama ambavyo nimejibu katika majibu ya msingi kuwa usanifu kama ambavyo Mheshimiwa Mbunge kweli amekiri ulifanyika siku nyingi, kawaida katika mambo ya ujenzi wa mabwawa ukishafanya usanifu na muda mrefu ukapita hamjatekeleza maana yake mnaanza kupitia kuona kwamba mahitaji kama bado yapo vilevile na kama yamebadilika basi na kuhusiana na masuala ya fidia ili waweze kulipwa watu wanaostahili kulipwa fidia na ili mradi uweze kuanza. Kwa hiyo nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge eneo hili tumejikita, tumejizatiti kuhakikisha kwamba mradi huu utaanza baada ya mapitio ya usanifu, ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea na Wizara ya Afya, Mheshimiwa Taska Restituta Mbogo, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 446

**Kukamilisha Ujenzi wa Wodi Hospitali ya Rufaa Mkoa wa Katavi**

**MHE. TASKA R. MBOGO** aliuliza:-

Je, lini ujenzi wa jengo la Mama na Mtoto, Wodi ya watoto na wodi ya wanaume Hospitali ya Rufaa Mkoa wa Katavi utakamilika?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya, Mheshimiwa Dkt. Godwin Mollel, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, Serikali imetenga kiasi cha shilingi bilioni tano kwa ajili ya ukamilishaji wa jengo la Mama na Mtoto, wodi ya watoto na wodi ya wanaume katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Katavi lenye sehemu mbili ambazo ni *Wing A* na *Wing B*. Aidha eneo la *Wing A* limekamilika kwa 98% ambapo tayari linatumika

kwa huduma za wagonjwa wa nje na huduma za Radiolojia na eneo la *Wing B* limefikia 20% na ujenzi unaendelea. Naomba kuwasilisha.

**SPIKA:** Mheshimiwa Taska Mbogo, swali la nyongeza.

**MHE. TASKA R. MBOGO:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu ya Serikali ninayo maswali mawili ya nyongeza. Kwanza, tunaishukuru Serikali kwa ujenzi wa hospitali, lakini hospitali imechukua muda mrefu takribani miaka saba haijakamilika. *Wing B,* ni eneo ambalo kuna *theatre* ya kisasa, kuna jengo la mama na kuna jengo la mtoto na sasa hivi wanatumia lile jengo la *ICU*. Swali la kwanza; je, ni nini kauli ya Waziri baada ya bajeti kupata hizo shilingi bilioni tano ili jengo hili liweze kukamilika? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili; wakati Waziri ananijibu swali mara ya mwisho hapa Bungeni, aliniahidi *ambulance* kwenye Hospitali ya Mkoa wa Katavi. Je, niwasiliane na uongozi wa Hospitali ya Mkoa, waweze kumtuma dereva aje kuchukua hiyo *ambulance? (Makofi/Kicheko)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, kwanza, kauli yangu moja ni kumpongeza Mbunge kwa sababu toka *zero* amekuwa pamoja na sisi na anajua miaka mitano iliyopita walikuwa hawana kabisa Hospitali ya Mkoa. Leo wana Hospitali ya Mkoa ambayo anaizungumzia majengo kumaliziwa na ameona mengine 98% mengine 20%. Nimhakikishie kwamba, litaenda kwisha.

Mheshimiwa Spika, swali lake la pili, la *ambulance,* kuna *ambulance* 47, ambazo zipo njiani zinakuja. Nimwombe asiwasiliane na hospitali walete, lakini mimi na yeye tukae nimkabidhi kwa mtaalamu anayegawa *ambulance* ahakikishe yeye mwenyewe kwamba zitakapofika ya Katavi iweze kuwekwa. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Rehema Juma Migilla, Mbunge wa Ulyankulu, sasa aulize swali lake.

Na. 447

**Kufutwa kwa Toto Afya Kadi**

**MHE. REHEMA J. MIGILLA** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwasaidia watoto kupata matibabu baada ya kufuta Toto Afya Kadi huku tukisubiri Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, mfumo wa kulipia bima za watoto kupitia Toto Afya Kadi umebadilika na kwa sasa unafanyika kupitia utaratibu wa shule na vifurushi vya bima ya afya vya najali, wekeza na timiza ambapo wanajiunga kupitia wazazi wao.

Mheshimiwa Spika, kuanza kwa utekelezaji wa Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote utawezesha makundi mbalimbali ya wananchi wakiwemo watoto kupata huduma za afya kwa urahisi pasipo kuwa na vikwazo, naomba kuwasilisha.

**SPIKA:** Mheshimiwa Rehema Juma Migilla, swali la nyongeza.

**MHE. REHEMA J. MIGILLA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu ya Serikali, nina maswali mawili ya nyongeza.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge, unamkatisha anayezungumza. Mheshimiwa Mbunge.

**MHE. REHEMA J. MIGILLA:** Mheshimiwa Spika…

**SPIKA:** Subiri kwanza Mheshimiwa. Mheshimiwa, tafadhali rejea kule nyuma utarejea mbele baadaye kidogo. Mheshimiwa

Mbunge, anayezungumza yupo mbele yako. Rejea uliko kuwa, ahsante sana.

Mheshimiwa Rehema.

**MHE. REHEMA J. MIGILLA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Serikali nina maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; kwa kuwa mfumo wa bima ya afya kwa wote haujaanza kutumika na watoto wetu wanaendelea kuugua. Je, Serikali kwa sasa kwa nini isione kuna haja ya kuendelea kulipia ile shilingi 50,400 kwa watoto wetu ambao wapo chini ya miaka 18 ambao walikuwa wanajisajili kule bima? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunafahamu kabisa wazazi wengi hawana uwezo wa kulipia bima hiyo ya najali na wekeza, lakini wana uwezo wa kulipia hiyo shilingi 50,000 au kuongeza kiwango kidogo kwa ajili ya matibabu ya watoto wao. Je, kwa nini Serikali haioni sasa…

**SPIKA:** Umeshauliza hilo swali la kwanza. Hilo sasa unarejea linakuwa la pili. Sasa nenda kwenye la pili usirejee la kwanza ulilouliza. *(Makofi/Kicheko)*

**MHE. REHEMA J. MIGILLA:** Mheshimiwa Spika, swali langu la pili; tunafahamu kabisa Sera ya Afya inasema watoto chini ya miaka mitano wanatibiwa bure, sasa hivi wazazi wengi wamekuwa watoto wao wakiugua chini ya miaka mitano anabeba mtoto wake mgongoni na kumpeleka hospitali yoyote ambayo ipo karibu na yeye.

Mheshimiwa Spika, wakifika kule anakuwa hana hata barua ya rufaa kwenye hiyo hospitali na akifika pale mtoto hatibiwi mpaka awe na barua ya rufaa. Je, hawa wahudumu wetu wa afya wanamwona kabisa mtoto yupo chini ya miaka mitano, lakini hawamtibu eti mpaka awe na barua ya rufaa hatuoni kama tuna mpango watoto wetu wafe? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, kwanza, nimpongeze Mheshimiwa Mbunge kwa maswali yake mazuri. Moja, kwanza atambue imeshakuwa ni zaidi ya miaka 18 ni watoto kuanzia miaka 21 kurudi chini ndio waliokuwepo kwenye huo utaratibu. Pia, ajue tu Mheshimiwa Mbunge, kwenye nchi hii ukipiga hesabu miaka 21 mpaka kurudi chini sifuri wapo kama watoto 30,700,000.

Mheshimiwa Spika, wale waliopo kwenye Toto Afya Kadi walikuwa 200,000 tu maana yake unaweza kuona kwamba, pamoja tunazungumzia hawa 200,000 waliokuwepo kwenye Toto Afya Kadi, lakini kuna watoto zaidi ya 30,700,000 wapo ambao wamekuwa wakiendelea na wakipata huduma kama kawaida.

Mheshimiwa Spika, nimwambie tu Mheshimiwa Mbunge kufanya kwamba, sasa huu mpango mpya haujaondoa shilingi 50,400 bado ni shilingi 50,400. Kilichobadilika sasa wanaingia kwa makundi ili tuweze kutimiza zile taratibu na sheria ambazo zinatakiwa kwenye bima ya afya ili kuulinda mfuko. Kwa sababu kama ambavyo tumeshasema hapa Bungeni walikuwa wanachangia shilingi bilioni tano wanatumia shilingi bilioni 49 maana yake walikuwa wanatumia hela za watumishi wa umma, wanatumia hela za watu wengine ambao walishachangia. Mwisho wa siku, tunaweza tukawatibu tukajikuta tunakosa kusaidia wengine; hilo ni moja.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili, nikwambie tu Mheshimiwa Mbunge, kwamba, kupitia taratibu nyingine na njia nyingine ambao hawa 30,000,000 wanapata huduma na hawapigi kelele pamoja na hiyo ya Toto Afya Kadi ambayo ni mpya. Nataka kumhakikishia Mbunge kwamba, Serikali itaendelea kutoa huduma na hao watoto hawatapata shida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali lake la pili ni kwamba, kuna watoto chini ya miaka mitano. Ni kweli kumekuwepo na shida sehemu mbalimbali kuhusu watoto chini ya miaka mitano. Ni kweli hiyo huduma inatakiwa iwepo bure, lakini hatujaweza kutoa kwa 100%, lakini zaidi ya 70% wamekuwa wakisaidiwa. Bado kuna

asilimia fulani ambayo haijaweza kupata hiyo bure kama inavyosema.

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na shida kama unavyosema mtoto ambaye anaumwa tu kifua na kikozi tu, lakini unashangaa ameshapelekwa mpaka hospitali ya mkoa. Mara nyingi wataalamu wetu wanapenda kusisitiza waanze huku chini, kwa sababu kuna magonjwa mengine yanaweza yakatibiwa kwenye zahanati na vituo vya afya hakuna sababu ya kwenda kwenye hospitali za mikoa.

Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii kuwaambia waganga wetu wafawidhi wa Hospitali za Wilaya, Hospitali za Mikoa na hospitali nyingine watoto wanaotoka kwenye maeneo yaliyozunguka hospitali zetu wapokelewe na wahudumiwa kulingana na miongozo na taratibu za Serikali zinavyotaka. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, hao 30,000,000 ni watoto wa chini ya miaka mitano au 30,000,000 wanaohudumiwa na hospitali? Washa kisemeo.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, nachosema ni kwamba, ukienda kwenye Sensa yetu ukiiangalia, watu chini ya miaka 21 kurudi chini utaona …

**SPIKA:** Ndio wapo 30,000,000 na siyo hawa wadogo wa chini ya miaka mitano?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, ndiyo. Siyo hawa chini ya miaka mitano.

**SPIKA:** Haya. Ahsante sana, umeeleweka.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, ndio waliotakiwa kupata Toto Afya Kadi, lakini wamekuwa wakihudumiwa tu vizuri, kwa sababu waliopo kwenye Toto Afya Kadi ni 200,000 tu lakini hawa ndio 200,000 wanapigiwa kelele zaidi ya hawa 30,000,000 ambao wanahudumiwa vizuri na Serikali.

**SPIKA:** Haya ahsante sana. Mheshimiwa Shally Josepha Raymond, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 448

**Kampeni ya Kuhamasisha Kunawa Mikono Kuepuka Magonjwa Ambukizi**

**MHE. SHALLY J. RAYMOND** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuendeleza Kampeni ya kunawa mikono ili kudhibiti magonjwa ambukizi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, Serikali imefanya uzinduzi wa Kampeni ya Mtu ni Afya kwa awamu ya pili ambapo inahimiza kuhusu kujengo vyoo bora, lishe bora, udhibiti wa taka, udhibiti wa magonjwa yasiyoambukiza sambamba na unawaji wa mikono kwa maji na sabuni.

Mheshimiwa Spika, kampeni hii imezinduliwa tarehe 9 Mei, 2024 na Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kutekelezwa kwake kutawezesha kudhibiti magonjwa ambukizi katika jamii.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**SPIKA:** Mheshimiwa Shally Raymond, swali la nyongeza.

**MHE. SHALLY J. RAYMOND:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa uzinduzi wa hii kampeni ni juzi tu mwezi huu, lakini kabla ya hapo mlipuko wa *COVID-19* ulikuwa umeleta aina fulani ya hali ya juu ya usafi katika nchi yetu. Maji yalikuwepo kila mahali ya kunawia mikono katika misikiti, kanisani, shuleni na hata hapa Bungeni. Jambo hilo limeisha tu baada ya kutangazwa *COVID* imekwisha.

Swali la kwanza; je, Serikali ina mpango gani wa kusimamia na kuona kwamba, usafi ule unarejeshwa mara moja? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili; kwa kuwa tabianchi inaleta mafuriko na maji mengi yanatiririka, maradhi mengi yanatokea yasiyo ambukizwa ikiwemo kipindupindu. Serikali ina mpango gani kuweka mafunzo kila mahali ambayo yatadhibiti usafi na kuona kwamba, ni mwendelezo na tabianchi yetu? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, kwanza, nianze kwa kuwashukuru wanawake wa Mkoa wa Kilimanjaro, kwa sababu kwa kweli wametuletea mama yetu ambaye sisi Waheshimiwa Wabunge wa Mkoa wa Kilimanjaro ni mama, ni dada na ni mshauri mzuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi nijibu maswali yake mawili; moja, hili la kwamba, wakati wa *COVID* tulikuwa kwa kweli na tabia nzuri ya kunawa mikono na kuzingatia usafi wetu kuanzia kunawa kwa maji, lakini kutumia *sanitizer* na vitu vingine. Mimi nitumie fursa hii kuwaomba Waheshimiwa Wabunge na Watanzania wote kwamba, hiyo tabia tuliyokuwa nayo mwanzo tuendelee nayo.

Mheshimiwa Spika, niombe, kwa sababu hapa Bungeni na sisi sasa tuwe wa mwanzo kwanza kurudisha hiyo tabia ndani ya Bunge haraka haraka. Wakati huko kwenye taasisi tukifanya mawasiliano kwa kushirikiana na wenzetu wa Wizara tofauti tofauti tuendelee na hiyo tabia kwa pamoja. Hiyo ni moja.

Mheshimiwa Spika, swali lake la pili la kwamba, sasa hivi kuna mafuriko. Ni kweli mafuriko yanapokuwepo maji yanapokuwa yametuama kuna magonjwa mbalimbali ambukizo ambayo yanaenda kutokea ikiwepo malaria na mambo mengine. Nimhakikishie Mbunge kwamba, Serikali ipo macho kwa ajili hiyo ndiyo maana unaona vifo vya watoto kwenye eneo la malaria haviongezeki. Pia, husikii milipuko ya kipindupindu na vitu vingine pamoja na matatizo yote yanayotokea ambayo unayasikia sehemu mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, Serikali imekuwa ikielekea upande huo na kuhakikisha inazingatia ushauri ambao umeusema. Ninachotaka kuhakikisha kutoka hapa Bungeni nitumie fursa hii kuwaomba wataalamu wetu kuanzia zahanati zetu, vituo vyetu vya afya na kila mahali tuongeze nguvu kwenye eneo kama ambavyo umeshauri tuendelee kuongeza nguvu na tusirudi nyuma. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea na Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Mheshimiwa Mussa Omar Salim, Mbunge wa Gando, swali lake litaulizwa kwa niaba yake na Mheshimiwa *Engineer* Ezra Chiwelesa.

Na. 449

**Mfumo wa *Cyber* Kuwa Chini ya Jeshi la Polisi**

**MHE. ENG. EZRA J. CHIWELESA K.n.y. MHE. SALIM MUSSA OMAR** aliuliza:-

Je, Serikali haioni haja ya kuhamishia Mfumo wa *Cyber* kuwa chini ya udhibiti wa Jeshi la Polisi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Mhandisi Maryprisca Mahundi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, ahsante, mkakati wa Taifa wa Usalama umeweka malengo na mpango wa kimkakati wa nchi kuhakikisha ulinzi na usalama wa anga yetu ya mtandao *(cyber space)*. Ndani ya Mkakati huo, taasisi zote zinazohusika na ushughulikiwaji wa makosa ya mtandao zimetambuliwa na majukumu yao kuwekwa bayana ili kuwepo utaratibu mzuri wa kushirikiana.

Mheshimiwa Spika, *Tanzania Computer Emergency Response Team,* Jeshi la Polisi, Ofisi ya Taifa ya Mashtaka, Mamlaka ya Serikali Mtandao na vyombo vingine vya ulinzi na usalama kwa pamoja zinashirikiana kusimamia masuala ya ushughulikiwaji wa makosa ya mtandao.

Mheshimiwa Spika, suala la ushughulikiwaji wa anga ya mtandao kwa maana ya *(cyber)* ni mtambuka na haliwezi kutekelezwa kwa ufanisi na taasisi moja hivyo ni muhimu taasisi hizo ziendelee kutekeleza usimamizi huo kwa kushirikiana na kwa utaratibu jumuishi ili kuongeza tija katika jukumu hilo. Hata hivyo, Serikali ipo tayari kupokea ushauri utakaowezesha kuboresha usalama wa matumizi ya mtandao hapa nchini. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Mhandisi Ezra Chiwelesa, swali la nyongeza.

**MHE. ENG. EZRA J. CHIWELESA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali. *Idea* ya Mheshimiwa Mbunge, mpaka kuuliza swali hili ni kwamba, sisi kama viongozi na kama Waheshimiwa Wabunge ni mashahidi wa mambo ambayo yanaendelea huko mitandaoni.

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na utapeli mkubwa sana kwa wananchi, lakini kwa sehemu kubwa watu wanaporipoti taarifa zimekuwa zinahitajika zitumwe *TCRA* na *TCRA* ndio waweze kurudisha polisi. Sasa hicho kitendo kinachukua muda sana, kwa sababu unavyoongelea utapeli leo hatuongelei wale watu waliopo mijini au kwenye majiji makubwa. Utapeli unafika mpaka vijijini na sehemu ambazo hakuna hata hayo mawasiliano saa nyingine inachukua muda mrefu sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa mchango umetosha. Swali.

**MHE. ENG. EZRA J. CHIWELESA:** Mheshimiwa Spika, sasa swali. Je, hatuoni kwamba, ili kuweza kuboresha mawasiliano na kusaidia Watanzania ambao wanapata dhuluma baadhi ya majukumu hasa ku-*access information* za wahalifu zingewekwa kwenye majeshi ya polisi tu ili mtu anapoibiwa polisi waweze

kupata *access* ya haraka kumhudumia kuliko kuanza kupeleka *information* mpaka zirudi huku?

Mheshimiwa Spika, ahsante sana, ni swali moja tu hilo. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Spika, ahsante, ninaomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mussa kupitia Mwakilishi wake Mheshimiwa *Engineer* Chiwelesa.

**SPIKA:** Ngoja. Hamwakilishi yeye ameuliza kwa niaba yake. Kwa hivyo, unamjibu yeye, kwa sababu hili ni swali la nyongeza, unamjibu yeye. *(Kicheko)*

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Spika, ahsante, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa *Engineer* Ezra, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, ni kweli sisi kama Wizara tunafahamu hili na tunalishughulikia kwa umakini sana. Kwa taarifa tu Tanzania ni nchi ya pili Afrika katika usalama wa kimtandao. Hii inaonesha Wizara ipo makini na tunashughulikia haya yote ambayo yanaendelea mitandaoni.

Mheshimiwa Spika, Jeshi la Polisi tumelipa hii kazi kupitia *Unit* yake ya *Cyber Crime Unit*. Kwa hiyo, si kwamba, Jeshi la Polisi halishughuliki moja kwa moja, lakini maboresho tutaendelea kuyafanya kadri ya ushauri mzuri ambao Waheshimiwa Wabunge, wanaendelea kutupatia.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Sasa ni Wizara ya Viwanda na Biashara. Mheshimiwa Janeth Elias Mahawanga, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 450

**Mkakati wa Kukuza Wajasiriamali Wadogo**

**MHE. JANETH E. MAHAWANGA** aliuliza:-

Je, upi Mkakati wa Serikali kuhakikisha wajasiriamali wadogo wanakuwa sehemu ya wawekezaji wa ndani kupitia shughuli zao?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa niaba ya Wizara ya Viwanda na Biashara. *(Makofi/Kicheko)*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA K.n.y. WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Janeth Elias Mahawanga, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, uwekezaji ni dhana pana ambayo imegawanyika katika kundi la uwekezaji mdogo sana, mdogo, wa kati na mkubwa. Hivyo, wajasiriamali wadogo ni sehemu ya wawekezaji wa ndani wanaotoa mchango mkubwa katika uchumi kwa kutoa ajira na kukuza kipato cha mtu binafsi na Taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, mkakati wa Serikali ni kuendelea kutoa huduma mbalimbali kwa wajasiriamali wadogo ikiwemo mafunzo ya ujasiriamali, mikopo ya riba nafuu, kujenga miundombinu ikiwemo majengo/mitaa ya viwanda na biashara, kuwapatia nembo ya ubora na kuwatafutia masoko kupitia taasisi za *CBE, SIDO, TBS* na *TANTRADE*. Huduma zote hizi zinawasaidia wajasiriamali kukua na hatimaye kuwa wawekezaji wakubwa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Janeth Mahawanga, swali la nyongeza.

**MHE. JANETH E. MAHAWANGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Serikali, nina maswali mawili madogo ya nyongeza. Swali la kwanza; ni lini *SIDO* itaanza kujiendesha kibiashara ili kukidhi mahitaji ya wajasiriamali wadogo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili; ni upi mpango wa Serikali katika kuboresha sera ya biashara na sera ya wajasiriamali wadogo ili ziendane na soko la ndani na mahitaji ya wajasiriamali? Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA K.n.y. WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Spika, lini *SIDO* itaanza kujiendesha kibiashara? Katika mwaka wa fedha 2023/2024, Serikali imeainisha maeneo ya miradi ya kimkakati na tayari katika baadhi ya maeneo vibali kwa ajili ya uanzishwaji wa maeneo hayo kwa kupitia Msajili wa Hazina vimeshakwishaombwa. Pili, maandiko mbalimbali kwa ajili ya uanzishwaji wa miradi ikiwemo kongani za viwanda nayo pia ni moja ya mkakati ambao umepangwa kutekeleza azma hiyo.

Mheshimiwa Spika, pili kuhusiana na sera; Serikali imeendelea kuboresha Sera ya Taifa ya Biashara na sasa tulipo tumekwishapeleka Sera hiyo katika Baraza la Mawaziri na Baraza limeridhia na sasa tupo katika hatua za mwisho kwa ajili ya uzinduzi wa sera hizo ili kuendana na mahitaji ya sasa katika ujasiriamali.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea na Wizara ya Ujenzi, Mheshimiwa Hussein Nassor Amar, Mbunge wa Nyang'hwale swali lake litaulizwa; Waheshimiwa, nawaona wawili. Nani mwenye majibu yanayotoka kwa Mheshimiwa Mbunge, mwenye swali?

**MHE. TUMAINI B. MAGESSA:** Mheshimiwa Spika, nipo hapa.

**SPIKA:** Sawa, Waheshimiwa Wabunge Mheshimiwa Hussein Amar, Mbunge wa Nyang'hwale swali lake litaulizwa kwa niaba yake na Mheshimiwa Tumaini Bryceson Magessa.

Na. 451

**Ujenzi wa Barabara ya Kharumwa**

**MHE. TUMAINI B. MAGESSA K.n.y. MHE. HUSSEIN N. AMAR** aliuliza: -

Je, lini ujenzi wa Barabara ya Kharumwa yenye urefu wa kilometa moja ya kiwango cha lami utakamilika?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa ujenzi, Mheshimiwa Innocent Bashungwa, majibu.

**WAZIRI WA UJENZI** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Hussein Nassor Amar, Mbunge wa Nyang'hwale, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya Wingi 3 - Kharumwa – Nyang'holongo yenye urefu wa kilometa 68, sehemu ya Kharumwa yenye urefu wa kilometa moja umefikia 75% na unatarajiwa kukamilika mwishoni mwa mwezi Juni, 2024.

**SPIKA:** Mheshimiwa Tumaini Bryceson Magessa, swali la nyongeza.

**MHE. TUMAINI B. MAGESSA:** Mheshimiwa Spika, kwanza niipongeze Serikali, kwamba kuna maendeleo mazuri kwenye barabara hii. Pamoja na majibu mazuri ya Serikali nina maswali mawili ya nyongeza.

Swali la kwanza; je, ni lini usanifu na upembuzi yakinifu wa barabara kutoka Busisi, Busolwa, Ijundu kuelekea Kahama utakamilika?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, je, Serikali ina mkakati gani wa ujenzi wa barabara kutoka Katoro Jimboni Busanda kuelekea Ushirombo Jimboni Bukombe? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, majibu

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, ninaomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Tumaini Magessa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza, kwamba ni lini usanifu wa barabara kutoka Busisi, Ijundu kuelekea Kahama utafanyika; kwa kipande hiki cha barabara kutoka Mwanza kuelekea Geita tayari tumekwishampata mkandarasi na usanifu umeanza. Kwa vile barabara hii ina kipande cha kuelekea upande wa Kahama nimwahidi Mheshimiwa Mbunge kwamba tutafanya haraka iwezekanavyo ili tupate mkandarasi wa kufanya usanifu wa hiki kipande cha upande wa Geita ambacho kimebaki.

Mheshimiwa Spika, kuhusu swali la pili Barabara ya Katoro – Ushirombo, nimwahidi Mheshimiwa Mbunge fedha itakapopatikana barabara hii tutaijenga kwa kiwango cha lami, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Oliver Semuguruka, swali la nyongeza.

**MHE. OLIVER D. SEMUGURUKA:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru sana kwa kuniona. Je, Barabara ya Omgakolongo - Kigalama mpaka Mlongo inayounganisha Wilaya mbili za Karagwe na Kyerwa imefikia wapi kujengwa kwa kiwango cha lami, maana ni ahadi ya muda mrefu? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Semuguruka, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, barabara aliyoitaja ya Omgakolongo kutoka Karagwe kuelekea Kyerwa mpaka Mlongo ni barabara

ambayo hata mimi ninaifahamu, ipo jimboni kwangu pamoja na kwa Mheshimiwa Innocent Bilakwate. Tupo katika hatua ya manunuzi ya kumpata mkandarasi na mara tu baada ya kumpata mkandarasi tutaanza kujenga barabara hii kwa kiwango cha lami. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge mmesimama wengi na ninawaona, lakini muda wetu hautoshi. Mheshimiwa Subira Mgalu, swali fupi.

**MHE. SUBIRA K. MGALU:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwa kuwa Serikali imekwishaanza kutangaza kazi za ujenzi wa kilometa tano kwa ajili ya wakandarasi wanawake na kazi imefanyika Mkoa wa Songwe. Je, anatupa matumaini gani, kwamba jambo hili litakuwa endelevu? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, majibu kwa kifupi.

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Subira Mgalu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza niendelee kumpongeza kwa namna ambavyo anawapambania wakandarasi wanawake. Nimwondoe wasiwasi, kwenye bajeti ya Wizara ya Ujenzi ambayo nitakayowasilisha kesho kutwa tunayo mikakati kabambe kwa ajili ya wakandarasi wanawake. Si hizi kilometa tano tu, tunazo kilometa nyingi ambazo tumezi-*earmark* kwa ajili ya kutekelezwa na wakandarasi wanawake. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Kilumbe Shabani Ng'enda, swali la nyongeza.

**MHE. KILUMBE S. NG'ENDA:** Mheshimiwa Spika, ningependa kujua; kipande cha barabara itokayo Malagarasi kwenda Uvinza, kilometa 51, kinasuasua kwa muda mrefu. Je, ni lini Serikali watakamilisha kazi hiyo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Kilumbe Ng'enda, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, ni kweli barabara hii mkandarasi yupo *site* lakini *speed* si ya kuridhisha. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, changamoto ya mkandarasi huyu tumeiwasilisha Hazina. Mara tu baada kupata malipo tutampa mkandarasi ili aweze kuongeza *speed;* lakini pia baada ya Bunge la Bajeti tutaenda huko kwa ajili ya kuweka msukumo ili ujenzi uende kwa kasi.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Fedha, Mheshimiwa Martha Nehemia Gwau, Mbunge wa Viti Maalum sasa aulize swali lake.

Na. 452

**Kampuni za Kutoa Taarifa za Mikopo**

**MHE. MARTHA N. GWAU** aliuliza: -

Je, kuna Kampuni ngapi nchini za kutoa taarifa za mikopo *(credit reporting company)* zinazoangalia hali ya kifedha ya mkopaji na uwezo wake wa kulipa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Hamad Chande, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Benki Kuu ya Tanzania ya mwaka 2006 imeipa Benki Kuu mamlaka ya kuanzisha na kusimamia kanzidata ya taarifa za wakopaji *(credit reference system),* kutoa leseni na kusimamia kampuni binafsi za kuchakata taarifa za mikopo.

Mheshimiwa Spika, hadi sasa, Benki Kuu imetoa leseni kwa kampuni mbili za kuchakata taarifa za mikopo. Kampuni hizo ni *Creditinfo Tanzania Limited na Dun & Bradstreet Credit Bureau Tanzania Limited.* Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Martha Gwau, swali la nyongeza.

**MHE. MARTHA N. GWAU:** Mheshimiwa Spika, ninashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali, lakini nilikuwa na maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; kwa kuwa taarifa za wakopaji ni muhimu kwa *financial institutions* zote. Je, na hizi *microfinance* ndogo ndogo nazo zinapeleka taarifa za wakopaji *BOT?*

Mheshimiwa Spika, swali la pili; ili kuepuka *default rate* kwa *financial institution* zetu. Je, *BOT* wana-*update* hizo taarifa kwenye *credit reference* kwa muda gani; kwa wiki au kwa mwezi kwa sababu tunajua wakopaji wanakopa kila siku, nashukuru. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Martha, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, taasisi zote za fedha kubwa na ndogo zinatakiwa zipeleke taarifa sahihi kwenye kanzidata inayosimamiwa na *BOT*.

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kila baada ya mwezi taarifa hizo zinapokelewa na kusambazwa kwa taasisi zinazohusika. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri tunakushukuru kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Spika, Mwongozo wa Spika.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa kipindi chetu cha maswali kutoka kwenu na majibu kutoka upande wa Serikali. Tunaendelea sasa na mambo yaliyo mbele yetu.

Waheshimiwa Wabunge, ninalo tangazo hapa la wageni. Tutaanza na wageni waliopo jukwaa la Spika, hawa ni wageni wa Mheshimiwa Jerry William Silaa ambaye ni Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya makazi. Hawa ni wapigakura na wafanyabishara kutoka Jimbo la Ukonga Jijiji Dar es Salaam. Sasa hapa wameandikwa wapigakura maarufu, sijajua kama hawapangi foleni ndiyo maana wanaitwa maarufu ama vipi, lakini karibuni sana wageni wetu kutoka Ukonga.

Yupo Nabii Nicolous Suguye, Wakili Nixon Mwera Tugara, Ndugu Violet Emmanuel Mbele, Ndugu Evarist Didas Massawe, Ndugu Nixon William Mbonile, Ndugu Abiadha Wilfred Mmari, Ndugu Rajab Said Nyangasa na Ndugu Safina Maluli. Ahsanteni sana na karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni mbalimbali pia ambao ni wageni wetu.

Tunaye mgeni wa Mheshimiwa Kundo Andrea Mathew ambaye ni Naibu Waziri wa Maji, huyu ni Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi, Kata ya Ikungulya-bashashi kutoka Jimbo la Bariadi, Mkoa wa Simiyu, karibu sana. *(Makofi)*

Yupo mgeni wa Mheshimiwa Daniel Baran Sillo, ambaye ni Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, huyu ni ndugu yake kutoka Babati. *(Makofi)*

Yupo mgeni wa Mheshimiwa Esther Matiko, mdogo wake kutoka Mkoa wa Tanga. *(Makofi)*

Wageni wanne wa Mheshimiwa Abubakar Asenga ambao ni viongozi wa mpira na mtangazaji wa *Radio One* kutoka Jimbo la Kilombero, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni sita wa Mheshimiwa Hamis Taletale, ambao ni ndugu zake kutoka Jijini Dar es Salaam na Zanzibar, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni nane wa Mheshimiwa Bonnah Kamoli ambao ni vijana wa Jimbo la Segerea wakiongozwa na Katibu wa Mheshimiwa Mbunge, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni 10 wa Mheshimiwa Mwita Waitara, hawa ni wanafunzi kutoka Chuo cha Serikali za Mitaa Hombolo, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni 17 wa Mheshimiwa Sophia Mwakagenda ambao ni wajumbe wa Kamati ya Fedha, Uongozi na Mipango kutoka Halmashauri ya Rungwe wakiongozwa na Mkurugenzi wa Halmashauri Ndugu Renatus Mchau, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, mnaozungumza nimesimama.

Tunao wageni 13 wa Mheshimiwa Angelina Malembeka, hawa ni Wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dodoma wanaotokea Masasi Mkoa wa Mtwara, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni 32 wa Mheshimiwa Florent Kyombo ambao ni viongozi wa *TK Movement* kutoka Mkoa wa Kagera, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo; wageni watatu kutoka Taasisi ya Mwanamke na Uongozi wakiongozwa na Mwanzilishi wa Shirika la Mwanamke na Uongozi. Sasa taasisi halafu shirika, haya, kimojawapo; Ndugu Shamira Mshangama ambaye pia ni Mjumbe wa Baraza Kuu la Umoja wa Vijana Chama Cha Mapinduzi, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wanafunzi 70 na walimu watano kutoka Shule ya Msingi St. Gaspar ya Jijini Dodoma, karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, hao ndiyo wageni tulionao Bungeni asubuhi hii. Tunaendelea sasa na ratiba yetu.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Spika, Mwongozo wa Spika.

**SPIKA:** Mheshimiwa Esther Matiko

**MWONGOZO WA SPIKA**

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Nimesimama kwa Kanuni ya 76. Katika kuokoa muda naomba nijielekeze kwenye mwongozo wangu kwa jambo ambalo limetokea leo mapema.

Mheshimiwa Spika, wakati Serikali ikijibu swali namba 442 ambalo lilihusiana na madai na madeni mbalimbali ya watumishi ambayo yanachukuwa muda mrefu, majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri wa Utumishi na Utawala Bora ambayo yalikuwa *supplemented* na majibu ya Mheshimiwa Jenista; kwanza tu nipende ku-*register* masikitiko yangu.

Mheshimiwa Spika, tunapokuja hapa Bungeni unakuta tunabeba kero za Watanzania ambazo zimekwishafanyiwa uhakiki na utafiti. Mathalani kwa hizi za wastaafu na za watumishi ni madeni ambayo yamechukuwa muda mrefu, yameshahakikiwa, hawa watumishi wanafuatilia kwa muda mrefu lakini hawalipwi. Sasa majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri yalionesha kama vile yale ambayo tunayauliza hapa Bungeni ni madai mapya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nina *evidence* na nitazi-*table* kwako, ambazo zingine watumishi wamedai, mathalani kuna askari ambao wamedai mwaka 2009 mpaka akaja kustaafu mwaka 2015 hajalipwa. Ameendelea kudai akiwa si mtumishi, ni mstaafu, na askari wengi sana. Kuna watumishi wa kada ya uuguzi na walimu ambao ni wastaafu, wengine bado wapo kazini wanadai madai mbalimbali. vilevile watendaji wengine ambao katika taasisi za Serikali wamekuwa wakidai, wanatufikishia sisi

Waheshimiwa Wabunge ili tuweze kufuatilia. Wamefuatilia, wanatumia nauli nyingi lakini hawawezi kulipwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mathalani tulipitisha hapa bilioni 15 kwa ajili ya kulipwa wastaafu (askari ambao wamestaafu) mpaka leo hawajaweza kulipwa. Naomba mwongozo wako. Hili la kusema kwamba Waheshimiwa Wabunge wapeleke si kweli kwa sababu haya ambayo tunayafuatilia ni ambayo yamekwishahakikiwa. Nikataka mwongozo wako, ni kwa nini Serikali isiwalipe hawa wafanyakazi ambao wanafanya kwa jasho sana? Madai yanachukuwa zaidi ya miaka 10, 12, 20 wanafuatilia tu; halafu Serikali inakuja inasema kwamba ni madai mapya ilhali ni madai ambayo tayari yapo Serikalini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo naomba mwongozo wako ili kuliweka jambo hili sawa. Je, ni lini Serikali itatekeleza haya madai yote ambayo wanayo ni mengi. Tukisema tupeleke mapya ambayo hayajahakikiwa itakuwa *overloaded*. Haya ambayo yapo kwa nini hamuwalipi hawa Watanzania ambao wanadai kwa muda mrefu na ambayo yamekwishahakikiwa? *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge amesimama Mheshimiwa Esther Matiko akiomba mwongozo kuhusu majibu yaliyotolewa kwa swali namba 442; na sasa katika mwongozo wake kwa kweli hajajielekeza kwenye hoja moja. Ameeleza hoja ya watumishi na vilevile akaeleza hoja ya wastaafu. Ameeleza watumishi ambao wanadai mpaka baadaye wanakuwa wastaafu na bado wanakuwa wanaendelea kudai. Swali namba 442 lilikuwa linahusu kulipa madeni ya muda mrefu ya watumishi. Ndiyo maana Waziri ama Naibu Waziri aliyekuja kujibu hapa amekuja kujibu wa utumishi. Kama ingekuwa inahusu wastaafu basi angekuja hapa mtu kutoka Ofisi ya Waziri Mkuu kwa sababu zile taasisi zinazoshughulika na hayo mambo zipo chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu.

Waheshimiwa Wabunge, kwamba jambo hili limetokea hapa Bungeni ni kweli limetokea hapa Bungeni. Sasa Mheshimiwa anataka mwongozo lakini ameuliza maswali kadhaa, kwamba kwa nini Serikali haiwalipi kwa wakati. Sasa maswali yanajibiwa na

Serikali na si Spika. Spika anaweza kutoa mwongozo wa jambo ambalo linakuwa limeulizwa. Hoja ya msingi ni kwamba wapo watumishi ambao wanadai madai yao ya muda mrefu; na hoja pia ya msingi ni kwamba madai haya kwa sababu ni ya muda mrefu Serikali ambacho imekifanya (Serikali hii) ni kuyachukua yale madeni na kwamba wanalipa taratibu. Huo ndio uhalisia.

Kwa maana ya kwamba, kama ni madeni ni kweli yalikuwa mengi na sisi Wabunge ni mashahidi, madeni hayajamalizika kulipwa, yanaendelea kulipwa; lakini sasa majibu aliyoyatoa Mheshimiwa Naibu Waziri na ndiyo maana nilikuwa najaribu kumwongoza; kwa kweli si kazi ya Waheshimiwa Wabunge kuyapeleka hayo. Kama kila Mheshimiwa Mbunge akisema akayakusanya ampelekee itakuwa ni shida kidogo, kwa sababu Serikali inao utaratibu wa kupokea haya madai ya watumishi mbalimbali. *(Makofi)*

Sisi kwa sababu ndio tunaopitisha bajeti, tujitahidi wakati tunapopitisha hizo bajeti tuwe tunatazama ni maeneo gani yenye changamoto ili tuishauri Serikali iyatengee fedha nyingi zaidi ili wale watumishi wawe wanafanya kazi kwa uhuru na kwa kufurahi, kwa sababu wanakuwa hawana madai ambayo wanayo. *(Makofi)*

Kwa upande wa wastaafu pia Serikali imechukua hatua kadhaa, lakini bado wastaafu hawajakwisha, ndiyo maana tunaendelea kuwapa ujumbe mbalimbali unaotoka kwa wapiga kura wetu ama wananchi ambao wanakuwa wanadai fedha zao. Kwa kweli na sisi ni jukumu letu kutazama bajeti zinapokuja hapa, kwamba yale madai yapo kwenye wizara zipi ili tuwashauri waweze kutenga, kwa maana ya sehemu zote mbili; upande wa wastaafu na pia upande wa watumishi. Kwa wale wanaokuja mmoja mmoja nadhani hawa wanaweza kupelekwa kwa Mheshimiwa Waziri kama alivyosema; lakini kwa maana ya ule utaratibu wa kawaida kabisa wa kudai madai uendelee ili watu wasije wakaleta madai sasa kwa Waheshimiwa Wabunge badala ya kupeleka kwenye ofisi zinazotakiwa, kwa sababu la sivyo tutawachanganya watumishi wa umma huko walipo.

Waheshimiwa Wabunge kwa kusema hivyo, kwa sababu aliuliza maswali, hayo ndiyo maelezo yangu ya jumla kuhusu jambo hili. Sasa tunaendelea na utaratibu wetu.

Katibu.

**NDG. EMMANUEL MPANDA – KATIBU MEZANI:**

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na majadiliano. Hapa mbele nimeletewa Majina ya Waheshimiwa Wabunge ambao wameomba kuchangia. Tutaanza na wale Waheshimiwa Wabunge ambao wamechangia mara chache zaidi halafu tutaendelea kadiri muda unavyokwenda. Tutaanza na Mheshimiwa Priscus Jacob Tarimo, atafuatiwa na Mheshimiwa Munira Mustapha Khatib, Mheshimiwa Innocent Sebba Bilakwate, ajiandae.

**MHE. PRISCUS J. TARIMO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa nafasi ya kwanza kuchangia hotuba ya Bajeti ya Wizara hii ya Ardhi siku hii ya leo ili niweze kufikisha masuala mbalimbali ambayo ni muhimu sana kwa ustawi wa Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, nianze kwanza kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa namna anavyoisimamia Wizara yake akisaidiana na Mheshimiwa Naibu Waziri. Kwa kweli wameleta chachu kubwa kwenye usimamizi wa masuala ya ardhi najua mfupa huu ni mfupa mgumu, lakini sina wasiwasi Mheshimiwa Waziri alikuwa Diwani, lakini ameshawahi kuwa Meya, kwa hiyo, anajua kule chini ambako hasa ndio kunakotengenezewa haya matatizo namna ambavyo kupo, kwa hiyo, nimtie moyo na nimwambie tu, tuna imani kwamba atatufikisha mbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nianze moja kwa moja kupongeza baadhi ya maeneo ambayo amefanya vizuri mpaka sasa. Majengo ya *National Housing Tanzania* nzima yapo maeneo ambayo ni *prime*, maeneo muhimu ambayo ndiyo yanabeba taswira. Majengo haya kwa muda mrefu yalikuwa hayafanyiwi ukarabati, yanakuwa yamebaki yamechakaachakaa, yana sura mbaya na kusababisha maeneo kama Mji wa Moshi kuonekana na sura chakavu. Nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri lakini na Mkurugenzi wa *National Housing* kwa kuleta zaidi ya shilingi milioni 300 kwenye mkoa wetu wa Kilimanjaro na kurekebisha au kufanya ukarabati kwenye majengo yale ya *National Housing* ambayo yapo katikati ya mji hasa barabara ya *Double Road*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niipongeze kazi ya Kliniki za Ardhi ambazo anazifanya Mheshimiwa Waziri ambazo zinaleta majibu ya moja kwa moja na kumuonesha uhalisia kwenye maeneo yale ambayo anafanyia kazi. Pia nimpongeze kwenye hati hizi za kielektroniki, unakuta sehemu moja watu watatu wana hati na zote zinafanana. Kwa kuleta hati hizi za kielektroniki ambazo zina *serial number* ina zina tarehe ina maana itapunguza kwa kiasi kikubwa sana migogoro, lakini italeta urahisi katika utatuzi kwa sababu itajulikana ni nani mwenye hati zile za mwanzo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pale kwenye ukarabati nilete ombi Mheshimiwa Waziri, pamoja na kukarabati zile nyumba hasa kwenye maeneo ya biashara ninaomba waangalie namna ya kurekebisha maeneo ya *pedestrian,* maeneo ya watembea kwa miguu yawekwe angalau *pavement* ili sasa uzuri huo ambao umeonekana katika ukarabati wa majengo u-*reflect* kwenye maeneo ya watembea kwa miguu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mchango wangu wa muhimu sana leo unakwenda kwenye ukurasa wa nane wa hotuba ya Mheshimiwa Waziri, lakini naangalia tena kwenye ukurasa wa 47 alipoorodhesha vile vipaumbele vya Wizara katika bajeti hii alisema ni kuongeza kasi ya upangaji, upimaji na umilikishwaji wa ardhi mijini na vijijini, sasa hapa ndio ninapotaka kuweka *point* yangu ya muhimu.

Mheshimiwa Spika, miji inakua, wakati Dar es Salaam inaanza enzi hizo pale Manzese palikuwa panaonekana ni nje ya mji, kwa hiyo, wakati inakua pale pakaachwa, pakajengwa kiholela, *slum*, hivyo hivyo pakaja Kimara. Sasa maeneo mengi ya miji yanayokua, watu wamekuwa na *tendency* ya kununua maeneo ya pembezoni, moja ni kwa sababu ya kasi ya ukuaji, lakini pili ni kwa sababu ya gharama kwenye yale maeneo yanayohusika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hili linasababisha maeneo ya pembezoni ya maeneo yale ambayo yameshatambulika kama ni maeneo ya miji kununuliwa kwa kasi na kujengwa kiholela maana yake ni nini? Kwa mfano, natolea mfano halisi wa Moshi Mjini, Moshi Mjini ndio mji mdogo zaidi Tanzania, una kilometa za mraba 58, ulipokuwa unapanuka, maeneo ambayo yalitambulika kuanzia na Baraza la Madiwani, yameshapita kwenye *DCC*, yamekwishapita kwenye *RCC* na yakaletwa Wizarani kwa ajili ya kupanua mji mwaka 2016. Mpaka leo tangu hayajapata baraka hiyo, yalishakwenda mbali sana mpaka tukapata *GN* Na. 219 ya terehe 15 Julai, 2016, lakini tangazo hilo lilitiwa saini na Mheshimiwa Lukuvi akiwa Waziri wa Ardhi tarehe 26 Juni, 2016.

Mheshimiwa Spika, ombi la msingi ni kupanua maeneo yale ya kiutawala kwa sababu eneo lile limeshajaa kabisa, hatuna maeneo ya makaburi, makaburi yamejaa, eneo la dampo tumenunua Moshi Vijijini na ni umbali mrefu, lakini adha kubwa zaidi ni kwamba barabara ya kwenda pale kwenye dampo hatuwezi kukarabati na maeneo mengine ya kiutawala. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa kwa sababu eneo la Moshi Mjini linapakana na eneo la Hai, linapakana na Moshi Vijijini ilikuwa ni vigumu kulifanyia maamuzi mara moja, lakini vikao vyote vimeshafanyika na wakati huo mimi nilikuwa Diwani nilishiriki, tukapitisha hayo, lakini mpaka leo tumeshindwa kuongezewa eneo hilo ili tuweze kupanga eneo hilo vizuri na kwa bahati mbaya waliokuwa wanapinga mwanzo walionesha eneo hilo ni eneo la kulima, lakini Mheshimiwa Waziri ninaomba ufanye ziara, uje nikutembeze, maeneo hayo yanauzwa kiholela, yanapangika

kiholela na yanajengeka kiholela, nyumba kubwa na za kifahari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, maana yake ni nini? Mnavyochelewa kuja kulifanyia maamuzi maana yake tutakuwa kila mara miji yetu badala ya kuipanga vizuri kazi yetu itakuwa ni kuirasimisha tu ambayo imeshapangika vibaya, barabara haziwezi kupelekwa, huduma za jamii haziwezi kupelekwa. Kwa hiyo, ninamwomba sana Waziri, sina nia ya kuja kukamata shilingi, nilikuwa ninaweza hapa na ndio ningekamatia, lakini ninaomba nimwelezee, naomba walifikishe mwisho suala la upanuzi na ninaelewa kuna matatizo ya kibajeti tunaposema liwe jiji, tuachane na jiji kwanza, turuhusuni yale maeneo ambayo tayari yameshapita kwenye vikao ya upanuzi yaingie, tupanue mji wetu ili suala la jiji lije baadaye, hilo ndio suala langu la kwanza ambalo nimeona ni muhimu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, eneo la pili ni eneo la urasimishaji makazi, limekuwa na *phases* mbalimbali, kuna mwanzo ilikuwa inafanyika na Serikali, baadaye wakaleta sekta binafsi ifanye, watu wakachanga hela, likaishia njiani. Tuna maeneo mengi kwenye baadhi ya kata hasa pale Moshi Mjini ambazo watu walishatoa hela kwenye makampuni ya urasimishaji, idadi haikufika ile inayotakiwa, makampuni mengine yakawa yameshaondoka na hela watu wameshatoa, urasimishaji haujakamilika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaomba Mheshimiwa Waziri wakati anahitimisha alete hoja ambayo itaonesha namna ya kufunga suala la urasimishaji hasa kwenye maeneo ya miji ambayo tayari yanahitaji sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna eneo linahitaji sana kuangaliwa na Wizara, kwa mfano Wizara ya Ardhi haina wataalamu kabisa, Mkoa wa Kilimanjaro nafikiri mkoa mzima *surveyor* ni mmoja, Moshi Mjini tulikuwa na *surveyor* tena msomi mwenye *PhD* wakamchukua, wakampeleka *UDOM*, hawajatuletea *surveyor* mpaka leo, ma-*QS* hali kadhalika.

Mheshimiwa Spika, sasa unajitahidi sana kutatua migogoro, lakini moja ya maeneo yanayokusababishia migogoro ni kutokuwa na wataalamu kule chini ambao watasimamia na kuhakikisha wanakupa taarifa za uhakika za kila siku kwenye maeneo yake, lakini pamoja na wataalam hata kwenye ofisi, sisi Moshi Mjini tulitoa eneo la ofisi kwa ajili ya Wizara ya Ardhi nimeona pale umeandika kwamba unaweka mkazo katika kujenga ofisi, lakini mpaka sasa hivi hamna kilichoendelea, eneo lipo pale kwa ajili ya ujenzi wa ofisi za Wizara yako. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, eneo lingine la muhimu sana ni eneo la maeneo ya wazi na nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri alikuwa Diwani, anafahamu jinsi maeneo ya wazi yanauzwa, yanauzwa kwa kasi sana na yanauzwa kwa watu binafsi, hili ni tatizo kubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, juzi Manispaa ya Moshi katika baadhi ya maeneo ya Kata ya Rau, Ng'ambo na Mji Mpya yalipata mafuriko, tumechukua watu tukawapeleka kwenye hizi shule mpya wakae pale kwa sababu gani? Hatuna maeneo ya wazi, yameuzwa, watu wanamilikishwa pamoja na mazuri yote ambayo yanaendelea kwenye Wizara yako naomba tutafute namna ya kuweka sheria kali kwenye maeneo ya wazi hata ikibidi hati yake iwe tofauti, lakini tuhakikishe kwamba inakuwa ni kosa la jinai mtu kununua eneo la wazi hata akiwa na hati shida hii ya kusema lazima afute Rais kwenye eneo la wazi hata kama ni miaka 20 mtu analo, tuweze kulirudisha kwa wananchi kwa sababu tunayahitaji sana maeneo ya wazi na maeneo ya wazi yanauzwa sana... *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Haya kengele ya pili imeshagonga Mheshimiwa.

**MHE. PRISCUS J. TARIMO:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja na nakushukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa Innocent Sebba Bilakwate, atafuatiwa na Mheshimiwa Suma Ikenda Fyandomo. Mheshimiwa Haji Amour Haji, ajiandae.

**MHE. INNOCENT S. BILAKWATE:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuongea kuchangia Wizara hii. Kwanza namshukuru Mungu ambaye amenipa nguvu na afya ya kuendelea kuwatumikia Wananchi wangu wa Jimbo la Kyerwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri pamoja na Katibu Mkuu na timu yake kwa kazi nzuri wanayoifanya. Mheshimiwa Waziri kwa kweli umeanza vizuri. Umeanza kuleta matumaini ambayo yalikuwa yamepotea kwa Watanzania walio wengi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nianze kuongelea kliniki ambayo Mheshimiwa Waziri ameianza. Kliniki hii imeanza kuleta matumaini makubwa. Tumeona Watanzania wengi wakitatuliwa migogoro yao kwa uwazi na kwa uhuru na hii kwa kweli imeondoa ile mianya ambayo ilikuwa wakati mwingine inaleta mazingira ya rushwa. Kwa hiyo, tunampongeza sana Mheshimiwa Waziri katika hili ameanza vizuri. Ila tunachomshauri, hizi kliniki zisambae, ziende mpaka vijijini, tumeona anaishia maeneo ya mikoani, tunataka tuone zinaenda vijijini ambapo kuna shida kubwa sana na huko ndiko kuna wananchi wengi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri hawezi akafanya hii kazi peke yake, atengeneze timu, tunapomwona yuko Arusha, tuone timu nyingine iko Kagera, tuone timu nyingine iko Dar es Salaam. Hautaweza kufika kila eneo, waengeneze timu, wawape mafunzo ili watatue migogoro kwa wananchi, kwa hiyo, ninamshauri katika hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo linguine, niongelee kupanga, kupima na kumilikisha ardhi, jambo hili ni jambo ambalo ni zuri sana na linaenda kuondoa kero na migogoro mingi ambayo imekuwepo kwa Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tumeshuhudia maeneo mengi yakiwa na migogoro, lakini pia tumeshuhudia katika maeneo mengi wananchi wanajenga maeneo ambayo ni hatarishi; kwenye mabonde na inapofika kipindi cha mvua, hali inakuwa mbaya sana. Kwa hiyo, tuombe sana Mheshimiwa Waziri wanapoenda kwenye halmashauri hizi ambazo zimepewa fedha lazima watafute mbinu ya kuwabana kwa kurejesha hizi fedha ili ziende kwenye halmashauri zingine ambazo bado hazijapimwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaamini tutakapopima maeneo yetu, tunaenda kuinua Uchumi wa Watanzania na tunaenda kuwaletea maendeleo. Nitoe mfano, ukipima kama Kagera na Kyerwa ambako kuna wakulima wengi wa kahawa, unaenda kuwainua wananchi hawa ambao wamekumbwa na biashara mbaya sana ya Butula. Wanafanya biashara ya Butula kwa sababu hawana fedha, hawana kitu ambacho wanaweza wakakipeleka benki wakapata mikopo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba sana na hili namwomba sana Waziri pamoja na Katibu Mkuu, niwaone kwa kweli wamefika maeneo ya Kyerwa, namwomba sana. Kule kuna wateja wengi na wanamsubiria sana Mheshimiwa Waziri ili na wao wapimiwe maeneo yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tutakapokuwa tumepima haya maeneo, tumeshuhudia taasisi za Serikali zimejengwa mpaka kwenye njia ambazo zilikuwa ni njia za wanyama, lakini haya maeneo yatakapokuwa yamepimwa, kila mmoja atajua eneo lake ambalo ni sahihi na kuondoa hii migogoro ya wakulima na wafugaji iliyopo na migogoro ya wananchi na Serikali kuingiliana kwenye maeneo ambayo siyo sahihi. Kwa hiyo, namwomba sana Mheshimiwa Waziri na ninamkaribisha sana, aje awapimie Wanakyerwa ili Wanakyerwa wanufaike na fedha hii ambayo imetolewa na Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine niongelee Mabaraza ya Ardhi; mabaraza haya yameundwa kwa nia ya kutatua migogoro, lakini maeneo mengi siyo yote, maeneo mengi imekuwa ni kinyume. Maeneo mengi yamekuwa ni kutengeneza

mianya ya rushwa, hakuna haki inayotendeka. Ninaomba sana Waziri afanye uchunguzi, maeneo haya kama tukibainisha maeneo Mheshimiwa Waziri, mengi hayafanyi vizuri, ni afadhali haya mabaraza yakaondolewa tukarudisha kwenye haki kwenye sheria, mahakama ambayo tunaamini wanaweza wakapata haki, lakini huku hali ni mbaya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nilikuwa nashangaa wakati mabaraza haya yanaundwa, yaani watu walikuwa wanapambana na kutumia nguvu kubwa na rushwa, kumbe ni kwenda kuwaibia wananchi. Kwa hiyo, naomba sana Mheshimiwa Waziri alichunguze hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo ni la kujiuliza, Mheshimiwa Waziri hivi haya mabaraza wameyawezesha au wameyaunda tu wakayaweka kule ikaishia hapo? Lazima tujiulize, mabaraza haya tumeyawezesha, wana vitendea kazi? Pia, posho zao zile wanazostahili kupewa, wanapewa na ni nani anayewapa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, namwomba sana Mheshimiwa Waziri, anapokuja hapa atueleze ni nani anayewalipa hawa? Pia, je, wamewawezesha na kuwapa mafunzo? Maana wengine hata sheria hawazijui. Kwa hiyo, naomba sana uliangalie hili ili haki iweze kutendeka na wananchi wetu waweze kufurahia jambo hili ambalo ni jema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo nilisemee, Mheshimiwa Waziri hawa Wakuu wa Idara za Ardhi, Maafisa Ardhi wa Wilaya pamoja na kuwaondoa kwenye halmashauri bado wako chini ya halmashauri. Naomba sana wawawezeshe hawa watu, siyo wamewaweka pale bado wanaendelea kuomba kule kwenye halmashauri, hawatafanya kazi vizuri. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri naomba sana wawawezeshe, wawape vifaa na mahali ambapo bado hawajawafikia kwenda kuwapimia kupitia Mpango huu wa KKK, waweze kuwapimia wananchi na maeneo yao yatambulike. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaamini tutakapokuwa tumeyafanya haya, wananchi wakapimiwa maeneo yao hizi kero zitaondoka na nchi itakuwa salama. Pia, tujue uchumi wa Taifa letu utakua kwa sababu mwananchi atakuwa na uwezo wa kufanya jambo lolote anaweza kujipatia fedha kupitia ardhi yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nampongeza Mheshimiwa Waziri, anafanya kazi nzuri na nimwambie neno moja, kuna jamaa mmoja, Mheshimiwa mmoja alichangia akasema ardhi imelaaniwa, lakini nimpe Neno la Bwana: "*Macho ya Bwana huwaelekea wenye haki na masikio yake husikia kilio chao". Uso wa Bwana ni juu ya watenda mabaya, utakapokuwa umesimama kwenye haki, ukatenda haki...*" Nina uhakika Mheshimiwa Waziri atakuwa salama na hakuna kitakachomdhuru. Mungu ambariki, Amina. *(Makofi)*

**WABUNGE FULANI:** Amina.

**SPIKA:** Mheshimiwa Suma Ikenda Fyandomo, atafuatiwa na Mheshimiwa Haji Amour Haji, Mheshimiwa Vita Rashid Kawawa, ajiandae.

**MHE. SUMA I. FYANDOMO:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia kwenye Wizara hii muhimu ya Ardhi. Kwanza, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa nafasi ambapo amenipa afya njema nimeweza kusimama kwenye Bunge hili Tukufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa nampongeza Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan ambapo Mwenyezi Mungu alimpa macho ya rohoni kumteua Mheshimiwa Waziri wa Wizara ya Ardhi, kaka yangu hapa na *aunt* yangu hapa Silaa, ambaye kwa kweli anaitendea haki sana hii Wizara ya Ardhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninampongeza Mheshimiwa Waziri Silaa kwa namna ambavyo anafanya vizuri. Anawatetea wananchi na amesimama kwenye haki. Nami namtia moyo kwa namna anavyofanya Mwenyezi Mungu asimpungukie, amsimamie

kwenye majukumu yake, asiwe na hofu wala wasiwasi Watanzania wote wanamfurahia kwa kazi nzuri hii anayoifanya kwa sababu anawasaidia hata wale wanyonge ambao hawana uwezo kabisa. Maana mara nyingi inaonekana kama haki haipo; haki inapatikana kwenye fedha, lakini wewe hilo kwako halipo. Ninampongeza sana pamoja na Wizara yake yote ya Ardhi, Mwenyezi Mungu aendelee kuwa pamoja nao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo naishukuru sana Serikali kwa kuleta fedha kupitia Mradi wa *World Bank* katika Mkoa wa Mbeya ambapo fedha hizo zimewezesha kuandaa mpango wa matumizi ya ardhi katika Wilaya ya Chunya ambapo kwa ujumla wa vijiji 21 vimeandaliwa mpango wa matumizi ya ardhi na pia migogoro ambayo ilikuwepo kati ya mipaka ya Songwe na Mbeya imeweza kutatuliwa na migogoro 18 ya mipaka na vijiji pamoja na Mbeya yenyewe Chunya na Songwe imekwenda kutatuliwa.

Mheshimiwa Spika, hivyo naipongeza sana Serikali na naishukuru kwa kufuatilia haya na kutuletea fedha hizo ambazo zinakwenda kufanya na kutenda haki. Pia, naishukuru sana Wizara kwa kutuletea mradi katika Halmashauri za Rungwe, Kyela na Busokelo ambapo zaidi ya vijiji 250 vinaenda kuandaliwa ambapo inakwenda kumaliza migogoro yote katika halmashauri hizo.

Mheshimiwa Spika, kwa shukrani hizi; unajua Mkoani Mbeya kesi zinakuwa nyingi sana kwa ajili ya kung'ang'ania ardhi wakati fulani hata ikizidi futi moja mtu anaweza asikubaliane na ile futi moja anakwenda Mahakamani kesi zinaenda kurundikana. Sasa kwa kutuleta fedha hizi tunaamini kwamba tunakwenda kupona kwa kesi hizi ambazo zinakuwa zinajitokeza.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa mpango kabambe wa Jiji la Mbeya kwa maana ya *masterplan,* Jiji la Mbeya ndiyo jiji pekee nchini ambayo sehemu yake kubwa katika kitovu cha jiji ina makazi yaliyo chakaa sana yenye ujenzi holela. Kutokana na hali hiyo *masterplan* ya jiji ambayo imeanza kutekelezwa mwaka 2022 ilikuja na mwongozo wa utekelezaji upya wa makazi yaliyochakaa ya Kata ya Maanga, Sinde, Ruanda na Mabatini.

Mheshimiwa Spika, Jiji la Mbeya kama nilivyoeleza hapa awali, Jiji la Mbeya ni jiji kongwe, ni jiji ambalo jina lake ni kubwa sana lakini jiji lile huwezi kusema sasa hivi unaingia hapa, kwamba hapa ndiyo mjini. Mji upo wapi? Mji ni Manga? Haiwezekani, Mji ni Sinde? Haiwezekani, Mji ni Mabatini? Pamejengwa kiholela hakuna mpango wa *masterplan*. Hivyo naiomba sana Wizara ya Ardhi iliangalie hili kwa macho yote kwenye Mkoa wa Mbeya katika mpango huu ambao unaendelea pale Mkoani Mbeya uliyoandaliwa tangu mwaka 2022 ili kuweka sura ya mji pale Mbeya iwe sawa sawa na majiji mengine.

Mheshimiwa Spika, wananchi wa Mkoa wa Mbeya kiu yao kubwa ni kuona jiji lile la Mkoa wa Mbeya linafanana na majiji mengine. Sawa kuna nyumba zipo pale lakini ni chakavu sana, nyumba zimechakaa lakini pia popote unapopita unaangalia hivi nakwenda mjini, ni wapi? Mjini ni Posta, Mafiati, Mwanjelwa ama mjini ni wapi? Kwa hiyo naomba sana Serikali tuangalieni sana wananchi wa Mkoa wa Mbeya ili na sisi pale pawe na sura nzuri inayofanana na majiji mengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali kwa Wizara, Wizara ina mkakati gani wa kusaidia utekelezaji wa uendeshaji upya wa makazi yaliyochakaa na yenye ujenzi holela katika kitovu cha Jiji la Mbeya? Kama kuna jambo Wananchi wa Jiji la Mbeya wanatamani ni uendelezaji mpya wa maeneo yaliyochakaa katika Jiji la Mbeya pamoja na *centre* inayokuwa na hadhi ya jiji kama yalivyo kwenye maeneo mengine.

Mheshimiwa Spika, upangaji na upimaji kwenye maeneo yote ambayo barabara ya mzunguko wa *ring road* na barabara ya mchepuko *by pass* maeneo hayo yanakwenda kutengenezwa ama yanakwenda kujengwa, hizo barabara ni mpango kwa sababu barabara hizo zinapita kwenye ardhi. Wakati Wizara inaendelea kujipanga kwenye ujenzi wa hiyo barabara tulitamani sana fedha ziende kwenye Wizara hiyo kwa maana ziende Jiji la Mbeya ili wakati wa mpango wa zile barabara ambazo zinakwenda kujengwa sasa kuwe tayari kumeshapimwa.

Mheshimiwa Spika, kwa namna ambavyo Mbeya ilivyokaa tunaomba sana ionekane ni jiji la kisasa. Ni jiji ambalo limeonekana na kwamba hilo jiji linakwenda kuonekana kama majiji mengine. Jiji kama jiji kwa maana Halmashauri ya Mbeya Mjini haiwezi kuwa na fedha ambazo zitaweza kutengeneza ama kuweka majengo ambayo yanatakiwa kwenye Jiji hilo la Mbeya. Tunaitegemea sana Wizara iangalie macho yote pale kwenye Jiji la Mbeya na mkiangalia jiji lenyewe hilo mnaona kabisa na mnajua kabisa mwenye jiji lake ni Mheshimiwa Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na bado ni Rais wa Mabunge ya Dunia - *IPU* linatakiwa lifanane pamoja na yeye mwenyewe kwa nafasi zake alizokuwa nazo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Wizara ikifanya hivyo itakuwa imetuheshimisha sana wananchi wa Mkoa wa Mbeya, lakini pia imekupa heshima kubwa sana kulingana na nafasi zako ulizonazo. Kwa kusema haya nishukuru sana kwa kunipa nafasi nami kuongea juu ya hili jambo. Mwisho Mheshimiwa Waziri Jerry Silaa Mwenyezi Mungu aendelee kumsimamia na kumwongoza kwenye majukumu yake kila anapopita anaombewa kwa Mwenyezi Mungu kulingana na unyenyekevu wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nasisitiza Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan tunamshukuru kwa sababu sisi wazalendo tunaomwombea mema kwenye Taifa hili la Tanzania Mwenyezi Mungu anakubali na anampa macho ya rohoni anakwenda kuwateua watu muhimu kama hawa akina Mheshimiwa Jerry Silaa. Mwenyezi Mungu aendelee kusimama na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan pamoja na Serikali yake yote, tunaikabidhi mikononi mwa Mwenyezi Mungu kwa jina la Yesu Kristo, Amina. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Haji Amour Haji atafuatiwa na Mheshimiwa Vita Rashid Kawawa na Mheshimiwa Hawa Mwaifunga ajiandae.

**MHE. HAJI AMOUR HAJI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kuweza kuniona leo hii katika kuchangia Bajeti ya Wizara ya Ardhi. Pili, niseme kwa kumpongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri

ya Muungano wa Tanzania kwa kuweza kutuchagulia mtu wetu huyu Mheshimiwa Jerry Silaa kwa namna ambavyo alivyomwona katika hali ya utendaji wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tutamzungumzia Mheshimiwa Jerry Silaa ambaye ni kiongozi wangu nimetoka naye kule akiwa kama Mwenyekiti wangu wa Kamati ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma, mwanzo kabla ya kuteuliwa nilimwambia maneno, mara ya pili baada ya kuteuliwa nayo pia nikamwambia maneno sijui kama anayakumbuka. Nilizungumza neno la Kiarabu nilimwambia *al-mujtahidu-l-wajada.* Sasa kama *al-mujtahidu-l-wajada* maana yake kwamba kwa kila mwenye kujitahidi Mwenyezi Mungu humpa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa kwa ndugu yangu Mheshimiwa Jerry haikuwa bahati mbaya kwa kuchaguliwa kuwa Mheshimiwa Waziri katika Wizara ya Ardhi, amechaguliwa kwa sababu ya jitihada zake na hilo maana yake aliweke kila anapokwenda na Mwenyezi Mungu ampe hekima hiyo ya kuweza kuwaongoza watu kwa hekima na maarifa.

Mheshimiwa Spika, labda pengine nimwambie tu Mheshimiwa Waziri kwamba tunampa pongezi nyingi sana lakini hizi pongezi ambazo tunampa na hizi sifa ambazo tunampa kwake yeye iwe ni changamoto. Asije akafanya hizi sifa tunazompa zikaja zikamfanya kwamba akaja akatoka nje ya reli. Hayo kwake yeye maana yake yawe kama ni changamoto na aone wazi kwamba wanaonisifia ni binadamu wenzangu kama kawaida, kwa maana hiyo maana yake kwamba nifanye kazi kwa mujibu wa hali ambayo Mwenyezi Mungu atakayonijalia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nije katika mchango wangu wa Wizara ya Ardhi. Ukweli katika hali ya kisomi kuna wengine wamechukulia suala la ardhi wakachukulia ule msemo wa chama chetu kwamba ardhi, watu na kadhalika kwamba ndiyo vitu vya msingi lakini katika masuala ya uchumi ardhi maana yake ni moja ya jifya ya uchumi namba tatu. Katika suala la uchumi tuna vitu

vitatu, tuna suala la ardhi, tuna suala la wafanyakazi *(labour)* na suala na mtaji.

Mheshimiwa Spika, lakini suala ambalo ni kubwa sana ni suala la ardhi, ardhi maana yake ni uchumi katika nchi yetu. Sasa nitazungumzia kwamba ardhi ni uchumi katika nchi yetu kwa sababu ardhi ina mambo mengi. Katika ardhi maana yake ndani yake ndimo mnamofanywa shughuli za kilimo, katika ardhi ndimo tunapopata maji ya kunywa, katika ardhi ndimo tunapofanya viwanda vyetu, katika ardhi ndimo tunamofanya kila kitu chetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa nizungumzie suala moja tu ambalo limezungumzwa na watu wengi sana hapa katika michango yao Waheshimiwa Wabunge na kila mmoja anazungumza kwamba kwenye matumizi ya ardhi maana yake hakupo vizuri lakini mimi nione kwamba katika matumizi ya ardhi kitu ambacho kinakosekana; bahati nzuri kwamba katika Wizara yetu tuna Tume ile ya Mipango inayoshughulika na masuala ya ardhi.

Mheshimiwa Spika, tusitosheke na ile Tume, nimshauri Mheshimiwa Waziri kwamba, lazima tuwe na *National Land Use Integration Planning* ambayo ni ya Kitaifa ambayo michoro yetu ya ardhi maana yake tufanye suala la *mapping,* kui-*map* nchi yetu na shughuli za kiuchumi. Kwa mfano Tanzania mpaka hii leo tunavyokwenda maana yake tunajaribu kuwashauri Waheshimiwa Mawaziri.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano juzi Mheshimiwa Waziri wa Viwanda, kila mmoja alishauri katika mkoa wake maana yake kuwe na viwanda. Kitu ambacho maana yake hakujafanywa ile *mapping* na suala la *planning* ya ile ardhi nini kitakachofanyika katika sehemu zile maana yake hicho kinakosekana. Sasa ushauri wangu mimi labda pengine tuige kule Zanzibar maana yake Zanzibar wao wameandaa na wamekifanya kitu wanachokiita *Integration Land Use Plan and Strengthen Land Management and Administration in Zanzibar*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa ile maana yake itasaidia nini? Inasaidia katika ku-*map* zile sehemu zote za ardhi kwa mujibu wa nchi yetu nzima ambayo ilivyo kwa kuangalia matumizi ya makazi ya watu, kuangalia matumizi ya kilimo, kuangalia matumizi ya utalii, kuangalia na matumizi ya shughuli za kibinadamu. Vilevile maana yake katika utaratibu huo tunatakiwa pia tuwe na yale maeneo ya wazi, kitu ambacho hata Waheshimiwa Wabunge hapa walizungumza sana kuhusu kuweka marufuku sana kwa sehemu za wazi hata katika hotuba ya Waziri amesema katika jambo ambalo atalikemea moja, watu kuchukua sehemu za wazi kwa sababu kuna umuhimu wake kubakisha sehemu za wazi.

Mheshimiwa Spika, umuhimu wake kwanza kwa watu kucheza, kama Waziri alivyozungumza katika hotuba yake ya bajeti, lakini kitu muhimu kikubwa zaidi kuliko yote ni suala la kiusalama. Suala la kiusalama maana yake linaangaliwa katika hali ya upana mkubwa sana, haiwezekani kwamba kwamba tumejenga makazi mahali fulani, lakini yanatoa maafa hatuna hata mahali pa kuwakusanya watu zaidi ya kuangalia maeneo ya shule na maeneo mengineyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nadhani nimshauri Mheshimiwa Waziri kwamba ajaribu katika kufanya shughuli zake kupanga mipango miji ya Kitaifa na tuwe na mpango maalum wa matumizi ya ardhi. Vilevile, maana yake ni vizuri zaidi tukawa tuna kitu cha *integration* kwa kuzishirikisha kwanza watu wa ardhi maana yake wawepo, tunataka Tume ya Mipango ya Taifa washirikiane nayo, tunataka kwamba Wizara inayoshughulika na masuala ya Mazingira maana yake iwepo pamoja na Wizara hii ambayo tunayosema ya hakimiliki ambayo inashughulika na mambo ya miliki iwepo ili kui-*map* nchi yetu katika shughuli za kiuchumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ardhi ni uchumi, ardhi ni faida kwa nchi yetu. Kwangu mimi kubwa nadhani ni hilo nililolizungumza na kumpa ushauri Mheshimiwa Waziri kwa suala hilo, lakini mwisho maana yake nampongeza sana Mheshimiwa Waziri kwa namna anavyofanya shughuli zake na alipoanza. Wachina wana msemo

wanasema; 'Heko', mimi nitampa heko kwa shughuli zake na kwa namna anavyofanya shughuli zake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Vita Rashid Kawawa, atafuatiwa na Mheshimiwa Hawa Mwaifunga na Mheshimiwa Jafari Wambura Chege.

**MHE. VITA R. KAWAWA:** Mheshimiwa Spika, nami nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii. Nami niungane na wenzangu kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri kwa kazi nzuri wanayoifanya yeye, Mheshimiwa Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watumishi wote wa Wizara ya Ardhi. Kazi nzuri sana wanaendelea kuifanya na hasa wanafanya kazi hiyo kwa msingi kwamba ardhi ndiyo msingi wa maendeleo ya Taifa letu na ndiyo eneo kubwa linalotegemewa na wananchi kimakazi lakini pia kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, ardhi kiuchumi katika wilaya yetu au katika nchi yetu haiongezeki ila wananchi tunaongezeka na matumizi yake yanaongezeka na ndiyo maana kuna migogoro ya ardhi. Kwa hiyo kazi nzuri wanayoifanya ya kuendelea kutatua migogoro ya ardhi tunaomba waendelee nayo hivyo hivyo.

Mheshimiwa Spika, sisi kwetu kule Namtumbo eneo kubwa la ardhi ni hifadhi lakini sisi ni wakulima. Kwa kuzingatia sera, Serikali iliyokuwa inahimiza matumizi bora ya ardhi na sisi tulipanga matumizi bora ya ardhi katika Wilaya ya Namtumbo. Katika matumizi hayo bora ya ardhi tulipanga katika maeneo ya kilimo, uhifadhi na makazi. Pia, tulipanga eneo la uhifadhi kwa maana ya kwamba watu wanapoongezeka, mahitaji yanapoongezeka basi ile ardhi iliyohifadhiwa ya kijiji ije kusaidia kwenye kilimo kwa ajili ya wananchi wetu kuzalisha mazao na kujiongezea kipato kiuchumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali ilikuja pia na mpango mwingine katika eneo letu la hifadhi za vijiji kwamba basi kuongeza mapato kwenye hifadhi ile tuzifanye pia kama *WMA*. Katika utaratibu

tuliowekeana vijiji na Serikali kwamba kila baada ya miaka 10 tutafanya mapitio ili kuona kuna hitaji la ardhi kwenye kilimo baada ya watu kongezeka, lakini mpaka leo hii zaidi ya miaka 15 jambo hilo halijafanyika na kumekuwa na *demand* kubwa sana ya wananchi kufanyiwa mapitio ya ardhi.

Mheshimiwa Spika, sasa hili nalieleza kwa sababu Wizara ndiyo wanasimamia ardhi hii. Sasa hii ni kero kubwa sana kwa wananchi, kule tuna jumuiya zinaitwa Kimbande, Kisungule na Mbarang'andu zinahitaji mapitio ya ardhi. Watu wa eneo la Mbarang'andu hususani Kata ya Mchomolo walilalamika sana kwa presha kubwa sana mpaka tukasukuma wakaenda kufanyiwa mapitio, lakini mpaka leo hakuna majawabu yanayoeleza hayo mapitio yake ya ardhi wataongezewa kiasi gani kwa ajili ya kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kinachotokea wakulima wanaonekana wanavunja sheria ya kuingilia maeneo ambayo yamehifadhiwa. Kwa hiyo sisi tunaomba Serikali itusaidie kwenye hili, haya mapitio ni makubaliano ya kisheria kwa hiyo yarudi yakamilishwe kisheria kama utaratibu ulivyofanyika wakulima waendelee kupata eneo la kulima. Watu wameongezeka wanataka kulima na uchumi wa watu wa Namtumbo unategemea kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la pili, Mheshimiwa Waziri aliongoza safari ya Mawaziri Nane kama kawaida ya kwenda kutembelea na kuangalia migogoro au kueleza maamuzi ya Baraza la Mawaziri. Walipokuja Namtumbo walienda katika Kijiji cha Lingusenguse mkaeleza maamuzi ya kutaka Kitongoji cha Semeni kiondoke pale kilipo kiende eneo lingine, wakaeleza vizuri, lakini nataka niwafahamishe kwamba kitongoji kile pale wale ndiyo asili na asili yao, hifadhi iliwakuta pale, wale hawana tofauti na Ngorongoro tofauti yao watu wa Ngorongoro wanavaa mgolole wale hawavai migolole lakini wao nao wanaishi na wanyama na wamekuwa wakiishi na wanyama miaka nenda miaka rudi, pale walipoenda ndipo asili ya babu wa babu yangu, pale ndiko asili yao na ndio walikuwa wanaishi na wanyama, sasa leo wanawaambia wanawahamisha, wanawahamisha hivi hivi tu?

Mheshimiwa Spika, dunia iko kiganjani watu wote dunia hii wanajua kila kinachoendelea siku hizi. Wanaohamishwa Ngorongoro wanawapeleka kule Msomera wanawajengea nyumba, wanawapa ardhi kwa ajili ya uchumi, wale wanaenda kuwahamisha hawakuwaambia wakiwahamisha wanawapeleka wapi na watawajengea? Kwa sababu pale Serikali ilijenga shule pale iliwatambua, wale wananchi wana mashamba yao makubwa ya chakula na ya biashara ya mikorosho, wanazo nyumba pale za kudumu, sasa wakienda kwa kauli ya wahame pale tu hivi hivi na wakaenda kusimamia wahame tu, bila kutengeneza utaratibu mzuri kama wa Msomera, watakuwa wametubagua, sisi sote ni wamoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimesema, tofauti yetu sisi na Ngorongoro, Ngorongoro wanavaa migolole na wanatembea na sime, sisi hatuvai migolole lakini tunaishi sawa tu na wanyama, tembo, simba, fisi na wengine wote, faru tunaishi nao. Kwa hiyo, tunaomba sana uamuzi huo wauangalie nasi wasitubague.

Mheshimiwa Spika, naishia hapa, ahsante sana kwa kunipa nafasi. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Hawa Subira Mwaifunga, atafuatiwa na Mheshimiwa Jafari Wambura Chege, Mheshimiwa Simai Hassan Sadiki ajiandae.

**MHE. HAWA S. MWAIFUNGA:** Mheshimiwa Spika, nikushukuru kwa kunipa nafasi. Kwanza nimshukuru sana Mwenyezi Mungu ametujalia afya na leo nimeweza kusimama, pia tunamshukuru Mwenyezi Mungu amekurudisha salama na umefika umeingia kazini, tunaendelea kukuombea katika majukumu ya hapa na huko kwa wenzetu ambako umeendelea kuwaongoza vema, Mwenyezi Mungu aendelee kukubariki sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa ningependa kumpongeza Waziri kwa kazi kubwa ambayo anafanya, lakini Waziri ana wasaidizi, hongera sana kwa Mheshimiwa Naibu Waziri kwa kazi nzuri ambayo amekuwa akishirikiana na Waziri wake kuifanya,

wamekuwa wasikivu, wamekuwa wakitusikiliza pale ambapo tumekuwa tuna changamoto.

Mheshimiwa Spika, kama sitampongeza Kamshina wangu wa Mkoa wa Tabora kwa kweli nitakuwa sijamtendea haki, Kaka yangu Hussein amekuwa ni Kamshina mzuri, amekuwa ni msikivu na wakati wote wananchi wa Tabora wamekuwa wakinipa changamoto nikizipeleka amekuwa akiwasaidia na kuwashughulikia kwa karibu kweli kweli, pia amekuwa akisimamia migogoro mbalimbali ambayo tunashukuru angalau kwa sasa wananchi wa Tabora kidogo tunapumua tofauti na ilivyokuwa huko nyuma.

Mheshimiwa Spika, naomba kwanza nijikite kwenye hii Tume ya Mipango na Matumizi Bora ya Ardhi. Nimesema hivi kwa sababu mara nyingi sana kila ninaposimama nimekuwa nachangia kwenye hii Tume, kwa sababu ya kujua na kuona umuhimu wa Tume hii. Nilikuwa sifahamu sana changamoto hizi za ardhi lakini kwa bahati nzuri alinipa nafasi ya kuwa kwenye Kamati ya Ardhi na Maliasili, kwa hiyo nilijua na kufahamu kwamba migogoro hii na changamoto hizi nini kifanyike ili tuweze kusaidia kutatua changamoto hizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tumemwona Mheshimiwa Waziri na timu yake wakienda maeneo mbalimbali kwa ajili ya kutatua migogoro, lakini kama Wizara ama Serikali haitatenga fedha ya kutosha kwa Tume hii ndugu yangu Waziri Jerry Silaa utasaga visigino, unamaliza mgogoro upande huu upande wa mashariki mgogoro umezuka kama jana, kama hatutafanya maamuzi thabiti ya kuiwezesha Tume hii iweze kufanya kazi yake na kumaliza kupima na kupanga kwa wananchi ili kila mmoja aweze kujua ni wapi anastahili kuwepo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama mtakumbuka ule mgogoro wa Loliondo, ni hii Tume imekwenda kusaidia sasa hivi pamekuwa patulivu kwa sababu wamekwenda kuonesha kila mwanakijiji na eneo lake, hapa utafuga hapa utalima, hapa utaishi na ndicho hicho ambacho Tume inakwenda kufanya kwenye maeneo mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, leo ninavyozungumza hapa, watu wamekuwa wakinunua maeneo kiholela, hizi fedha ambazo tunaziomba na kuzipitisha zikajenge hospitali, zikajenge shule, zikajenge vituo vya afya badala ya kufika na kufanya ujenzi wanaanza kwanza kulipa fidia kwa wale walionunua ardhi tena kwa fedha wanayoitaka wao, wakati maeneo hayo yalikuwa ni maeneo ya Serikali kiasi kwamba kama yangekuwa tayari yameshatengwa ina maana pale tukiambiwa kijiji hiki shule inakwenda, shule inakwenda kujengwa bila matatizo yoyote ya kulipana fidia ambazo ni fedha nyingi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimeona na nilikuwa najaribu kupitia maeneo mbalimbali, nimeona nguvu kubwa na ya kutosha kwa kazi ambayo Tume hii wanaifanya. Safari hii 2023/2024, kwanza tulipunguza bajeti hata ile bilioni nne ambayo walisema watawapa 2022/2023 haikukamilika, lakini 2023/2024 wamepewa bilioni 3.4 na wamefanya kazi kwa asilimia mia moja, uone ni kwa namna gani Tume hii ina uwezo mkubwa wa kufanya kazi kama tutawasaidia kuwapa fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakuhakikishia kama kweli tunataka migogoro ya ardhi nchini ipungue siyo kwa Mheshimiwa Jerry Silaa kupita na kuangalia matatizo ya watu. Ni lazima tukubali kama Taifa kutenga walau kwa mwaka hata bilioni 20 ili ziweze kwenda kufanya kazi ya kupima vijiji vyetu kule. Hili linawezekana, nilikuwa napitia bajeti ya mwaka huu, Tume wametengewa eti bilioni tano! Hivi kweli tuko *serious?*

Mheshimiwa Spika, nakwambia kama bilioni tano hii itatoka yote Mungu shahidi, wamekuwa wakija hapa tunawapitishia fedha. Kama utakumbuka bajeti ya mwaka jana ilikuwa ya moto kweli kweli, kila Mbunge aliyesimama hapa alizungumzia kuhusu suala la Tume, Serikali ikaji-*commit* ikasema katika ule mradi wa *LTIP* Serikali itatoa bilioni 20 ili kuweza kupeleka Tume ikapime. Mpaka sasa hivi tunavyozungumza hakuna fedha iliyokwenda na wanafanya hivyo, wanatudanganya Wabunge ili tusishike shilingi zao ili tusiweze kusema sana humu ndani, wanatudanganya, wanatuambia lakini hayatekelezeki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa watuambie huu Mradi wa *LTIP* si umeshaanza, sasa kama umeanza kwa nini hizi fedha hazitoki zikapelekwa Tume ikafanya kazi yake? Kama Tume inahitaji shilingi bilioni 20 kwa mwaka angalau katika vijiji 8,500 kupima vijiji 1,400 kila mwaka, tutakuwa wapi, lakini bado tukumbuke Wana-CCM wenzangu…*(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, unapoingia kwenye Bunge, naona nakaribishwa vizuri na makofi, nimepokea makofi jamani. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, unapoingia Bungeni moja kati ya *package* ambayo tunapewa katika lile furushi la mabegi huwa tunapewa Ilani ya Chama Cha Mapinduzi ili kuangalia utekelezaji wa yale ambayo wanataka kuyafanya kwa kipindi cha miaka mitano. Moja katika vitu ambavyo wanataka kuvifanya ni kupima zaidi ya vijiji 2500 mpaka mwaka 2025, lakini mpaka sasa kama kwa *trend* hii ambayo tunakwenda nayo ya kupeana bilioni tatu, kupeana bilioni moja, ya kupeana shilingi bilioni tano ambazo tunaambiwa kwenye makaratasi lakini hazitoki, tutafanikisha upimaji huu?

Mheshimiwa Spika, hii ni Ibara ya 74 ambayo ilikuwa inazungumzia hilo, lakini Takwimu za Wizara zinaonesha vijiji 8,500 vinatakiwa vikapimwe, vinapimwaje kama fedha hakuna?

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumzie tena Tume hii ambapo na niwaambie ukweli kama tunataka kuingia kwenye uchaguzi tukiwa salama bila kelele za migogoro iliyopo ya ardhi, hii Tume nadhani ndiyo *strategic point* ya ninyi kuingia kwenye uchaguzi huu na kupata ushindi 2024/2025, 2025/2026. Namwambia Mheshimiwa Waziri leo kama hajaja na majibu ya maana kuhusiana na Tume hii na fedha hizi namuahidi Mheshimiwa Jerry shilingi yake nitaishika na nitaishika mpaka mwisho. Lazima wafike mahali waone umuhimu wa hii Tume, waweze kuipatia pesa ili wananchi wetu waweze kupata ahueni, lakini hata Waziri na timu yake pia wapumzike! Kwa sababu hii kwenda kila siku huko, atakutana na mambo mengine mabaya! Namwonea huruma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ni bora tenga fedha watu wako wakafanye kazi, una watu wazuri, Tume yako ni nzuri, ina kiongozi mzuri na watendaji wake wazuri, wanao uwezo mkubwa wa kufanya kazi. Waende wakafanye kazi kwa kuipa Tume na kama hawaitaki basi walete sheria, hii Tume ipo kwa mujibu wa Sheria, Sura 116, kwa hiyo kama ni Sura 116 walete hapa tuibadilishe, tuipeleke kwa Mheshimiwa Profesa Kitila kwenye Tume ya Mipango ili akiwa na Tume ya Mipango ya Matumizi Bora ya Ardhi na kule, pengine kule wataweza kutenga fedha nyingi na hii kazi ikaenda kwisha na mwisho wa siku hii migogoro ikaweza kupungua.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Jafari Wambura Chege, atafuatiwa na Mheshimiwa Simai Hassan Sadiki na Mheshimiwa Munira Mustapha Khatib ajiandae.

**MHE. JAFARI W. CHEGE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia bajeti ya Wizara ya Ardhi. Kwa kuanza tu niseme, mimi ni mzaliwa wa Mkoa wa Mara na desturi za Mkoa wa Mara, mara nyingi sisi huwa ni wasema kweli daima, nyeupe kama ni nyeupe itasemwa nyeupe na nyeusi kama ni nyeusi itasemwa nyeusi, pale inapolazimika nyeusi kusemwa nyeupe basi huwa tunaisema kwa sauti ya mnong'ono huwezi kuisema kwa sauti kubwa kwa sababu unakuwa umesema kinyume na matakwa yako. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimeanza kwa kusema hivyo, niseme ukweli nimesoma taarifa ya bajeti ya Mheshimiwa Waziri, nimesoma randama, wikendi yote hizi siku mbili nimejipa muda wa kusoma kipengele kwa kipengele kwa kutambua ni mdau wa Sekta ya Ardhi.

Mheshimiwa Spika, nikwambie na niwaambie Wabunge, Mheshimiwa Waziri kupitia hotuba yake na kazi kubwa aliyoifanya amefanya kazi kubwa sana, nasema hayo kwa kuwa nimekuwa mtumishi kwa miaka nane ndani ya Wizara hii na hata nilipoacha utumishi bado nilirudi mtaani kufanya kazi ya sekta ya ardhi. Kwa

hiyo, kwa maana moja ama nyingine ni mdau wa sekta ya ardhi kwa zaidi ya miaka 14. Najua mfumo wa ndani wa Wizara unavyofanya kazi, lakini ukirudi kama kimtaani mtaani namna ya uendeshaji changamoto zinazowakumba wadau wa sekta ya ardhi, kule mtaani napo nazijua kwa sababu nimefanya kazi kama dalali na kwa bahati nzuri Waheshimiwa Wabunge wengi humu nimewauzia ardhi. Kwa hiyo, najua changamoto za sekta ya ardhi *in and out. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaposema kwamba Mheshimiwa Waziri ametutendea haki sisi wadau ni pale ambapo tumeona ameyagusa maeneo mengi ambayo ndiyo vilio vya sekta ya ardhi na wadau wa ardhi kwa miaka nenda rudi. Amegusa maboresho ya kanuni ambayo sisi kama wadau tumekuwa tukizungumza namna kanuni zinavyotukwamisha kwenye utendaji wa kazi zetu. Amekwenda kuzungumzia maboresho ya sera ikiwemo na sera ya Taifa ya Ardhi ya mwaka 1995, amezungumzia namna ya kutambua Wathamini *(Valuers)* ambao kimsingi kazi yao kubwa baada ya kufanya uthamini wale wamekuwa wakirushiwa mzigo. Ndiyo wameonekana wezi, wamekuwa wakionekana matapeli, lakini amekwenda kutengeneza mwongozo ambao unawanusuru wathamini na naamini kwa kutumia ule mwongozo hawa wathamini wataenda kuheshimika maeneo yote ndani ya nchi hii.

Mheshimiwa Spika, amekwenda kugusa maboresho mbalimbali ya sheria kwenye taarifa hii. Kubwa ambalo amelifanya ni kutambua na kuthamini *private sector* ambazo wanafanya shughuli za ardhi na amezirudisha na kufanya nao kazi. Mheshimiwa Waziri Mungu akurehemu umefanya kazi kubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu tu, kwenye hii *transformation* unayokwenda nayo ya mabadiliko ya sera, mabadiliko ya kanuni na mabadiliko ya miongozo kwenye sekta ya ardhi, nimwombe Mheshimiwa Waziri ajitahidi sana kuhusisha Chuo Kikuu cha Ardhi. Atambue wadau na watu ambao wamesomea kozi mbalimbali pale ili aweze kuwa-*accommodate* na hii *transformation* anayokwenda nayo asije akafika mbele

akarudi nyuma, akajikuta yuko peke yake na wale akawa amewaacha.

Mheshimiwa Spika, nitaje mambo matatu ambayo Mheshimiwa Rais ametukumbuka wadau wa sekta ya ardhi na ameyagusa kwa kiwango kikubwa na tumekuwa tukiyasema ndani ya Bunge hili. Kwanza, ndani ya Bunge hili tumekuwa tukizungumzia Mfuko wa Maendeleo ya Ardhi wa Taifa. Mfuko huu ulianzishwa mwaka 1991 kwenda 1992. Mwaka 2016 wakati Mifuko mbalimbali ya maendeleo ya sekta nyingi inafutwa na Mfuko huu ulifutwa. Sisi wadau wa sekta ya ardhi tuliona kama halijakaa sawasawa kwa sababu maelezo yake hayakuwa sawia.

Mheshimiwa Spika, leo ninavyozungumza na wewe Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mama Samia, baada ya kulisema ndani ya Bunge amerudisha Mfuko wa Maendeleo ya Ardhi wa Taifa na unakwenda kufanya kazi na kwa kuanza amewapa bilioni 15.1 ili kuunufaisha na kuunenepesha ule Mfuko na ametoa maelekezo mengine. Mheshimiwa Waziri amesema hapa bilioni 50 ambayo ipo kwenye KKK (Kupanga, Kupima na Kumilikisha) kwenye Halmashauri mbalimbali, marejesho ya fedha zile ziende zikanufaishe Mfuko huu. Tumekuwa tukisema ndani ya Bunge, ndiyo ushauri wa Bunge na umekuwa ndiyo mchango wangu kwa miaka yote mitatu. Mheshimiwa Waziri atupelekee salamu, tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kulifanya hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la pili ambalo tumelisema ndani ya michango yetu ya Wabunge, tumekuwa tukisema juu ya mradi wa uboreshaji wa usalama wa miliki, fedha zimekuja kwa ajili ya mkopo bilioni 345. Tulisema hapa fedha zile hatukuona kama ni sawia kwenda kupanga matumizi bora ya ardhi kwa vijiji 250 peke yake. Bilioni 300 ya mkopo kupanga matumizi bora kwa vijiji 250 ilikuwa inatumika zaidi ya bilioni tatu peke yake, bilioni mia tatu na ngapi ilikuwa inaenda wapi. Tukatoa ushauri hapa ndani ya Bunge tukamwomba Waziri aliyekuwepo Mheshimiwa Dkt. Angeline Mabula na Serikali kwa ujumla wake waka-*review* fedha ya mkopo iende ikafanye kazi ya kupanga matumizi bora ya ardhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, leo ninavyozungumza na wewe vijiji 1667 vimepangwa matumizi bora ya ardhi ndani ya mwaka mmoja na wametoka 2,400, leo tunazungumza vijiji 4100 vimepangiwa matumizi bora ya ardhi. Mheshimiwa Waziri, atupelekee salamu tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kuliona hili na wewe mwenyewe kwa utashi wa kisiasa kuamua kuridhia kuwapa fedha hawa watu kwa ajili ya kuboresha.

Mheshimiwa Spika, jambo la mwisho la kumshukuru Mheshimiwa Rais ni pale ambapo tumepata taarifa nzuri kwamba Sera ya Ardhi ya Taifa imekwishaidhinishwa, sasa kilichobaki ni Wizara hii na sekta hii kwenda kutoa elimu kwa wadau, wananchi ili angalau sera hii iweze kufanya kazi kwa manufaa ya wananchi.

Mheshimiwa Spika, tumekuwa tukisema hapa, moja ya changamoto kubwa ya migogoro inasababishwa na Sera ya Ardhi ya Taifa. Sera ya Ardhi ya Taifa ina miaka zaidi ya 20 *back* toka 1995, watu wanakua, changamoto zimekuwa kubwa na matumizi ya ardhi yanaongezeka kila leo. Sera ile haiendani na kasi ya ukuaji wa matumizi bora ya ardhi nchi hii, tukashauri maboresho yafanyike. Nimshukuru Mheshimiwa Waziri sana kupata taarifa kwamba sera ile sasa imekamilika na inakwenda kufanya kazi. Namwomba sasa kwa kuwa tayari imeidhinishwa aende akafanyie kazi sera hii, nenda akatoe elimu kwa haraka kwa sababu kuna baadhi ya maeneo yamekwama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, eneo mojawapo ni hadhi maalum kwa watu wa *diaspora*. Leo Waziri wa Mambo ya Nje ameanzisha mchakato kutoa hadhi maalum kwa wenzetu ambao ni wana asili ya Tanzania lakini wako nje ya nchi ili kwa ajili ya kupewa kumiliki ardhi. Wameshindwa kuendelea kwa sababu sera haiwatambui kama wahusika halisi wa kumiliki ardhi, wamekwama. Kwa hiyo, kutoa elimu kwako ku-*initiate* sera hii kutakwenda kumsaidia Waziri wa Mambo ya Nje ili kazi iweze kwenda kufanyika.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hayo mazuri ambayo yamefanyika kwenye sekta hii ya ardhi. Ninayo mambo kadhaa kama maoni na ushauri wangu. Jambo la kwanza, nimeona hapa umetoa taarifa ya kutokulipwa kwa kodi ya ardhi kwa

baadhi ya wananchi na mashirika ya umma. Hili lazima tuwe *serious* sana, Mheshimiwa Rais aliridhia na akafuta madeni yaliyokuwa ya muda mrefu ambayo ni ya kodi ya ardhi ambayo yalikuwa hayajalipwa na wananchi na taasisi mbalimbali, akaridhia akafuta ili watu wapate mwamko wa namna ya kuanza kulipa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, huzuni yangu na wasiwasi wangu ni pale ninapoona kwenye taarifa ya Waziri, pamoja na mazuri aliyofanya Mheshimiwa Rais maoni yake ya kufanya hivi bado mashirika ya umma yamelimbikiza zaidi ya bilioni 136, hayataki kulipa kodi ya ardhi. Sasa wanaturudisha kule kule nyuma, Mheshimiwa Rais anafuta madeni, wanaanza kulimbikiza madeni ambayo hayana msingi wowote. Nichukue nafasi hii kumwomba Mheshimiwa Waziri, kwa kuwa ametoa mwezi mmoja kwa wananchi kulipa kodi ya ardhi na namuunga mkono, akianza utekelezaji wa agizo lake aanze na haya mashirika ya umma haya ambayo yanamwangusha Mheshimiwa Rais, haya ambayo hayataki kulipa kodi ya ardhi na wakati wamepanga kwenye bajeti.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri ashughulike kwanza na haya mashirika ya umma, ndiyo aje kwa mwananchi mnyonge ambaye anatakiwa kulipa shilingi 2,000 wakati kuna bilioni 136 zimekaliwa na haya mashirika ya umma ambao ni wateule na wateuzi wa Mheshimiwa Rais. Hawafanyi vizuri na wanamwangusha Mheshimiwa Rais. Naomba uanze na haya mashirika walipe hii fedha kwa sababu hii fedha inakuangusha wewe, inaonekana unashindwa kutimiza lengo lako la makusanyo la kila mwaka kwa sababu kuna fedha kama *default* wameshikilia hawa watu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la pili kama ushauri wangu kwa Mheshimiwa Waziri ni kuhusu kuchelewa kulipwa kwa uthamini *(valuation report)*. Hili nimeona Mheshimiwa Waziri ametoa mwongozo, naomba asimamie mwongozo huu.

Mheshimiwa Spika, mwananchi anapopisha eneo kwa maslahi mapana ya umma, likafanyiwa uthamini na likatakiwa

lilipwe aidha na Serikali au taasisi fulani, Sheria ya Uthamini inasema eneo hili linatakiwa lilipwe na thamani ile inatakiwa ilipwe ndani ya miezi sita peke yake. Leo tunaona wananchi wanapisha maeneo baada ya kufanyika uthamini inachukua miaka sita, kumi na miaka nenda rudi kinyume kabisa na Sheria. Mheshimiwa Waziri kwa sababu ametoa mwongozo aende akakatae hili jambo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hili jambo kwanza linatengeneza mgogoro kwenye maeneo hayo. Pia, linazalisha na kuonekana wale wathamini (maskini ya Mungu) hawafai na wakati siyo kazi yao. Yule amekwishafanya uthamini, amekabidhi uthamini kwa mtu husika, asipolipa kiasi kinachotakiwa wanarudisha lawama na wanatengeneza mgogoro ambao hauna msingi. Niombe sana kama ni Serikali wakifanya uthamini walipe kwa wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la tatu ambalo ni ushauri wangu ni usimamizi wa masharti ya uendelezaji wa miliki. Mheshimiwa Waziri, ametoa siku 90 kwenye maeneo ambayo hayajaendelezwa yaweze kuendelezwa na yasipoendelezwa atagawa kwenye maeneo mengine. Sina shaka na namuunga mkono kwenye hili. Hata hivyo, tutambue kuna baadhi ya maeneo hayajaendelezwa kwa sababu huduma za kijamii zinakosekana.

Mheshimiwa Spika, mtu anashindwa kujenga nyumba au kiwanda kwa sababu hakuna barabara, hakuna maji na hakuna umeme kwenye eneo lile. Pia, kwa kuwa kwenye umiliki wa hati, mtu analipa hati analipa kitu kinaitwa *premium* (malipo ya mbele). *Premium* kazi yake ni kuhakikisha huduma hizi ninazosema zinapelekwa kwenye maeneo yale. Mheshimiwa Waziri, sasa utakapoanza utekelezaji wa kuwanyang'anya wale watu maeneo kwanza tazama hili linasababishwa na nini? Inawezekana anataka kujenga hakuna barabara, maji au umeme. Mheshimiwa Waziri akimnyang'anya na kwenda kwa mtu mwingine tutakuwa hatuwafanyii kazi watu hawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, namalizia dakika moja. la mwisho ambalo nimwombe Mheshimiwa Waziri ni namna ambavyo

Mabaraza ya Ardhi ya wilaya yanavyokuwa yakilalamikiwa kwa kuchukua rushwa na kutokutenda haki. Kesi ya Mabaraza ya Ardhi ndani ya vijiji kwenye haya maeneo, yanachukua zaidi ya miaka miwili kwenye kesi ndogo tu. Leo unakwenda unapigwa kalenda kwamba njoo miezi sita, njoo mwaka mmoja. Hawa wananchi ni wanyonge na wanaumia. Niombe Mheshimiwa Waziri aweze kulitazama hili kwa maboresho mazuri.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi na naomba nimalizie kwa kusema kazi nzuri imefanyika. Tunamshukuru sana Waziri, akaze moyo na naamini anafanya haya kwa kufuata mikono na miguu ya watangulizi wake Mheshimiwa Lukuvi na Mama yetu Mheshimiwa Dkt. Angeline Mabula. Mungu ambariki sana hongera sana na naunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Simai Hassan Sadiki, atafuatiwa na Mheshimiwa Munira Mustapha Khatib na Mheshimiwa Muharami Shabani Mkenge ajiandae.

**MHE. SIMAI HASSAN SADIKI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuwa mchangiaji. Kwanza, nitumie fursa hii kumshukuru sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kazi kubwa anazozifanya. Pili, nitumie fursa hii kumshukuru sana Mheshimiwa Waziri wa Ardhi pamoja na Wizara yake kwa jinsi wanavyofanya kazi. Hakika Watanzania wanaziona na wataziheshimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kusema kwamba, ieleweke ya kwamba ardhi siyo utajiri. Ardhi na rasilimali ardhi ni msingi mkuu wa uhai wa Taifa pamoja na wananchi wake. Pia, sisi kama wanandamu, msingi mkuu wa uhai wetu ni uhai. Tunayo haki ya kuishi na tunayo haki ya kumiliki mali ikiwemo ardhi. Hata hivyo, haki hii ya kumiliki ardhi na haki hii ya ardhi imekabiliwa na changamoto nyingi mno. Kwa sababu ya muda nitazungumza kwa uchache sana mambo matatu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la kwanza linaloikabili ardhi yetu ni changamoto ya ongezeko la idadi ya watu. Mara baada ya

kupata uhuru, ukiunganisha idadi ya watu wa Tanzania Bara na Tanzania Visiwani hatukufikia hata milioni 10. Hata hivyo, baada ya miaka 60 ya uhuru idadi hiyo imekuwa ni zaidi ya mara tano au sita zaidi kwani tumekuwa si chini ya milioni 60. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hii inaleta picha kwamba, mahitaji ya ardhi kwa shughuli za kiuchumi kwa maendeleo ya watu yameongezeka. Hata hivyo, licha ya ongezeko kubwa la watu ardhi tuliyokuwa nayo ni ileile bado haijakua. Kwa hiyo, inaonesha wazi kwamba kasi ya ongezeko la watu iko mbele zaidi ya kasi ya upangaji wa miji tuliyokuwa nayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la pili linalofanana na hili kwanza ni upanukaji wa miji kiholela. Hata yale maeneo ambayo yalikuwa yakitumika kwa ajili ya shughuli za kilimo sasa hivi yamekuwa miji. Yale maeneo ambayo yalikuwa yanatumika kwa shughuli za ufugaji sasa hivi yamekuwa miji. Upanukaji huu wa miji kiholela usiozingatia mipango bora ya matumizi ya ardhi unaweza ukaleta shida kitu ambacho unaweza ukazidisha thamani ardhi na ikawasababishia shida kwa wanyonge. Upanukaji wa miji uliopo sasa hivi hauendani sambamba kabisa na upangaji wa miji yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la tatu ni hili jambo la kiulimwengu la athari ya mabadiliko ya tabianchi. Huwezi ukazungumzia maendeleo ya nchi, huwezi ukazungumzia athari au changamoto zinazoikabili ardhi bila kuzungumzia athari ya mabadiliko ya tabianchi zinazoikabili Tanzania. Hii ni kwa sababu yale maeneo mengi ya fukwe, kando za mito na milima sasa hivi yameliwa. Maeneo ya kilimo kumetokea ukame, wananchi wafugaji wamehama maeneo yao wamehamia maeneo mengine na baadaye migogoro imetokea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa suluhisho la changamoto zote hizi tatu nilizozisema ni kuwa na Sera na Sheria bora. Niipongeze sana Serikali kwa kuanza mchakato mpya wa mapitio ya Sera ya Taifa ya Ardhi pamoja na Sheria zake. Hata hivyo, katika hili ni vizuri tukajifunza utaratibu uliokuwepo kwa waliotunga Sera na Sheria kwa wakati ule wa utawala wa Marehemu Mzee Mwinyi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Sera ya Taifa ya Ardhi ya mwaka 1995, mchakato wake ulikuwa ni tofauti sana na huu ambao tunauendesha sasa hivi. Yaani haukuwa mchakato wa kawaida kawaida hivi. Mchakato ule ulitoka hadharani ukawashirikisha wananchi. Mheshimiwa Rais alitengeneza Tume Maalum ya kushughulikia ardhi ambayo ilikuwa chini ya usimamizi wake yeye. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Tume ile ilitembea Tanzania nzima ikahoji watu, watu wakasikilizwa, wakashirikishwa na wakatoa maoni yao. Baadaye sasa maoni yale ndiyo yaliyotumika baada ya kuchakatwa yakatengeneza hizi Sera na Sheria ambazo tunazitumia sasa hivi. Hata hivyo, hofu yangu na wasiwasi wangu niliokuwa nao kwa huu mchakato unaoendelea sasa hivi ni juu ya ushirikishwaji wa wananchi mwamko bado ni mdogo mno. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, inawezekana hata wananchi hawajui nini kinachoendelea. Tukiendelea kunyamaza kimya bila kuwashirikisha wananchi inaweza kuja hoja tukatoka na sera na sheria ambazo zimetungwa katika meza. Sera ambazo zina uwezo wa kuwapa watu maneno ya kusema kwamba Serikali imetunga Sera dhidi ya wananchi au imetunga sheria dhidi ya wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tukumbuke kwamba Serikali ni taasisi na umma ndiyo nchi. Ardhi ni mali ya umma na siyo mali ya Serikali. Kwa hiyo, Serikali lazima iwahusishe wananchi katika masuala yote yanayohusu ardhi. Ni lazima Serikali iende chini kwa wananchi kuhusiana na huu mchakato. Wananchi wao ndiyo watakaosema kwa mujibu wa changamoto zilizopo sasa hivi, vipi viwe vipaumbele vya Sera yetu ya Taifa, vipi viwe vipaumbele vya sheria zetu tunazotarajia kutunga. Hata hivyo, tumeanza huu mchakato ingawa mchakato wa mwaka 1995 ulikuwa na kasoro zake lakini kitu cha msingi na kujivunia ni ule ushirikishwaji wa wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa hivi tumeanza mchakato, lakini lile vuguvugu ni dogo mno ukilinganisha na miaka ile. Jambo hili la

utungaji wa Sera na Sheria za Ardhi ni jambo zito na linahitaji mijadala ya Kitaifa. Kama tulivyokuwa na Tume ya Haki Jinai, basi umefikia wakati kwa sasa hivi ingekuwa ni kitu cha busara na hekima tukawa na Tume ya Haki Ardhi kutokana na unyeti wa jambo lenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niendeleze kwa kusema kwamba, migogoro inayoendelea kuibuka ni mingi. Wakati wa wasilisho la Kamati walielezea changamoto ambazo zinaendelea kutokea hususan katika masuala ya ulipaji wa fidia ilihali utaratibu wa Sheria za ulipaji wa Fidia za Ardhi na mambo mengine upo wazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, utaratibu unatutaka wazi kwamba, unapokwenda kuchukua ardhi ya mtu kwa matumizi ya umma kama ni Serikali, lipa fidia. Hata hivyo, kabla ya kulipa fidia lazima utafanya tathmini ambayo tathmini hiyo ndiyo itakayokwenda kukuongoza wewe katika utaratibu wa kulipa fidia. Ikifika miezi sita, kama umeshindwa kulipa fidia maana yake kutakuwa na ongezeko au riba. Hata hivyo, leo Serikali tumekuwa tunafika hata miaka 10 bila kulipa fidia na ardhi hizo tayari tunakuwa tumezichukua. Maana yake nini? Tuna uwezo wa kusababisha umaskini kwa wananchi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Sheria iko wazi, itakapofika zaidi ya miaka miwili maana yake ile tathmini iliyofanyika mwanzo inakufa na uende ukafanye upya kwa sababu ardhi ni mali ambayo haijawahi kushuka bei. Utajiri wa mwanzo na thamani ya mwanzo ya mwanadamu inatokana na ardhi. Taifa lolote lile mipaka yake inalindwa kutokana na ardhi.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja na ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Munira Mustapha Khatib, atafuatiwa na Mheshimiwa Muharami Shabani Mkenge na Mheshimiwa Dkt. John Pallangyo, ajiandae.

**MHE. MUNIRA MUSTAPHA KHATIB:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipatia nafasi ya kuweza kuchangia Wizara hii ya Ardhi. Pia, niungane na wenzangu kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Naibu Katibu Mkuu. Hakika wamekuwa mkifanya kazi kubwa na nzuri ndani ya Wizara hii ya Ardhi kwa muda mfupi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kuendelea kufanya kazi nzuri na kuongeza kasi ya upimaji ambapo zaidi ya vijiji 1,000 vimepimwa. Niendelee kuiomba Serikali iendelee kuongeza pesa kwenye Tume ya Upangaji wa Ardhi ili vijiji vingi viendelee kupimwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nichangie mchango wangu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na migogoro mingi kwenye Mabaraza ya Ardhi. Kwanza, kwenye haya Mabaraza ya Ardhi, Wenyeviti wamekuwa hawalipwi fedha zao kwa wakati, jambo ambalo linasababisha rushwa kubwa ndani ya Mabaraza haya. Niiombe Serikali iweze kuwalipa Mabaraza ya Ardhi fedha zao kwa wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la pili, kwenye Mabaraza ya Ardhi. Katika baadhi ya Wilaya bado hakuna Mabaraza ya Ardhi. Kwa hiyo, niiombe Serikali iangalie zile wilaya zitakazokuwa hazina Mabaraza ya Ardhi.

**MHE. COSATO D. CHUMI:** Mheshimiwa Spika, Taarifa.

**TAARIFA**

**SPIKA:** Mheshimiwa Munira kuna Taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Cosato Chumi.

**MHE. COSATO D. CHUMI:** Mheshimiwa Spika, naomba nimpe Mheshimiwa Munira Taarifa kwamba, hata sisi wananchi wa Mufindi mpaka sasa bado hatuna baraza hilo na ndicho

ambacho nilikuwa naandika hapa kwenye mchango wangu wa maandishi. Kwa hiyo, ni kweli kwamba kuna maeneo bado watu hawana Mabaraza ya Ardhi. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Munira, unaipokea Taarifa hiyo?

**MHE. MUNIRA MUSTAPHA KHATIB:** Mheshimiwa Spika, naipokea na niiombe Serikali iweze kuangalia zile wilaya zote ambazo zilikuwa hazijapatiwa bado Mabaraza ya Ardhi waendelee kuwapatia Mabaraza haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nataka niongelee uthamini. Wizara imekuwa ikifanya uthamini kwenye ile miradi ambayo ilikuwa inakuja kufanya miradi ya maendeleo lakini kumekuwa na changamoto kubwa ambayo imekuwa inasababisha migogoro ya ardhi. Wanafanya uthamini lakini fedha zinachelewa kutoka kwa wananchi. Wanatoa fedha baada ya miaka mitatu au minne mpaka miaka sita jambo ambalo Serikali yenyewe inapata hasara kwa sababu inabidi iende ikafanye tena uthamini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia wananchi wamefanyiwa uthamini leo wanakuja kulipwa baada ya miaka sita. Wengine wanataka kulipwa kwa fedha ileile ambayo walikuwa wamefanyiwa baada ya miaka sita jambo ambalo limekuwa linasababisha migogoro mingi kati ya Serikali na wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niiombe sana Serikali isifanye uthamini mpaka mradi unapokuwa upo tayari kwa ajili ya kutekeleza na ambapo Serikali tayari ina fedha za kuwalipa wale wananchi ndiyo iweze kufanya uthamini na waweze kulipa fidia kwa wakati. Nimwombe sana Mheshimiwa Waziri anabeba mzigo ambao ulikuwa siyo wake, lakini mathalan uthamini unafanywa ndani ya Wizara ya Ardhi huu mzigo tutaendelea kumbebesha yeye. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna fedha za miradi ya KKK. Kuna halmashauri hadi leo hii zinadaiwa zaidi ya shilingi bilioni 27 wakati kuna nyingine hazijapatiwa fedha hadi leo. Niiombe Wizara

itafute namna nzuri ya kuweza kurejesha fedha hizi ambazo kuna halmashauri nyingine zinahitaji fedha kwa ajili ya kwenda kupima vijiji vyetu. Niiombe sana Wizara itafute njia nzuri ya kuweza kurejesha fedha hizi ili halmashauri nyingine ambazo zina uhitaji ziweze kupatiwa fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna migogoro mikubwa ya ardhi. Migogoro hii inatokana zaidi na wawekezaji ambao walikuwa wanamiliki mashamba makubwa. Pia, kuna migogoro mingine ya hifadhi na wananchi. Niwaombe sana Serikali iangalie wawekezaji hawa ambao wanamiliki maeneo makubwa. Maeneo ambayo hayajaendelezwa wakae chini na wawekezaji hawa kuangalia namna nzuri ya kuweza kupunguza maeneo yale ili kuwapatia wananchi waweze kufanya shughuli za maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, migogoro hii inasababisha wananchi na wawekezaji kugombana jambo ambalo halileti tija kwenye nchi yetu. Tuiombe sana Serikali iangalie namna nzuri. Tusishikilie wawekezaji hawa wana hati tu na ni wamiliki, lakini tuangalie wananchi wetu wanakosa maeneo ya kulima, wanakosa maeneo ya ufugaji na wanakosa maeneo ya kujenga nyumba zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, watu bado tunaongezeka mwekezaji yupo mmoja, haendelezi maeneo. Kwa nini tusikae na wawekezaji hawa tukaangalia namna nzuri ya kuweza kuwapunguzia wananchi maeneo haya ili wapate maeneo ya kulima? Tunaingia mgogoro ambao hauna sababu. Mwekezaji anamiliki zaidi ya hekta 25,000 maeneo hayo hajaendeleza. Tuangalie namna nzuri mwekezaji apate eneo la kuendesha miradi yake na wananchi wapate eneo la kulima na kufugia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna jambo lingine la migogoro ya ardhi kati ya hifadhi na wananchi. Waende wakaangalie namna nzuri ya kuweka *beacon* ambazo zinaonekana kati ya hifadhi na eneo la mpaka la kijiji. Jambo hili litaondoa zaidi migogoro kati ya wananchi na hifadhi. Niiombe sana Wizara ishirikiane na Wizara ya

Maliasili na Utalii kuangalia namna nzuri ya kuweza kuondoa migogoro hii ya ardhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nataka niiongelee Tume ya Mipango. Tume ya Mipango imekuwa ikifanya kazi nzuri kwa sababu inapima vijiji lakini bado haijapewa fedha za kutosha. Tuiombe sana Serikali iwape pesa hii Tume waende wakapime vijiji, watakapowapa pesa tutaondoa migogoro mingi kati ya wananchi na Serikali. Pia tutakapoipa Tume tutaenda kupima maeneo mengi zaidi ya vijiji 1,100 ndani ya mwaka huu vimepimwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tutakapoendelea kuwapa fedha wataenda kupima vijiji vingi zaidi. Kwa hiyo, ushauri wangu kwa Serikali, iendelee kutoa fedha kwa Tume ili waweze kwenda kupima maendeo mengi zaidi.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Muharami Shabani Mkenge atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. John Danielson Pallangyo, Mheshimiwa Tumaini Bryceson Magessa, ajiandae.

Mheshimiwa Dkt. John Danielson Pallangyo, atafuatiwa na Mheshimiwa Tumaini Bryceson Magessa, Mheshimiwa Esther Nicholas Matiko, ajiandae.

**MHE. DKT. JOHN D. PALLANGYO:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru sana kwa nafasi hii ili nami nichangie kwenye hii Hotuba ya Wizara ya Ardhi. Nianze kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri. Kwa kweli nikiri kwamba anaitendea haki nafasi yake na ninamfahamu sana Mheshimiwa Jerry Silaa, alikuwa Mwenyekiti wangu kwenye Kamati ya *PIC*. Kazi anayoifanya hapa hata Mheshimiwa Rais ameiona akamkubali na akasema anaitambua. Nisimsahau naibu wake kwa sababu hawa wanafanya kazi pamoja, wakiwa pamoja na watumishi wote katika Wizara hii, wanafanya kazi nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ardhi ni mali, ardhi ni utajiri, ardhi ni *commodity* ambayo haipungui thamani, siku zote thamani yake inaongezeka. Kwa hiyo mwenye ardhi ana utajiri.

Mheshimiwa Spika, nimesimama hapa leo kuchangia kwa kifupi sana. Nikiri kwamba wenzangu wameshazungumza sana maneno mazuri na ya msingi. Niseme kwamba nataka kutoa ombi maalumu. Kwa kuzingatia na kwa kukiri kwamba ardhi ni mali; kule Meru kuna matatizo makubwa sana ni ya ardhi. Ukienda kwa *DC* pale utakuta mara kwa mara kuna watu wamekwenda kulalamika kwa sababu ya migogoro ya ardhi. Kwa hiyo nimesimama kuomba Serikali iangalie ni namna gani italinda huu utajiri kwa wale ambao tayari wana ardhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wananchi wa *KIA* walioondolewa kwenye eneo la *KIA* wameondolewa wakalipwa fidia ambazo hazitoshi chochote, hazimsaidii kitu mwananchi aliyeondolewa. Kwa ajili hiyo niombe Wizara iangalie na ikiwezekana ilete sheria hapa Bungeni, kwamba kabla ya kumtoa mwananchi kwenye ardhi ambayo ameikalia ambayo ni mali yake ihakikishe kwamba kuna ardhi mbadala ambayo imetengwa.

Mheshimiwa Spika, kwa wananchi ambao sasa hivi wameondolewa pale eneo la *KIA*; kuna shamba la *TPC* limerudishwa Serikalini, tunaomba Wizara iangale ili wale wananchi ambao wameondolewa kwenye maeneo yao wapatiwe ardhi mbadala ili waweze kuendelea kuishi. Si eneo la *KIA* tu, hata eneo la Momera ambako wananchi wameondolewa kwenye maeneo yao ili kupisha upanuzi wa Hifadhi ya Arusha. Tunaomba sana Mheshimiwa Waziri aliangalie hili.

Mheshimiwa Spika, hawa wananchi wote waliopoteza ardhi tusiwafanye wakawa maskini, tusiwafanye maisha yao yakaenda yakawa *miserable,* tuangalie ni namna gani tutalinda utajiri wao ili waendelee kuishi; kwa sababu wengine wamekaa kwenye yale maeneo waliyoondolewa kwa miaka 40. Kwa mfano pale *KIA* kuna watu ambao wamekaa na wamejenga kwa kushiriki kuchanganya zege; lakini leo wanaondolewa na kuitwa ni wavamizi. Kwa kweli sidhani kama kuwaita wavamizi ni sahihi, ni

kwamba tuna eneo limetengwa kwa ajili ya maendeleo ya kiwanja. Kwa hivyo tunaomba Mheshimiwa Waziri aliangalie sana hilo.

Mheshimiwa Spika, pia kuna shule tumejenga pale Shambarai Burka; ile shule tuliijenga lakini eneo lile halitoshi. Ombi langu, kuna wananchi ambao wamelizunguka lile eneo la shule, wao wako tayari kupisha ili waende mahali pengine lakini kwa kupatiwa ardhi mbadala.

Mheshimiwa Spika, kule kwenye lile shamba la *TPC* kuna maeneo ambayo yametengwa kwa ajili ya huduma za jamii. Tunaomba sana kwenye lile eneo tupate pale kama heka kumi lipatiwe sekondari ya Shambarai Burka ili libadilishwe sasa na wale wananchi ambao wamezunguka ile shule wao wahamie kule kwenye lile eneo ambalo litakuwa limetengwa kwenye lile shamba na yale maeneo yao yakabidhiwe shule ili shule iendelee kujengwa vizuri na kuwekwa *infrastructure* ambazo ni za muhimu. Hili ndilo ombi langu na nimesimama mahususi kwa ajili ya kutoa ombi hili.

Mheshimiwa Spika, baada ya ombi hili nina uhakika kabisa Mheshimiwa Waziri ameyachukua haya. Ninaomba kumalizia hapa na ninaunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Tumaini Bryceson Magessa atafuatiwa na Mheshimiwa Esther Nicholas Matiko, Mheshimiwa Dennis Lazaro Londo, ajiandae.

**MHE. TUMAINI B. MAGESSA:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru sana kwa fursa hii ya kuchangia Wizara nyeti sana ya Ardhi. Pia ninamshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa nafasi hii ya kutupatia uhai leo hii tena.

Mheshimiwa Spika, ninampongeza sana Mheshimiwa Waziri kwa kazi kubwa anayoifanya, Naibu Waziri ndugu yangu Mheshimiwa Geophrey Pinda, Katibu Mkuu ndugu yangu Sanga na Naibu Katibu Mkuu na watalaamu wote wa Wizara hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nianze kuchangia mchango wangu baada ya kuwa nimepitia ukurasa namba 15 unaozungumzia usimamizi wa masharti ya umiliki. Kama kuna mahali kuna migogoro mingi nchi hii ipo katika sehemu hii ya ardhi. Wizara wameendelea kujitahidi kila wakati kuhakikisha kwamba inapungua, lakini kadiri wanapopunguza ndivyo inavyoanza tena.

Mheshimiwa Spika, hapa kwenye usimamizi wa masharti ya umiliki bado kuna changamoto, ndipo mahali ambapo watu wanakwenda kuangalia zile hati lakini wanagundua kwamba kuna watu wengi tu hawana hati. Nimesikia wachangiaji wengi wakionesha kwamba 30% tu ya ardhi ndiyo iliyopimwa. Tuna kitu cha kufanya kwenye upimaji, na kama hatukifanyi sasa maana yake migogoro itazalishwa kila baada ya muda mfupi unaokuja.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hilo nilikuwa napitia Taarifa ya Mheshimiwa Waziri hapa ukurasa namba 28 nikaona ameweka mazingira yanaonesha wazi kwamba, ifahamike kuwa jukumu la Wizara ni kuratibu uthamini na wajibu wa kulipa fidia ni wajibu wa atakayenufaika na ardhi atakayokuwa amechukua, na kwa nini nimekimbilia kwenye uthamini huu, ni kwa sababu kuna uthamini na fidia. Jimboni ninakotoka kuna uchimbaji wa madini ya dhahabu na madini mengine, kama kuna changamoto ambayo inatafutiwa majibu na bado majibu yake hayajapatikana vizuri ni pale tunapozungumzia habari ya umiliki wa juu wa ardhi na umiliki wa chini wa ardhi *(surface right* na *mineral right)*.

Mheshimiwa Spika, mwananchi ambaye ameishi mahali fulani kwenye ardhi yake kwa zaidi ya miaka 40 au 50, kwa bahati nzuri imetokea dhahabu eneo la chini anaambiwa sasa anatakiwa afanyiwe tathmini afanye uthamini na apewe fidia. Sasa anatokaje pale? Bahati nzuri mchimbaji anayekuja anakuja kuchimba *open cast,* maana yake anakwenda kubomoa ile ardhi ya juu, kwa hiyo hawezi kuishi mahali pale. Kwa hiyo kumekuwa na changamoto kubwa ya hizi sheria mbili. Wananchi wengi wanalalamika kwa sababu kuna wakati wanaondolewa wanaambiwa pale ulipotoka unatakiwa ulipwe labda shilingi milioni mbili. Mwananchi huyo ameishi miaka 12, sasa akilipwa milioni mbili huko anakohamia milioni mbili itafanya kazi gani?

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo niombe sana na niishauri Serikali, watu wa ardhi na watu wa madini wakae chini, wamekwishafanya kazi nzuri sana, lakini waendelee kuboresha eneo hili kwa sababu migogoro yake bado inafukuta kwenye maeneo tuliyopo. Wananchi wengi wanaohama, kwa sababu inawezekana malipo yao ni kidogo, badala ya kuendelea wanapata taarifa kwamba yule aliyeingia kuchimba pale kwao amepata labda bilioni tano lakini yeye alichukua milioni tano ama milioni sita. Kwa hiyo anaendelea kuumia ndani ya moyo wake na kwa hiyo migogoro hii inashindwa kwisha.

Mheshimiwa Spika, tujue kabisa *surface right* itafanya nini kama mtu huya amekuja kuchimba eneo hilo. Ikiwezekana huyo anayekuja kuchimba ampe basi ubia kidogo hata wa *percent* wakati huyu mtu anaondoka kwenye eneo lile. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na hili ambalo nimelisema la *surface rights* kuna suala wanasema kwenye sheria, kwamba tunapokwenda kulipa hiyo fidia, fidia lazima iwe kamilifu, iwe ya haki na ilipwe kwa wakati. Kwa lugha ya Kisukuma wanasema *it should be fair full and prompt compensation.* Hoja yetu hapa ni kwamba je, hawa wanaokwenda kulipwa hizi fidia, je, ni fidia kamilifu? Ni fidia zinazolipwa kwa wakati? Nimesikia watu wengi wanasema kwamba mtu anakwenda kulipwa fidia baada ya miaka sita lakini sheria inasema baada ya miezi sita; na wanaonesha kwamba baada ya miezi sita inabidi iwekewe riba. Sasa je, riba hizo zinalipwa? Niombe tu Wizara iangalie namna ya kuwasaidia hawa ambao tunawazungumzia. Yako maeneo mengi ambayo ukienda sasa hivi utakuta migogoro mikubwa tuliyonayo ni ya hiyo *surface rights* na *mining rights.*

Mheshimiwa Spika, kingine ambacho nilitaka kuchangia eneo hili ni ukurasa namba 30 unaozungumzia Sheria ya Mipango Miji. Tumekuwa tunasema humu ndani kila siku kwamba sasa kuna maeneo ambayo inaonekana vijiji vimeiva kwa ajili ya kupandishwa, lakini havipandishi. Hapa kwenye ukurasa huu wa 30 ambao ameandika Mheshimiwa Waziri hapa anaonesha wanashughulikia kuona maeneo yaliyoiva. Tunayo maeneo mengi yaliyoiva, lakini hayapandishwi. Nina maeneo kule kwangu

Katoro, nimekuwa nikisema kila siku, yana jumla ya watu laki tatu kama na thelathini na moja. Sasa watu 331,000 unahisi eneo hili bado halijaiva? Limekwishaiva tayari, hivyo twende kwenye upandishaji.

Mheshimiwa Spika, nimpongeze Mkurugenzi wa Halmashauri ya Geita, tulikopeshwa fedha kwa ajili ya kupanga miji, zaidi ya milioni 600 ambazo zimekwisharudishwa. Sasa niwaombe watu wa ardhi, tukopesheni tena ili tuendelee kupanga miji yetu kwenye maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, yako maeneo katika eneo ambalo mimi natoka; Katoro nimekwishaitaja, Nyarugusu, Bukoli, Nyakagwe Rwamgasa, Chigunga na Chikobe na mengine mengi yamekwishaiva kwa ajili ya kupandishwa. Niwaombe sana watu wa ardhi hasa wale wanaoshughulika na upangaji wa miji waende wakalifanyie kazi.

Mheshimiwa Spika, suala la tatu ambalo ninataka kulizungumzia ni kuhusu Tume ya Matumizi Bora ya Ardhi. Tume hii imezungumziwa sana hapa. Hoja ni kwamba, tumekwishapima 30%, moja ya tatu, vijiji 4,000, lakini, kati ya hivyo vijiji 4,000 ni matumizi mangapi ya ardhi yanayoheshimiwa, kwa sababu tunaweza kuona kwamba tumepima eneo kubwa lakini wanaoheshimu wako tu ni vijiji 500.

Mheshimiwa Spika, ninafahamu matumizi bora ya ardhi sehemu nyingi tumeweka; kwamba hapa ni sehemu watu wataishi, sehemu fulani itakuwa ni kwa ajili ya ufugaji, sehemu fulani kwa ajili ya kilimo na maeneo ya wazi; lakini utashangaa hakuna anayemheshimu mwenzie. Sehemu ambayo tulisema ni kilimo utashangaa wafugaji wamekwenda kulisha ng'ombe; sehemu ambayo tumesema ni mifugo wakulima wamekwenda kulima huko; kwa hiyo unaweza ukashangaa. Shida tuliyonayo hapa ni usimamizi. Matumizi bora ya ardhi tuliyoyaweka yanasimamiwaje? Je, wananchi wanayo elimu ya kutosha ya kuhakikisha kwamba matumizi bora ya ardhi ambayo tumeyaweka yanaweza kufanyiwa kazi vizuri? Kama hawana tutaendelea kuona migogoro inaendelea.

Mheshimiwa Spika, katika hili la migogoro tumeunda mabaraza ya ardhi. Mabaraza mengi katika wilaya nyingi ambazo tunazo hayana Wenyeviti wa Mabaraza. Sasa kama haina Mwenyekiti wa Baraza, na labda Mwenyekiti wa Baraza Geita inabidi asafiri kutoka Mwanza. Mwanza kuna migogoro lakini anakwenda kushughulika na Baraza la Ardhi la Geita. Huyu anakwenda kila baada ya miezi mitatu au minne, migogoro kule inazidi kukua na inazidi kuwa mingi. Kwa hiyo niombe sana hawa wenyeviti nao waongezwe kwenye mabaraza haya. Pamoja na kuyaunda lakini yawe na wenyeviti ambao ni wakazi, hivyo wanaweza kutatua migogoro hii kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, tusipofanya hili migogoro hii baadaye inahama inakwenda mpaka kwenye jinai; watu wanaanza kufika mahali wanauana, wanaumizana kwa sababu uamuzi wa migogoro hiyo umechelewa. Inatakiwa mgogoro wowote uamuliwe kwenye *infant stage,* kwenye *stage* ile ya kwanza, lakini kwa bahati mbaya tunachelewa sana mpaka migogoro inakuwa mikubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na matumizi bora ya ardhi niseme tu wazi kwamba vijiji hivi ambavyo tumevipanga je, wananchi wamehusishwa? Kama hawajahusishwa vizuri matokeo yake ni kwamba yale tuliyoyaamua hayawezi kutekelezwa, na ndicho kinachotokea mara nyingi. Nimeona watu wengi wakishughulika na matumizi bora ya ardhi wanaanza hatua ya kwanza, hatua ya pili, hatua ya tatu, hatua ya mwisho inaonekana kuna wananchi wengine wanapinga. Sasa haya maeneo mengi ya namna hii tunashindwa kuvuka vizuri kwa sababu ya utaratibu uliotumika.

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa nimwombe Mheshimiwa Waziri; kwenye hoja ambayo niliisema mwanzo, ya *surface right na mining right* watu wake na wataalamu wake waende kule kutoa elimu kwa wananchi ili wananchi hao wajue utaratibu huu ukoje, ili tunapokwenda kwenye maamuzi ya mtu mmoja amekuja kuzalisha amechukua amenufaika na eneo fulani wananchi wawe na elimu. Bila hivyo tutakuwa na *resistance* kila wakati kumbe Wizara hizi mbili wanaweza kutengeneza timu nzuri

ya kutoa elimu kwenye maeneo yetu hayo na watu wakaishi kwa amani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya maneno haya, naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Dennis Lazaro Londo. Mheshimiwa Muharami Shabani Mkenge atafuatiwa na Mheshimiwa Abeid Ramadhani Ighondo, Mheshimiwa Condester Michael Sichalwe, ajiandae.

**MHE. MUHARAMI S. MKENGE:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru kwa kupata nafasi hii ya kuchangia kwenye Wizara yetu hii ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa siku ya leo.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa napenda kuchukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Ardhi kwa kazi kubwa ambayo anaifanya. Kwa kweli ni jambo lisilopingika kwamba Mheshimiwa Waziri tangu ameteuliwa katika Wizara hii anafanya kazi usiku na mchana ili kuhakikisha kwamba masuala ya ardhi yanapatiwa ufumbuzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tarehe 23/09/2023 Mheshimiwa Waziri alitembelea jimboni kwangu Bagamoyo kwenye kliniki ya ardhi ambayo iliandaliwa na Mkuu wetu wa Wilaya ya Bagamoyo. Kwa kweli nimshukuru sana na kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri. Siku hiyo aliyokuja amefanya kazi kubwa sana na nzuri ambayo leo hii inaleta matunda katika mji wetu wa Bagamoyo.

Mheshimiwa Spika, Jimbo la Bagamoyo lina migogoro mikubwa sana ya ardhi; bado ipo na inaendelea mpaka sasa haijamalizika. Katika Jimbo la Bagamoyo kuna kata mbili ambazo zinakuwa na migogoro mikubwa sana ya ardhi, Kata ya Mapinga pamoja na Kata ya Makurunge. Haya ni maeneo sugu kabisa kabisa kwa migogoro ya ardhi katika Jimbo la Bagamoyo.

Mheshimiwa Spika, nimpongeze sana Mheshimiwa Mkuu wetu wa Mkoa wa Pwani Alhaji Abubakari Kunenge; anafanya

kazi kubwa sana ya kuhakikisha kwamba maombi mengi ya migogoro ya ardhi anayatatua. Hata hivyo bado kuna changamoto ambazo zinajitokeza. Changamoto kubwa ambayo iko Bagamoyo ni uvamizi wa maeneo ya ardhi. Watu wengi wanavamia mashamba ya watu, wanavamia maeneo ya watu pasipo kujua na hatimaye migogoro hii ya ardhi inakwenda Mahakamani na kusababisha mahakama zinapotoa maamuzi yake watu wengi kuvunjiwa nyumba zao.

Mheshimiwa Spika, hivi karibuni tumepata changamoto kubwa sana katika Kitongoji cha Kimele ambapo zaidi ya nyumba 28 na 29 hivi zimevunjwa kutokana na migogoro ya ardhi baada ya mhusika mwenye ardhi yake kushinda kesi Mahakamani.

Mheshimiwa Spika, kwa kweli nilikuwa nataka niiombe Serikali, watu wengi na wananchi wengi wanauziwa haya maeneo ya ardhi kwa kutapeliwa na walio wengi hawajui. Mtu anaokoteza fedha yake kwa miaka mingi anaamua kujenga nyumba yake; nyumba anaweza ikajengwa kwa miaka kumi ama kumi na tano, lakini leo hii mtu anaposhinda mahakamani nyumba inabomolewa kwa dakika tano. Kwa kweli jambo hili tuliangaliwe. Sasa hivi kuwe na mazungumzo kati ya watu wenye maeneo ambayo yamevamiwa pamoja na wahusika ambao wamejenga katika maeneo hayo ili kuwaondolea adha na hasara kubwa ambayo wanaipata kwenye ujenzi ambao wamejiandaa kwa miaka mingi katika kujenga nyumba hizo.

Mheshimiwa Spika, mgogoro mwingine uliopo Bagamoyo ni suala la *GN* ambayo imewekwa katika Kata ya Zinga pamoja na ya Kilomo kupisha Mradi wa *EPZA;* huu mgogoro huu ni mkubwa sana. Mheshimiwa Waziri huu mgogoro tulikuwa tunaomba, kwa sababu *EPZD* washa-*declare* kwamba kuna maeneo ambayo watayaacha hawatoendelea nayo. Kwa hiyo, ninaomba ikiwezekana muende mkaondoe *GN* katika yale maeneo ambayo *EPZA* wameyaacha ili wananchi hao waweze kuyatumia maeneo yao kwa uhuru kwa sababu leo hii mtu akitaka kwenda kuuza eneo lake anaambiwa huwezi kuuza kwa sababu eneo hili lina *GN* ambayo iko chini ya *EPZA;* wakati *EPZA* hawalitumii lile eneo. Kwa hiyo, ninamwomba sana Mheshimiwa Waziri

alishughulikie suala hilo ili wananchi wengi waweze kunufaika na maeneo yao.

Mheshimiwa Spika, kuna suala lingine ambalo lina mgogoro mkubwa sana, Mheshimiwa Waziri kuna mgogoro katika Shamba la Razaba, hili linafahamika. Shamba lile ni moja kwa moja 100% ni mali ya Serikali, hilo halipingiki lakini kuna wananchi pale wamehamia miaka mingi sana na wale waliohamia miaka mingi wengine wamefariki wameacha vizazi vyao pale. Wale watoto walioachwa hawajui kama hili eneo baba yetu kavamia; baba kafa kaacha watoto na watoto wanajua kwamba hili eneo ni mali yao, kwa hiyo, wana haki ya kuishi pale lakini lile eneo ni mali ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, wananchi wale wamenituma wanasema kwamba hawapingi maamuzi ya Serikali kwamba lile eneo siyo mali ya Serikali, lile eneo wazazi wao walivamia na wengine walikwenda pale miaka mingi karibuni miaka 15 au 20, lakini wanaomba pale katika eneo la Razaba, kuna hekta karibuni 12,000; walikuwa wanaomba angalau Serikali iwaonee huruma ikate japo hekta 3,000 iwapimie viwanja ili wawe na makazi ya kukaa wapate sehemu ya kuishi kuliko ambavyo wanahangaika hivi sasa, Serikali ikiwaambia waondoke hapa hili eneo siyo lao hawana pakwenda.

Mheshimiwa Spika, ninamwomba sana Mheshimiwa Waziri aliangalie kwa macho ya huruma jambo hili. Yeye ni msikivu na anajua jinsi gani wananchi wanavyopata tabu katika suala zima la ardhi. Kwa hiyo, naomba sana awaonee huruma wananchi hawa wa Razaba *at least* eneo hili ligawanywe japo hekta hizo 3,000 waweze kugawiwa ili waweze kukatiwa viwanja na kuweza kuishi.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo nataka kulizungumzia ni masuala ya mabaraza ya ardhi; kwa kweli kidogo bado utendaji kazi wao una malalamiko mengi. Wananchi wengi wanalalamika kwamba mabaraza haya bado haki haitendeki. Kwa hiyo, waangalie ni jinsi gani sasa kutafuta watu ambao ni

makini ambao watakuwa wanatenda haki katika haya mabaraza ili wananchi wasipoteze haki zao.

Mheshimiwa Spika, la mwisho napenda kumshukuru sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mama yetu Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa anayoifanya. Nashukuru kwa pale Bagamoyo kufuta mashamba mawili; Shamba la Kiembeni, Mapinga pamoja na shamba la kwa Mchina, Kisutu - Bagamoyo; mashamba haya yamefutiwa hati na sasa hivi yako chini ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, nimwombe Mheshimiwa Waziri hili Shamba la Mapinga 99% au 100% limejengwa nyumba za watu. Ninaomba basi Serikali ichukue nafasi kurasimisha rasmi lile eneo kwa wananchi wa Mapinga pale maeneo ya Kiembeni ili waweze kulipia kodi za ardhi waendelee kuishi katika lile eneo kwa amani zaidi kwa sababu ni wananchi wetu. Zipo zaidi ya nyumba 4,000 pale, kwa hiyo, leo hii ukisema kwamba unawavunjia au unawaondoa wale watu wanakuwa hawana pakwenda.

Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi hii kukuomba Mheshimiwa Waziri kwa sababu Mheshimiwa Rais ameridhia kufuta yale maeneo basi wananchi hawa wapate nafasi kuweza kuishi katika maeneo hayo; warasimishiwe. *Otherwise* nampongeza sana Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu Waziri pamoja na timu yenu yote kwa kazi kubwa anayoifanya. Migogoro ya ardhi Bagamoyo wataitatua; naona kwa mwendo wanaokwenda tutafika hatua tutafika pazuri.

Mheshimiwa Spika, kwa hayo machache, naomba kuunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Abeid Ramadhan Ighondo atafuatiwa na Mheshimiwa Condester Michael Sichalwe, Mheshimiwa Constantine John Kanyasu ajiandae.

**MHE. ABEID R. IGHONDO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa fursa ili nichangie katika Wizara yetu hii ya Ardhi ambayo ni muhimu kwa ajili ya maendeleo ya nchi yetu. Kwa

muktadha huo naomba nianze kwanza kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri Jerry Silaa pamoja na Naibu wake kwa utendaji mzuri. Kimsingi tumemwona Mheshimiwa Waziri akipambana sana kuhakikisha ana-*over whole* na kuleta mabadiliko na maendeleo katika sekta hii ikiwa ni pamoja na kuondoa migogoro, kutenda haki na niendelee kumpa moyo kwamba aendelee kuchapa kazi. Kikubwa tu ni kwamba watendaji walioko chini yake hasa kule kwenye maeneo ya wilaya ndiyo kunakotakiwa kuboresha na kumulikwa hasa.

Mheshimiwa Spika, nampongeza pia Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan ambaye tunaona kazi yake kwenye maeneo mengi: kwenye ardhi, kwenye utendaji haki na utoaji haki anapambana kuhakikisha Watanzania wanaishi katika maisha ya haki katika kutendeana haki.

Mheshimiwa Spika, leo nina mambo machache na kubwa katika uchangiaji wangu nataka nizungumzie kwenye upande wa kupata hati miliki za ardhi na hasa hasa ule uaminifu wa watumishi wetu, hasa katika Jiji la Dodoma. Natoa ushauri sana hapa kwa watendaji wa ardhi. Nampa Mheshimiwa Waziri aangalie Idara ya Ardhi katika Jiji la Dodoma kuna matatizo makubwa, ndiyo chanzo cha migogoro ambayo wananchi wanakosa haki zao na wananyang'anywa ardhi yaani ni usimamizi wa watendaji wale wa ardhi (wataalamu) wanashiriki moja kwa moja kuwanyang'anya wananchi maeneo. Wao wanajigeuza kuwa wanasheria na wanajigeuza kuwa ni madalali; sasa hili jambo linakera. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wananchi wanakwenda na *genuine cases* lakini haziendi mpaka mwisho ni danadana tupu. Ninamwomba sana Mheshimiwa Waziri amulike sana eneo hili, linamchafua na linachafua kabisa hata taswira ya Mheshimiwa Rais ambaye amesimama kuhakikisha wananchi wanatendewa haki. Wananchi wengi wanakuwa ni wanyonge na mnafahamu mambo haya ya ardhi yanahusisha hata pia kutoa fedha kwa maana ya kulipia na nini, hasa kwenye maeneo ya kumilikishwa.

Mheshimiwa Spika, sasa mwananchi mnyonge anapokuwa hana uwezo aangaliwe, lakini hawa watu wetu wa ardhi wanapoona mwananchi hana uwezo wanampiga danadana mwisho wanammilikisha mtu mwingine au ananyang'anywa kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninazo *cases* zaidi ya tatu, sitaki kutaja watu majina hapa, Mheshimiwa Waziri nitakuletea hayo majina; kwa ridhaa yako nitampa Mheshimiwa Waziri hizi *cases* ili azifanyie kazi aangalie, yaani mwananchi anakuwa kama digidigi kwenye nchi yake, hili siyo sawa. Namwomba sana Mheshimiwa Waziri alitazame kwa karibu eneo hili, alijaribu kuna wakati hapa Jiji la Dodoma zaidi ya watumishi 90 waliondolewa, lakini vile vimelea bado vipo havijaisha. Namwomba sana asogelee hili eneo asilitazame juu juu tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ni kuhusu haya Mabaraza ya Ardhi ya Wilaya pamoja na yale ya kata; mengi hayana Wenyeviti; unakuta mwenyekiti mmoja anahudumia wilaya tatu au mbili. Sasa ule mzigo ni mkubwa na wanafahamu maeneo haya ya ardhi migogoro inaanzia kwenye vijiji uende kwenye kata. Sasa ukichanganya wilaya tatu mwenyekiti mmoja inakuwa ni mzigo mkubwa. Kwa hiyo, naomba sana eneo hili Wenyeviti wa Ardhi waajiriwe ili waweze kufanya kazi ya kutoa haki kwa wananchi wetu.

Mheshimiwa Spika, hapo hapo kwenye mabaraza ya kata, tumeyang'oa meno kwa kusema wawe washauri tu. Sasa wanabaki kushauri mambo ambayo wakati mwingine yangehitajika kufanyiwa maamuzi ili mwananchi apate haki, lakini wanaambiwa wanashauri na wanaposhauri huku juu tunasema hakuna wenyeviti wa Mabaraza ya Ardhi ya Wilaya; maamuzi yanakuwa hayafanyiki wananchi wanabaki na malalamiko bila kutatuliwa kero zao na kupatiwa haki zao. Kwa hiyo, hili nalo nashauri Mheshimiwa Waziri alitazame kwa karibu ili kuhakikisha Wenyeviti wa Mabaraza ya Ardhi kila Wilaya wanapatikana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ni kuhusu kupima maeneo kwenye miji yetu midogo, Mji wetu wa Ilongero ndiyo tunasema ni makao makuu ya halmashauri lakini nimeona juhudi nzuri zinafanyika pale kupima maeneo, lakini ni eneo dogo sana. Maeneo mengi ya wananchi hayajapimwa na tusipopima ina maana tunaandaa *squatters,* tunaandaa maeneo yasiyokuwa rasmi; yaani unakuwa ni mji mchafu. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri naomba sana ututazame kwenye maeneo yetu haya ya miji midogo hasa hasa Mji wa Ilongero ambayo ndiyo makao makuu ya wilaya, upimwe wote ili maeneo haya yaweze kupangika vizuri na pia tukipima yanapanda thamani. Kwa hiyo, wananchi wetu nao waweze kupata angalau nini kwenye maeneo yao haya.

Mheshimiwa Spika, hiyo iende sambamba na miji midogo iliyoko kwenye wilaya yangu ikiwemo Mji wa Mtinko upimwe, Mji wa Ngamu upimwe wote, Itaja nayo ni mji unaokuwa na wenyewe unatakiwa upimwe na pale Msange papimwe ili sasa twende kwenye maeneo yetu huko tunakoenda tuhakikishe kwamba tunakuwa na miji iliyopangika na ambayo inakaa vizuri.

Mheshimiwa Spika, kwa leo nilikuwa na mchango huu mdogo, lakini ninasisitiza sana pale kwenye eneo la migogoro katika Jiji la Dodoma, Maafisa Ardhi wa Jiji letu la Dodoma walio wengi siyo waaminifu; wapo wachache ambao ni wazuri, lakini walio wengi *cases* za Wabunge na wananchi wa kawaida malalamiko ni mengi.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema haya, ninaomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Condester Michael Sichalwe atafuatiwa na Mheshimiwa Constantine John Kanyasu na Mheshimiwa Boniphace Mwita Getere ajiandae.

**MHE. CONDESTER M. SICHALWE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi, lakini karibu tena tuliku-*miss* sana. Wakati Baba wa Taifa anapigania sisi tuweze kupata

uhuru na baada ya kupata uhuru alitangaza maadui watatu: maradhi, ujinga na umaskini; kwa muktadha huo kwenye janga hilo moja la ujinga zaidi ya Watanzania 95 walikuwa hawawezi kusoma na kuandika. Pia, tulikuwa hatuna lugha moja ambayo inaweza ikatuunganisha kama Watanganyika hata na Wazanzibar ili tuweze kuwasiliana.

Mheshimiwa Spika, bado viongozi hawa wawili waliendelea kuwa wazalendo pamoja na kujua Watanganyika hawajui kusoma na kuandika, hawawezi kuwasiliana na hakuna *document* yoyote ambayo wangeweza kuidadavua lakini kiongozi huyu na wenzake waliendelea kuwa waaminifu na wazalendo kuendelea kutulindia sisi vizazi ambao tupo mpaka leo akina Condester kwamba tukizaliwa ardhi ya Watanzania iwe ni mali yetu.

Mheshimiwa Spika, tunaona nchi nyingine viongozi ambao walipigania kupata uhuru waliweza kujimegea maeneo makubwa. Tunavyoongea sasa inawezekana Baba wa Taifa angeamua kusema Nyanda za juu Kusini yote ni eneo lake, tungesema nini? Sasa hivi ingekuwa ni ardhi ya kina Makongoro au angeweza kusema Mbuga za Wanyama zote ni zake. Kwa hiyo, sasa hivi kila mtalii ambaye angekuwa akiingia nchini kwetu hela zote zingekuwa zinaenda kwenye familia ya Baba wa Taifa, lakini sisi tumekiri na tumekuwa ni mashahidi kuona sisi na kina Makongoro tunaishi sote kama Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Baba wa Taifa huyo huyo alishawahi kusema kwamba hatuwezi kutatua matatizo yetu kwa kujidanganya kuwa hayapo Mheshimiwa Waziri naomba niungane na maneno haya ya Baba wa Taifa. Tunakiri na kukubali kwamba bado ipo changamoto ndani ya Wizara ya Ardhi kwenye migogoro. Wakati siku mlipokuwa mnazindua *Clinic* ya Ardhi hapa Bungeni tarehe 23 Mei, 2024, ninanukuu; “Mheshimiwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Kassim Majaliwa anazitaka taasisi zinazoshughulika na masuala ya jinai kuhakikisha zinawashughulikia wavamizi wa ardhi kama wanavyoshughulikia wahalifu wa jinai nyingine.”

Mheshimiwa Spika, Waziri Mkuu Majaliwa alitoa kauli hiyo tarehe 23 Mei, 2024, katika hotuba yake iliyosomwa kwa niaba na Mheshimiwa Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge na Uratibu Mheshimiwa Jenista Mhagama. Hata Waziri Mkuu anakiri kwamba bado kuna watu ambao wana changamoto kwenye nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, naomba niendelee kunukuu tena maneno ya Baba wa Taifa; mwaka 1958 wakati anaendelea kupigania uhuru wa Watanganyika aliyasema maneno haya; "Katika hii nchi kama yetu ambamo Waafrika ni maskini na wageni ni matajjiri, kuna uwezekano mkubwa kwamba Waafrika wakiruhusiwa kuuza ardhi yao katika miaka 80 au 100 ijayo ardhi yote ya Tanganyika itamilikiwa na matajiri na wenyeji watakuwa watwana, lakini hata kama wageni wasingekuwa matajiri, litaibuka la Watanganyika matajiri na wajanja, tukiruhusu ardhi iuzwe kama kanzu katika muda mchache tutakuwa na kundi dogo la Waafrika wakiwa na ardhi na walio wengi watakuwa watwana." *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nataka kurudia hapa ambapo Baba wa Taifa anasema kwamba; litaibuka tabaka la Watanganyika matajiri na wajanja, *as we are speaking now* Watanzania. Nachelea kusema kwamba viongozi hawa ni wazalendo; tunamwona hata Rais wa kwanza wa Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar, Rais Karume, baada ya Mapinduzi Matukufu kila wilaya iliyoko Zanzibar aliweza kujenga nyumba za Wazanzibari wenzake na kuwapatia waweze kuishi bure, ni uzalendo wa pekee, angeamua kuwaacha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri nije ndani ya Wizara yako, ninakiri na kukubali kwamba migogoro ya ardhi ipo ile ambayo ni ya kiasili kama ambavyo ni desturi wanadamu kugombana tu; mnaweza mkagombana na kwenye ardhi hivyo hivyo, lakini migogoro hii ya ardhi inapoibuka tulitegemea Wizara ya Ardhi wao wawe kama Mahakama kuzuia hiyo migogoro au ikiwezekana kuisitisha isiwepo kabisa, lakini ndani ya Wizara yako wapo baadhi ya watumishi, hapa nieleweke siyo wote, wapo ambao ni wazalendo; wapo baadhi ya watumishi ambao siyo

waaminifu kwa uchu wao wa madaraka na kutaka kujipatia pesa haraka haraka wameendelea kuwa chanzo cha kuchochea migogoro kwa wenzao hapa nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wapo baadhi ya Watanzania wanauana na wanagombana na wanakufa kwa presha, lakini ni kwa sababu ya watumishi hawa wasiokuwa waaminifu. Katika hili naomba nitume salamu zangu za kipekee kwa Kamishna wetu Msaidizi wa Mkoa wa Songwe amejitahidi kuwa mzalendo katika hili, iko *scenario* moja hapo mbele nitaeleza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri ameanzisha hiyo *Clinic* yake ya Ardhi; nataka kukwambia ndege wanaofanana huruka kwa pamoja. Mheshimiwa Waziri atakuwa analima shamba wakienda kulala usiku wenzao wanaleta magugu wanarudisha tena kwenye lile shamba. Wanaamka tena wanakusanya takataka, wenzao tena wanaendelea kuleta, ndiyo hilo kundi ambalo liko ndani ya Wizara yako. Ili hiyo *Clinic* ya Ardhi iweze kufanya vizuri na kuleta matunda kikamilifu na kuonesha hali ya uzalendo kama viongozi wetu waliopita ni lazima aone namna ya ku-*reform* tena baadhi ya watumishi ambao wako ndani ya Wizara ya Ardhi. Wameshakubuhu na wameshaota mizizi na wameshaona kwamba wao wako hawapaswi hata kuguswa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hapa Dodoma ni mfano dhahiri Wabunge wengine wataungana na mimi kwamba nini kinachoendelea hapa Dodoma. Mheshimiwa Waziri yupo mwananchi mmoja anatokea kule Kijiji cha Kamsamba anaitwa Mzee Kauzeni toka mimi naomba kura mwaka 2020 kila kiongozi anayemwona anaenda kulia shida yake kwa ajili ya ardhi, lakini kwa sababu wapo Watanzania wachache wajanja na matajiri ambao wameshirikiana na baadhi ya watu wa ardhi kumpora maskini huyu ardhi na kuendelea kumfanya aendelee kuwa mtwana. Wazo la Mheshimiwa Waziri litafanya vizuri kama atachagua ndege ambao wataweza kuruka nao kwa pamoja, atatafuta kundi la watu ambao lazima watambue wanaowarudisha nyuma na watu sahihi ambao watawafanya waweze kwenda mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naendelea kumnukuu Baba wa Taifa, anasema kwamba; "Ardhi ni msingi wa maisha ya mwanadamu na Watanzania wote waitumie wa ajili ya kuwekeza kwa maendeleo yao ya baadaye kwa sababu ardhi ni mali ya Taifa, Serikali ione kwamba inatumia ardhi kwa manufaa ya Taifa lote kwa ujumla na si kwa manufaa ya mtu mmoja mmoja au kikundi cha watu wachache." *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hapa nchini kuna kikundi cha watu wachache, watu wachache au mtu mmoja mmoja ambao wameinuka wamekuwa ndiyo hawa Watanganyika waliosemwa zamani hawa, ambao wao wamekuwa ni wajanja na ni matajiri, lengo lao ni kuwafanya wenzao kuwa watwana.

Mheshimiwa Spika, kule kwenye Jimbo la Momba, sisi wote ni Watanzania na ni haki ya kila Mtanzania kumiliki ardhi mahali popote maadamu anafuata utaratibu, lakini wapo Watanzania wenzetu ambao, sisi tumezaliwa kwenye ardhi hiyo, tukaitunza na kuilinda toka vizazi vya babu zetu na babu zetu. Wao kwa ajili ya ujanja wao na utajiri wao, wamefika ndani ya jimbo letu na kutaka kutugeuza sisi kuwa watumwa ndani ya ardhi yetu wenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitumie nafasi hii kumwomba Mheshimiwa Waziri aitishe hati zote ambazo ziko ndani ya Jimbo la Momba, hati zote, ziwe ni za kimila aweze kuzihakiki. Nimeshawahi kuchangia hapa nikamwambia Mheshimiwa Waziri, kuhusu *scenario* moja, Mtanzania mmoja ambaye amefika Kijiji cha Msungwe alipofika hapo akajifanya kuwa Tajiri na huyo ni mmojawapo tu. Wako wengi zaidi ya 30 na wengine hawawezi hata kuguswa wanasema wametumwa huko juu. Huko juu ni wapi kama Baba wa Taifa yeye mwenyewe aliamua kuipigania nchi hii akawaachia, huko juu ni wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika hili wasiwachafue viongozi…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Mheshimiwa kengele ya pili imeshagonga.

**MHE. CONDESTER M. SICHALWE:** Mheshimiwa Spika, wasimchafue hata Mheshimiwa Rais, wametumwa huko juu wapi? Amehodhi ardhi yote yeye kwa makusudi mazima na kijiji kizima kiendelee kunyanyasika. Mheshimiwa Waziri, kwa kuona yeye ni mjanja kaenda kujipatia hati kutoka kwenye kijiji kingine kwa sababu alijua kijiji hiki hakiwezi kumpatia hati. Aliyetusaidia kutambua hilo ni Kamishna wa Mkoa wa Songwe, nampongeza sana kwa moyo wake wa kizalendo. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Condester kengele ya pili imeshagonga.

**MHE. CONDESTER M. SICHALWE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana, lakini tunaomba hawa matajiri na wajanja ambao Baba wa Taifa aliwakataa tuone Mheshimiwa Waziri akiwashughulikia hadharani bila kuwaogopa. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Constantine John Kanyasu atafuatiwa na Mheshimiwa Profesa Patrick Alois Ndakidemi. Mheshimiwa Cosato David Chumi ajiandae. *(Makofi)*

**MHE. CONSTANTINE J. KANYASU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Naomba nianze kwa kuunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri. Kipekee nampongeza Mheshimiwa Waziri, yeye na timu yake yote kwa kazi nzuri ambayo wanaendelea kufanya. Nataka kumwambia Mheshimiwa Waziri, ana Katibu Mkuu mzuri sana, ni mnyenyekevu na ni mtu ambaye nimepata bahati ya kumfahamu tangu akiwa Mwanza, lakini anasikiliza. Sasa naamini na wengine wataiga mfano wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwenye vipaumbele vya Wizara, Mheshimiwa Waziri amesema anaongeza kasi ya upangaji na upimaji na umilikishaji wa ardhi. Pia, akasema kuimarisha mfumo wa utatuzi wa migogoro ya ardhi na mengine yaliyoko huko chini. Tukienda pia kwenye Sera ya Ardhi, Toleo la mwaka 2023 na bahati nzuri Mheshimiwa Waziri alipitisha mwenyewe juzi, amesema hata kwenye mpangilio, suala la kuimarisha Mfumo wa Umiliki wa Ardhi na kuwezesha raia wote kuwa na haki sawa na kupata ardhi na kulinda ardhi ya Serikali limewekwa kwenye

vipaumbele namba moja. Pia kuwepo na uwazi na haki katika utoaji wa ardhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nikiendelea kwenye eneo hilo, kuimarisha mifumo ya utatuzi wa migogoro ya ardhi na kuimarisha utawala bora. Nimeona nianze kusema maneno haya ambayo Mheshimiwa Waziri mwenyewe ameyaweka kwenye vipaumbele, lakini pia yametajwa vizuri kwenye Sera ya Ardhi. Niweke kumbukumbu vizuri kwamba nimesema naunga mkono hatuba yako Mheshimiwa Waziri na haya nitakayosema hayamaanishi kwamba siungi mkono. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwanza, sisi tuna mgogoro mkubwa sana wa ardhi pale Geita Mjini. Ni mgogoro ambao tumeishirikisha sana ofisi yako, Wizara ya Madini imeshiriki sana, mgogoro huu unatokana na sheria mbili ambazo zote zinatoa haki za kumiliki ardhi ile, lakini hazimpi haki mmiliki wa asili wa ardhi ile kupata haki yake.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Madini inampa mtu mwenye leseni *Mining Right* (haki ya madini) yaliyopo chini ya ardhi. Pia, inampa haki ya kuzuia maendelezo mengine mpaka atakapotaka kuitumia. Matumizi ya Sheria hii yamesababisha kwa miaka 25 wananchi wa takriban wa mitaa saba, ardhi yao kupokwa na kunyimwa haki ya kumiliki ardhi kwa sababu ya matumizi ya sheria hii. Tumemshirikisha *Chief Valuer* amekuja, namshukuru sana Mheshimiwa Waziri wa Madini, tumekaa naye wiki nzima Geita, amepekua vipengele vyote vya sheria, amekosa sheria ambayo inawalazimisha wale wenye leseni kutoa hata *shake hand* hata *ex gratia* hata kulipa fidia, lakini wanaendelea kuwa na haki ya kuzuia matumizi ya ardhi ya eneo lile. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo nataka kuweka hapa kumbukumbu vizuri kwamba sera ya Waziri haiwatendei haki wananchi hawa, yeye mwenyewe ameweka ya kwanza. Pili, sheria ambazo zipo haziwatendei haki, vipaumbele ambavyo vipo kwenye Wizara yako, haviwatendei haki. Mheshimiwa Waziri naomba, nilifikiria kukamata shilingi mpaka nijue hatma ya

wananchi hawa ikoje, lakini sitakamata shilingi yako. Namwomba jambo hili tunataka tupate suluhu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tumemwambia Waziri wa Madini maeneo yote ambayo yana migogoro hawa watu wana-*renew license* kwa nini yasiondolewe kwenye leseni yao? Ni kwa sababu vile vijiji sasa vinakua, watu wanaongezeka na ardhi haiongezeki. Kwenye taarifa ya Waziri amesema *by 2050* kwa Tanzania ardhi itakuwa haipo, *almost* itakuwa haipo kwa sababu Watanzania wanaongezeka kwa kasi. Sasa hii ni haki yao ambayo ofisi ya Waziri inayo. nataka nimwambie Mheshimiwa Waziri kwamba, wananchi wa Nyakabale na Nyamalembo wanamsubiri kwa hamu aende akawape hatima ya miaka 25 ya Serikali kushindwa kutafuta suluhu ya mgogoro wa ardhi ambao upo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Ardhi ilikuja na Kamati ya Mawaziri Nane, wakatoa maelekezo, wakamwelekeza Afisa Ardhi kwamba jambo hili walishughulikie na kamishna alikuwepo. Kila wakisoma sheria wanashindwa kwenda kupima, hawawezi kupima kwa sababu *coordinates* zinaingiliana na kusomana. Sasa tunaishi kama tunaishi mjini na nimeangalia kwenye vipaumbele vya Mheshimiwa Waziri wa Ardhi. Nilidhani kwenye moja ya vipaumbele angesema kuifanya Wizara hii kuwa chanzo kikuu cha mapato cha nchi. Sasa kwa sababu haipo hata kwenye vipaumbele, ndiyo maana mitaa saba haijapimwa, ipo mjini hiyo, mitaa saba haijapimwa. Eneo takriban kilometa 154 halijapimwa, linakaliwa na watu na hakuna kodi ya ardhi inayokusanywa. Wananchi hawalipi chochote na mwekezaji hawalipi watu fidia, ni kwa sababu kitu hiki siyo kipaumbele kwenye Wizara yako Mheshimiwa Waziri. Kama kingekuwa kipaumbele kwamba kuifanya ardhi ya Tanzania kwanza imilikiwe kwa haki lakini pili iwe chanzo cha mapato, hii ardhi ingepimwa na mgogoro huu ungeisha. Kwa hiyo, nimwombe Mheshimiwa Waziri kwenye eneo hilo lishughulikiwe vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la pili, amesema kwenye kuimarisha utatuzi wa migogoro ya ardhi. Kwanza nampongeza kwa kliniki yako aliyoianzisha, nampongeza sana. Ilianza mwaka jana alianzisha Mheshimiwa Mama Mabula, nampongeza sana na

Waziri amekuja ameiimarisha. Nataka nimshauri na namshauri tu kwa nia njema, amesema hapa Mheshimiwa Ighondo, atakwenda kwenye wilaya ngapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, shida ninayoiona kwenye eneo hili, hebu twende mbali zaidi Mheshimiwa Waziri, kama anaweza kwenda kwenye kliniki ya siku moja akatatua mgogoro wa miaka 20 na hakuna *extra force* aliyoleta, yaani hakuna nyongeza yaani hujaleta Wizara tofauti, yaani Wizara yako ileile, hapo watu wako wale wale, lakini yeye akafika siku moja akatatua mgogoro basi tatizo liko ndani ya Wizara yako. Ingekuwa akifika, analeta watu wa Mahakama, analeta watu sijui wa nani, halafu wanasaidia kwenye kutatua migogoro, tungesema hizi kliniki uwepo wake una sababu za msingi kuendelea kwa mfumo huu uliopo. Kwa sababu mimi ni muumini sana wa operesheni, naamini siku atakaposema amechoka, migogoro itazaliana maradufu kwa sababu watengenezaji wa migogoro wako ndani ya Wizara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, *I am so much worried* kwamba Mheshimiwa Waziri ni Mwanasheria, leo ana bahati hiyo, anaenda pale anatatua mgogoro. Mgogoro wowote unaoutatua kwa siku moja nina uhakika unaacha *grievance* kwa watu wengine kwa sababu yuko mtu pengine amekuwa na mategemeo kwamba anayo hiyo haki. Sasa kwa bahati mbaya sana ikatokea siku hiyo mtu akagundua haki yake haikutendeka vizuri kesho yake akaenda Mahakamani akakupinga Mheshimiwa Waziri na yeye alishatoa haki hiyo pale, huko baadaye watu watasema Waziri alitumia madaraka yake vibaya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa mimi nikataka nishauri, hebu tengeneza mfumo ndani, uwepo wako kama haupo migogoro hii iweze kutatuliwa bila wasiwasi. Yaani hata unavyozungumza hapa, mtu aliyeko Kigoma, akutane na *One Stop Center* ileile ambayo wewe ukifika pale unapata majibu na unatoa suluhu ya jambo lile pale pale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nataka nitoe mfano, watu wa *PCCB* Wilayani kwangu Geita walifanya uchunguzi wakagundua kwamba kuna mwananchi ambaye Baraza la Ardhi mpaka na

Mahakama Kuu iliamua anyang'anywe ardhi, lakini kumbe watu wake walipeleka ramani *fake* kutoa ushahidi ikasababisha yule mwananchi ashinde. Sasa kuirudisha Mahakamani anahitaji kibali tena huku. Najua akienda Waziri akisoma zile *document* ataamuru apewe sasa hapo, nitaona kuna vitu viwili, moja, yule wa zamani anaweza kuendelea na hukumu yake aliyoipata Mahakama Kuu, lakini huyu ana vielelezo vya kutosha kwamba ile hukumu ilikuwa *induced* na ramani feki ambayo ilisababisha yule mtu apate haki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa jambo hili nadhani tutengeneze *one stop center,* iwe na wataalamu, kwa sababu ni wale wale hakuna *externals* wanaokuja pale ndani, waimarishwe, watengenezewe mfumo ambao haki inaweza ikatendeka *in your absence*. *Otherwise* nadhani Mheshimiwa Waziri anafanya kazi yake vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la tatu, Mheshimiwa Waziri tuna shida kwenye maeneo ya wakulima na wafugaji na juzi nilisema kwenye semina ya Waziri. Katika nchi hii wamezungumza Wabunge wengine kuhusu Mpango wa Matumizi Bora ya Ardhi, kwanza hauheshimiwi, pili haufuatwi, tatu, *speed* yake ni ndogo sana, lakini ongezeko la mifugo na wakulima ni kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nimalizie, katika nchi hii popote alipo mfugaji analima, popote alipo mkulima anafuga. Matokeo yake vijiji vya wafugaji ni wakulima na vijiji vya wakulima ni wafugaji. Sasa kinachotokea ni nini? Kadiri wanavyolima, wanawafukuza wafugaji kusogea kwenye hifadhi na kadiri wanavyoenda kwenye hifadhi wanaanzisha vijiji vipya. Maeneo yote 33% ni hifadhi yataisha na hakuna siku yatatosha. Lazima tuje na sheria kali ya kumtaka mkulima abaki kwenye maeneo ya wakulima na mfugaji akae kwenye maeneo ya wafugaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Kabla hatujaendelea na uchangiaji kuna wageni wako hapa Bungeni ambao wamekuja baada ya tangazo la awali la wageni.

Tunao wageni 55 wa Mheshimiwa Antony Peter Mavunde, Waziri wa Madini, hawa ni wanafunzi na watumishi kutoka Shule ya Msingi Chimwaga, Jijini Dodoma. Wageni mkitangazwa mnasimama. *(Makofi)*

Haya, naambiwa walisinzia kidogo, haya simameni baada ya kuamshwa. Haya, karibuni sana walimu na wanafunzi kutoka Shule hii ya Msingi Chimwaga. *(Makofi)*

Pia wapo wageni 37 wa Mheshimiwa Jumanne Sagini ambaye ni Naibu Waziri wa Katiba na Sheria. Hawa ni vijana wa *TK Movement* kutoka Mkoa wa Mara, wakiongozwa na Christian Myombe, karibuni sana. *(Makofi)*

Wapo wageni wengine wa Mheshimiwa Jumanne Sagini ambao ni viongozi na watendaji wa chama na Serikali kutoka Butiama wakiongozwa na Mwenyekiti wa CCM wilaya, Ndugu Marwa Siagi, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni watano wa Mheshimiwa Benaya Kapinga, hawa ni wapiga kura wake kutoka Mbinga, karibuni sana. *(Makofi)*

Tuna wageni 120 wa Mheshimiwa Ng'wasi Kamani ambao ni vijana wa *TK Movement* kutoka Mwanza, karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge nilikuwa nimeshamtaja Mheshimiwa Profesa Patrick Alois Ndakidemi, tutamalizia na Mheshimiwa Cosato David Chumi.

**MHE. PROF. PATRICK A. NDAKIDEMI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa fursa. Nianze kwa kumshukuru Mheshimiwa Rais kwa uteuzi makini ambao ametuletea, kijana wetu Mheshimiwa Jerry Silaa. Huyu kijana amekuwa faraja kwa Watanzania wote kwa kusema kweli, kwa hiyo, tunamshukuru sana Rais kwa hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia nampongeza Rais na kumshukuru kwa kuongeza bajeti ya Wizara hii kwani imeongezeka kutoka shilingi bilioni 163.17 mpaka shilingi bilioni 171.37. Kwa hiyo tunamshukuru sana Rais, hii itamsaidia Waziri na wenzake wote kufanya kazi kwa umakini wa hali ya juu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunaona mageuzi makubwa sana yanafanyika kwenye wizara na kuna utendaji, kuna mambo mazuri yanaendelea. Nimpongeze Waziri na wasaidizi wake wote, hongera kwa kliniki za ardhi ambazo zimekuwa zinaendelea nchi nzima. Tunampa moyo, amekuwa faraja kwa Watanzania wengi, aendelee hivyo hivyo tusikukatishe tamaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niseme huyu Waziri wetu amekuwa mfano wa kuigwa kwa sababu wakitaka kumpa rushwa anatangaza anasema; "Sitaki mimi nina pesa yangu." Kwa hiyo, hongera sana, ashikili hapo hapo na Mwalimu Nyerere alikuwa anapenda viongozi kama Mheshimiwa Waziri, aendelee hivyo hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwenye hizi kliniki hata tukienda hapo kwenye meza yake anatusikiliza, siyo zile tu. Nimshukuru yeye binafsi, nilimletea hoja za watu wangu kule Moshi, kwa mfano Mabogini wameitatua. Nilimletea hoja ya wapiga kura wangu wa Kibosho Mashariki na Uru, ameniahidi atakuja kutatua kule kule kwa hiyo tunakushukuru sana. Ila, kama walivyosema wenzangu wachache, kuna watu bado wanakukwamisha na naomba awe makini kwenye hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nilivyokuwa naingia hapa Bungeni nimekutana na Mama mmoja anaitwa Elizabeth Donald Mbozu ni mpigakura wa Mheshimiwa Mavunde, anakutafuta, ni mama kilema lakini alikuwa anamtafuta yeye. Alishasema kwamba apewe ardhi yake na watendaji wake wanampiga danadana hawajampa hiyo ardhi. Sasa yule mama ni kilema…

**SPIKA:** Mheshimiwa Profesa ngoja kwanza, hilo ni jina la mtu hiyo kilema au ni mlemavu?

**MHE. PROF. PATRICK A. NDAKIDEMI:** Mheshimiwa Spika, mwenye shida.

**SPIKA:** Ni mlemavu?

**MHE. PROF. PATRICK A. NDAKIDEMI:** Mheshimiwa Spika, mwenye ulemavu.

**SPIKA:** Basi anaitwa mwenye ulemavu siyo kilema.

**MHE. PROF. PATRICK A. NDAKIDEMI:** Mheshimiwa Spika, anadai haki yake huyu mlemavu.

**SPIKA:** Ndiyo nakutengenezea lugha vizuri, anaitwa mtu mwenye…

**MHE. PROF. PATRICK A. NDAKIDEMI:** Mheshimiwa Spika, anaitwa Elizabeth Donald Mbozu. *(Makofi/Kicheko)*

**SPIKA:** Sijui jina lake, ila anaitwa mtu mwenye ulemavu, haitwi kilema, ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. PROF. PATRICK A. NDAKIDEMI:** Mheshimiwa Spika, ndiyo ni mwenye ulemavu. Kwa hiyo, nimwombe tumsaidie huyu kusema kweli. Hao wanaompiga danadana sijui nia yao ni nini na wewe ulishasema apewe eneo lake. Sasa kama kuna mtu mkubwa kuliko wewe tunataka tujue.

Mheshimiwa Spika, basi mchango wangu utajikita kwenye ardhi. Nianze kwa kusema kwamba Tanzania imejaaliwa kuwa na ardhi yenye utajiri mkubwa; kuna watu, madini, gesi, misitu, mazao na vitu vingine vingi. Mwenyezi Mungu alitupa rasilimali hizi ili tuzitawale na zitusaidie, lakini cha kusikitisha utajiri huu ambao tumepewa na Mungu, kwa bahati mbaya haujioneshi kwenye maisha ya kawaida ya Watanzania. Bado watu wetu ni maskini na ni kwa sababu mahali fulani masuala ya umiliki wa ardhi yameleta matatizo kwa Watanzania wetu. Kwa hiyo niombe kwamba kuna vitu vya kuangalia kwa umakini wa hali ya juu ili watu waweze kunufaika na hii rasilimali ardhi ambayo tumepewa.

Mheshimiwa Spika, kikubwa, wakoloni walivyokuja walitunga sheria za kutunyang'anya ardhi yetu na wakawakabidhi watu wachache. Walijitwalia zile ardhi zetu wakajimilikisha miaka 33, 66 mpaka 99. Nitatoa mfano kule Kilimanjaro, Eneo la Uchagani karibu lote, Arusha na Manyara eneo kubwa lilichukuliwa na hawa wakoloni na wakajimilikisha, lakini tunamshukuru sana Baba wa Taifa tulipopata uhuru alikuja akataifisha hizi mali akazirudisha mikononi mwa umma, ikiwa ni pamoja na mashamba na zile nyumba ambazo walikuwa wametunyonya wakajitwalia. Sasa pamoja na kumilikishwa hivi vitu na Baba wa Taifa bado tumekuwa na changamoto kwenye hizi rasilimali zetu za ardhi ambazo zipo.

Mheshimiwa Spika, nitatoa mfano, narudia tena kule Kilimanjaro maeneo ya Siha Wilaya ya Siha, Wilaya ya Hai na Wilaya ya Moshi, sehemu kubwa ilikuwa imemilikiwa na wanalima kahawa, kwa hiyo wazawa wa kule wengi hawana ardhi ya kulima na wazee wengi ambao wametokea maeneo haya, wamekuwa manamba wanakwenda kufanya kazi kwenye haya mashamba, kwa hiyo kuna tatizo hapo.

Mheshimiwa Spika, yale mashamba ambayo yalibinafsishwa wakapewa Vyama vya Ushirika, hayatumiki vizuri vilevile. Wale viongozi wa ushirika kwa namna moja hawajayaendeleza na kwa wale ambao wameyaendeleza, bado kuna chengachenga ambazo wanafanya kuyauza kinyemela na kuyatoa kwa watu kinyemela, watu wamekuwa na shida ya ardhi lakini hawapati huduma. Kwa hiyo namwomba kitu kimoja, suala la umiliki wa ardhi ambapo watu wachache wanapewa na kuacha kuwamilikisha watu wengi ni la kuangalia kwa umakini wa hali ya juu katika nchi yetu ili tuhakikishe watu wote wanapata haki yao ya kuimiliki na kuitumia ardhi, hasa wazawa wa nchi hii. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, niseme kitu kimoja ambacho nimekigundua, kuna watu hawajamwelewa Mheshimiwa Bashe kwenye lile suala lake la *BBT*. Mheshimiwa Bashe ile programu ambayo ameianzisha ni programu muhimu sana ambapo anataka awamilikishe vijana wazawa, wananchi wazawa wa

Kitanzania ardhi. Tunakuwa na wawekezaji wa Kitanzania ambao watakuwa wanazalisha mazao hapahapa badala ya kuwapa watu wachache. Nitatoa mfano, badala ya kumpa mtu mmoja hekta 500, Mheshimiwa Bashe hapa anawapa vijana 50 wanazalisha, huyu mtu mmoja akifa, ule mradi wake unakuwa umekwisha, umekwenda vibaya, lakini ukiwamilikisha watu 49 ardhi hiyohiyo, ekari 500, akifa yule mmoja, wale 49 wataendeleza ule mradi na watakuwa ni wazawa na wanatoa huduma kwa nchi yao. Kwa hiyo naomba tuishauri Serikali kwenye suala la umilikishaji wa ardhi, wawe waangalifu na tuwamilikishe. Ushauri wangu sasa ni kwamba tuwamilikishe vijana wazawa ardhi ili waweze kuzalisha na kuliendeleza Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu wa pili kwenye umiliki wa ardhi, Wizara ya Ardhi kwa namna yoyote ile ilinde haki kwa nguvu zote, haki za kumiliki ardhi kwa wazawa. Pale ambapo tunaona ardhi imetumika vibaya, mamlaka za juu, Mheshimiwa Waziri umshauri Mheshimiwa Rais vizuri, hata kama ni kule Kilimanjaro kwamba watu hawajayatumia yale mashamba vizuri, a-*revoke* zile *ownership*, wafute zile hati wapewe watu ambao wanastahili, watakaotumia hiii ardhi sawasawa, tuwape wazawa ardhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kule kwetu watu wengi hawana mashamba, huwa tunaomba hata twende mahali kotekote watu wameshajiandikisha, lakini pale tuna mashamba ambayo yanatumika vibaya, watu hawajapewa zile ardhi. Tunaomba, wale ambao wameshajiridhisha, wakifanya utafiti wakiona hayatumiki vizuri, m-*revoke* zile hati zao tuwape wananchi ardhi.

Mheshimiwa Spika, naomba, huko mbele ya safari, suala la kuwamilikisha ardhi watu wachache liangaliwe kwa umakini wa hali ya juu. Kabla hatujampa mtu ardhi, tutafakari sana kwa sababu watu huwa wanatumia wale viongozi wa vijiji kwa kuwa wanazo pesa, anakwenda, anawapa pesa, hajawashirikisha wananchi, wanapitisha muhtasari wanachukua mashamba makubwa ambayo watu wetu wanaumia.

Mheshimiwa Spika, vile Vyama vya Ushirika, zile Bodi za yale mashamba, wakishahongwa pesa kidogo, wanapitisha *ownership* ya mashamba inakwenda kwa watu ambao siyo sahihi. Kwa hiyo, tujitahidi tuhakikishe tumeshirikisha wananchi wote kwenye masuala yoyote yale yanayohusiana na ardhi yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa, tunaendelea kumwombea Mungu aendelee kumbariki Mheshimiwa Silaa Jerry, anapotoa maamuzi magumu hasa yanayohusiana na haki ya kumiliki ardhi kwa Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba kuunga mkono hoja na tunakutakia kila la kheri katika kutekeleza majukumu yako. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Tunaendelea na Mheshimiwa Cosato David Chumi.

**MHE. COSATO D. CHUMI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi na Mwenyezi Mungu atubariki wote kabisa humu ndani ya Bunge ili tuweze kutoa mawazo ambayo yatasaidia katika kuboresha sekta yetu ya ardhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa naanza na pongezi. Nampongeza Mheshimiwa Rais, kwanza kwa kutuletea Mheshimiwa Jerry Silaa. Bahati nzuri namfahamu toka akiwa Mwenyekiti wa UVCCM, lakini na mimi nikifanya kazi pale Ilala Boma, enzi zile pale kwa Mzee Makamba tulikuwa tunaita Ilala Boma kwa Mzee Makamba, yeye alikuwa Meya, kwa hiyo najua utendaji wake na ninavyokumbuka, alikuwa Meya mdogo kuliko wote. Kwa hiyo, napongeza sana uteuzi hii na sisi tunaendelea kumwombea utendaji mwema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pongezi ziende mpaka kwa Mheshimiwa Naibu Waziri Mheshimiwa Geophrey Pinda, pengine wasiofahamu Mheshimiwa Pinda alinipokea mimi Wizara ya Mambo ya Nje na mimi nimekuja kumpokea hapa Mjengoni, nilikuwa namwonesha korido za hapa Bungeni kama yeye alivyokuwa ananionesha pale *Foreign Affairs* na alinifundisha kazi, lazima nikiri. Kwa hiyo

nafahamu utendaji wake na moyo wake wa kujitoa katika utendaji wa kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nampongeza pia Mheshimiwa Katibu Mkuu *Engineer* Sanga, Naibu Katibu Mkuu, Kamishna Mathew, Makamishna wote, Watendaji na wataalam wa ardhi kwa ujumla kwa sababu mara nyingi binadamu tumezoea kulaumu, lakini kuna wakati pia tupongeze kwa sababu pia wanafanya kazi katika mazingira ambayo ni *delicate* na tete.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili napongeza kuhusu hizi *clinic* za ardhi. Ni kweli Waheshimiwa wengi wamesema kwamba Mheshimiwa Waziri huwezi kwenda kila sehemu, lakini nataka kusema kwamba, hizi *clinic* kwa kiasi fulani, zimeleta amshaamsha fulani ambayo pia imeleta woga kwa matapeli wa ardhi. Kwa kweli hilo lazima tuseme, kama mtu sasa hivi alikuwa ni mjanja mjanja wa mambo ya ardhi, akienda kule *YouTube* akaona ile mikutano ya Waziri anavyowabana wale watu, mmh! Anapata moyo wa kurudi nyuma?

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo pamoja na kwamba hawezi kufika kila sehemu, lakini kuna amsha amsha fulani ameleta, kwa kweli imesaidia sana. Nilimwambia kama shemeji yake, anatakiwa aanze kunichangia bando kwa sababu usiku nachelewa kulala, naangalia zile *YouTube* mwanzo mpaka mwisho. *In fact*, zinasaidia sana naangalia siyo kujifurahisha, najifunza pia namna ya ku-*solve* migogoro na namna ya kusikiliza kila upande na namna ya kufikia hitimisho, kwa hiyo nampongeza sana Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napongeza pia mradi wa uboreshaji usalama wa milki za ardhi ambao unatekelezwa pia katika Halmashauri ya Mji wa Mafinga, lakini Mheshimiwa Waziri namwomba, Mafinga bado hatujaanza utekelezaji wa ule mradi, baadhi ya maeneo wameanza lakini kuna baadhi ya maeneo nimeambiwa kuna changamoto, wamesimama kwa sababu ya taratibu fulani fulani, hebu atukwamue katika jambo hilo ili mambo yaweze kwenda vizuri.

Mheshimiwa Spika, sasa baada ya pongezi hizi, nakuja kwenye hoja zangu. Nitakuwa na hoja zangu kama mbili. Kwanza, wananchi wa Wilaya ya Mufindi, nadhani hili jambo nitakuwa nasema sasa ni mwaka wa nane toka nimekuwa Mbunge hapa 2015, tunaomba tuwe na Baraza letu la Ardhi kwa sababu wananchi wanatoka Mgololo, wanatoka Malangali, wanatoka Mtula, wanatoka Bumilahinga, ni gharama kwenda kupata huduma Iringa Mjini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwanza mwananchi atoke asafiri afike Mafinga, alale, atoke Mafinga aende Iringa akapate huduma, saa nyingine tena alale Iringa Mjini, arudi tena alale Mafinga aanze kutawanyika kwenda huko maeneo ya vijijini, kwa kweli gharama inakuwa ni kubwa kwa wananchi. Nimelisema na naomba Mheshimiwa Waziri, watu wengi hapa jinsi walivyoongea, ameonesha kwamba yeye ni tumaini, tumaini la watu wengi, tumaini hata la watu ambao walipoteza haki zao miaka 20, 30, wamepata ardhi zao, wamepata haki zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, namwomba kwa ajili ya wananchi wa Wilaya ya Mufindi, tupate Baraza la Ardhi, liwe pale Mafinga. Mara ya mwisho nilipouliza, niliambiwa kwamba, tayari kila kitu kiko vizuri, kiko hatua za mwisho, sijui wamepata Wenyeviti kama wangapi, wanasubiri sijui vibali utumishi, *something like that*, lakini kwa wananchi kwa kweli itoshe jamani kusema Mheshimiwa Rais anafanya kazi nzuri sana, sasa ile kazi nzuri iguse kila maeneo.

Mheshimiwa Spika, mahali ambako naomba iguse, ni Baraza la Ardhi Wilaya ya Mufindi ili wananchi wapate huduma, wasogezewe huduma karibu. Kwa kweli nitaomba katika hitimisho, mimi sina kawaida ya kushika shilingi, niliwahi kushika shilingi zamani wakati wa mambo ya vinyungu, kwa hiyo mimi sitashika shilingi ila namwomba tu Mheshimiwa Waziri anisaidie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala la pili, Mafinga tumetenga ekari 750 na tuliomba pale tupime kwa ajili ya *Industrial Park*. Ninavyozungumza hapa, Wilaya ya Mufindi ina viwanda kama 35 vya mazao ya misitu, vimetawanyika tawanyika. Tulisema tutenge

eneo, tuwe na eneo kwa ajili ya viwanda, wakati walipokuwa wanatupa semina ya Mradi huu wa *LTIP*, niliomba kwamba, tuingize pia lile eneo, lakini Kamishna Mathew akashauri kwamba hapana huu mradi uende peke yake tutawapa *Revolving Fund*.

Mheshimiwa Spika, nafahamu kwamba kuna maeneo ambako kuna Halmashauri zilipewa hizi fedha, zikatumia ndivyo sivyo, sasa dhambi za halmashauri nyingine, tusiumie sisi wananchi wa Mafinga! Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Waziri tuone uwezekano na sisi kupewa hizo fedha za *revolving fund*, tuweze kupima eneo la *industrial park*. Sisi kwa sababu tuko eneo ambalo ni ukanda wa kuelekea *SADC*, naamini litakuwa na tija siyo tu kwa wananchi wa Mafinga na kwa Taifa zima kwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, watu wengi wamezungumza hapa kuhusu migogoro Dodoma. Kwa sababu ya kazi yangu ya Mwakilishi wa wananchi na vikao vinafanyika Dodoma, kwa kiasi fulani maisha yangu yanakuwa pia Dodoma. Kwa hiyo natoa ushauri, migogoro hapa Dodoma imetajwa sana, kwa hiyo namwomba Mheshimiwa Waziri, arejee kwanza mapungufu gani yalitokana na ile Sheria iliyokuwa imeunda *CDA*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ile sheria kwa namna moja au nyingine imekuwa ni chanzo cha migogoro hii iliyopo kwa sababu, ile Sheria jinsi ilivyokuwa, ilikuwa inatoa eneo, linapimwa, viwanja anagawiwa Mheshimiwa Chumi, viwanja anagawiwa Mheshimiwa Lucy, viwanja anagawiwa Mheshimiwa Silaa, kesho mtu anakuja anasema hili eneo lilikuwa la kwetu, lakini tayari ile ardhi ameshapewa mtu. Kwa hiyo, namwomba Waziri, naweza nikawa tofauti na watu wengine, hebu kaangalieni ile sheria ilikuwa na mapungufu gani na imeacha makovu gani kwenye Jiji la Dodoma, vinginevyo Mheshimiwa Waziri, sitetei watumishi wala sitetei wataalam, lakini mta-*victimize* watumishi, mta-*victimize* wataalam, mwisho wa siku kumbe ni makovu yaliyoachwa kutokana na ile sheria iliyokuwa imeunda *CDA*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hili Mheshimiwa Waziri akilifanyia kazi kwa utulivu, namwambia, hata akija Malaika hapa Jiji la Dodoma, migogoro haiwezi kwisha kwa sababu kuna makovu yameachwa

kutokana na ile Sheria iliyokuwa ya *CDA*, kwa hiyo namwomba sana.

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo, namwomba, kwa hapa Dodoma, kuna migogoro Mheshimiwa Waziri ndiyo maana Dodoma inaonekana kama ni migogoro, ni migogoro, ni migogoro. Kuna ile migogoro ya makundi, kwa mfano kuna hawa watu 562 maarufu kama Nala Sheli Mbili. Toka mwaka 2019 walikuwa wanapimiwa na watu wa *Global*, lakini mpaka leo unakuta hadi Mheshimiwa Lukuvi alikuwepo alishughulikia hili jambo, amekuja Mama Mabula ameshughulikia hili jambo, sasa kwa sababu hatukamilishi mpaka hitimisho la hii migogoro ndiyo maana Dodoma inaonekana kama ni Dodoma ya migogoro.

Mheshimiwa Spika, ukienda pale Ndachi, kuna mgogoro wa makundi yaani wa watu wengi, ukienda pale Kizota Mbuyuni ambapo kuna mgogoro kati ya wananchi na wawekezaji, kwa hiyo hii migogoro ya makundi makundi, naomba Mheshimiwa Waziri, ajipe wiki mbili aamue kwamba kama alivyoweza kufanya masuluhisho kwenye maeneo mengine, basi ajipe muda kwamba hii migogoro ya makundi ya watu wengi hapa Dodoma, nataka nihitimishe na ikamilike. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mara nyingi migogoro hii inaenda inafikia 90% inaishia njiani, anakuja kiongozi mwingine anaanza sifuri, inafikia 90%, inaishia njiani, kwa hiyo namwomba aangalie hili jambo.

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa naendelea kusisitiza na kushauri, hizi kliniki Mheshimiwa Waziri nimeona anafanya maeneo ya mijini, hebu pia ajipe nafasi hata wiki mbili zingine, aende *level* ya vijiji nako wananchi tunaweza tukajikuta wana changamoto mbalimbali ambazo pia akawa amesaidia kuzipatia suluhisho.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nashukuru, namwomba mambo makubwa mawili, Baraza la Ardhi Wilaya ya Mufindi na kupewa fedha *Revolving Fund Industrial Park*.

Mheshimiwa Spika, namshukuru kwa kunipa nafasi, Mungu atubariki wote na nawapongeza Yanga kwa lile gwaride zuri, hata kama mimi ni Simba, Mungu awabariki sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa sehemu ya kwanza ya kukutana kwetu leo.

Waheshimiwa Wabunge, ninalo tangazo moja hapa mbele, Waheshimiwa Wabunge wanatangaziwa na Katibu wa Bunge kuwa Wizara ya Ujenzi na taasisi zake inawaalika kwenye maonesho ya siku mbili ambayo yataanza leo na yatahitimishwa kesho katika viwanja vya Bunge.

Waheshimiwa Wabunge, maonesho hayo yanahusu mafanikio ya miaka mitatu ya uongozi wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa hiyo Waheshimiwa Wabunge wote wanakaribishwa hapo wakaone hayo ambayo yameshafanyika na yale yanayokusudiwa kufanyika.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, nasitisha shughuli za Bunge mpaka saa kumi na moja kamili jioni leo.

*(Saa 6.54 Mchana Bunge Lilisitishwa hadi Saa 11.00 Jioni)*

*(Saa 11.00 Jioni Bunge Lilirudia)*

**SPIKA:** Waheshimiwa tukae.

Katibu.

**NDG. MICHAEL CHIKOKOTO, *ndc* – KATIBU MEZANI:**

**HOJA ZA SERIKALI**

**Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025**

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na majadiliano. Tutaanza na Mheshimiwa Boniphace Mwita Getere.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia Wizara ya Ardhi. Wizara hii kwa sasa ina Waziri mpya na tunaona anafanya kazi nzuri sana, namshukuru sana na nampongeza sana. Nampongeza Naibu Waziri, nampongeza Katibu Mkuu Wizara, Kamishna na Watendaji wote wa Wizara ya Ardhi, wanafanya kazi nzuri tunaona wanahangaika huku na kule. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, leo nataka nizungumze mambo kama matatu hivi. Jambo la kwanza ni migogoro ya ardhi. Nashauri Wizara pale ambapo kuna mgogoro wa ardhi na Wizara imepeleka vifaa vyake vyote na watendaji wake wote wamesuluhisha huo mgogoro, Wizara itoe vibali au barua kwa Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya kuonyesha kwamba sisi tumefika kwenye mgogoro fulani tumefanya usuluhishi na sasa kwa Wizara ya Ardhi tumemaliza, kwa sababu tumekuwa na mambo mawili ambayo yanajitenganisha.

Mheshimiwa Spika, kuna wakati fulani kuna mgogoro wa mpaka, wanasema mpaka uko sawa, lakini ndani kuna watu wanakaa wanataka kuhama kwenye eneo hilo kwa mujibu wa Sheria za Kijiji, lakini hawahami. Wakuu wa Wilaya na Wakuu wa Mikoa wanakuwa bado wana shida na jambo hilo. Kwa hiyo, kunapotokea migogoro ya mipaka, nimwombe Waziri mhusika, kama mpaka huo wenyewe wameusuluhisha watoe barua ya kuonyesha kwamba huo mpaka umesuluhishwa na sasa kama mtu amebaki kuhama na kama siyo wao wanaomhamisha ni Wizara ya TAMISEMI basi viongozi wanaohusika waende TAMISEMI kuwaambia wahamishe mtu anayehusika.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, niombe kwenye jambo hilo kwamba kwenye eneo langu limetokea Mekomariro na tumezungumza na nyie nawashukuru sana. Kwenye kliniki ya ardhi mnafanya vizuri, mimi nawapongeza kwa hilo, mtatekeleza yale ambayo tunawashauri ili twende vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo nilikuwa nataka nilizungumze hapa ni upimaji wa matumizi bora ya ardhi. Sasa matumizi bora ya ardhi mnaenda kupima kwenye vijiji, mnapima vizuri. Bahati mbaya kwenye Jimbo la Bunda nawashukuru sana wamepima karibu vijiji vyote, lakini kuna Vijiji vya Hunyari, Kihumbu, Mariwanda na Sarakwa. Watu wao wa Mashirika sijui *NGOs* wanakuja wanalazimisha wale watu waweke *WMA*. Sasa nashindwa kuelewa, wananchi ndiyo wenye ardhi wanaendaje kuwalazimisha waweke *WMA* kwenye maeneo ambayo wao hawataki?

Mheshimiwa Spika, bahati nzuri anayehusika kwenye matumizi bora ya ardhi Mkurugenzi wake ameniambia hili jambo atalikataza na ameandika barua kwa Mkuu wa Wilaya kuzuia kulazimisha wananchi kupanga matumizi bora ya ardhi kwa maana ya *WMA*. Kwa hiyo, nawashukuru sana hilo nalo limetoka, lakini niombe wawaelimishe wananchi. Wanapokwenda kupima matumizi bora ya ardhi wanapanga makaburi, maeneo ya malisho na maeneo mengine. Maeneo hayo wanakuta yamekaliwa na wananchi na wanashauri kwamba *either* mtu anayepangwa kwenye eneo la makuburi ili ahame anatakiwa apewe fidia au apewe eneo lingine la kuishi.

Mheshimiwa Spika, je kama fidia haipo? Je, kwenye maeneo ya kuishi kama hayapo? Je, kama hakuna makubaliano na kijiji anahamishwaje? Kwa hiyo waelimishe wanakijiji katika matumizi bora ya ardhi wawe wanajua tunahamaje? Maana yake unakwenda kupima halafu wale wa Serikali za vijiji wanawaambia sasa nyie tunaweka vibao tokeni hapa. Anatoka anaenda wapi? Anaendaje kwenye eneo gani kuishi na alikuwa anaishi maeneo hayo?

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo tuwaelimishe wananchi na sheria inasema nini kwa ambaye amekuja hapa? Watueleze inasema nini kwa mtu aliyehamishwa kutoka eneo alilokuwa anakaa kwa matumizi bora ya ardhi ahamie sehemu nyingine kwa sababu hapa tumeweka makaburi, mashamba au jambo lingine? Kwa hiyo, tunaomba tupate hiyo sheria ili wananchi wawe wanaelimishwa wanajue pa kwenda.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo liko hapa naliona ni suala la malisho. Kuna vijiji sasa hivi huwezi kutenga eneo la malisho kama hawajatenga. Kama wametenga ni sawa ila kama hawajatenga maana yake ni kwamba kila mtu anaishi kutokana na anavyokaa kwenye maeneo yake. Wakienda kulazimisha watu kutenga maeneo ya malisho ambayo tayari kila mtu ana-*block* yake ndiyo inatusababishia tunazalisha mgogoro mwingine ambao haupo. Kwa hiyo twende pale tukubaliane kama watu wametengeneza *block,* ukienda kwenye maeneo kama ya Hanang, kwenye maeneo mengine kama kule kijijini kwangu kunaitwa Sarakwa na maeneo mengine kila mtu ana-*block* yake ya kuchungia.

Mheshimiwa Spika, sasa ukianza kumwambia toka tuchunge wote na eneo lenyewe halitoshi, wanachunga akina nani? Kwa hiyo, tukubaliane na matumizi bora ya ardhi pale wananchi wanapokuwa wanapanga ili tusiishi kwa kukariri kwamba lazima kuwe na maeneo ya malisho, lazima kuwe na maeneo fulani hapana, tuangalie hali halisi. Kama mtu ana-*block* yake ni *block* yake aendelee nayo kuishi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika hii Wizara, huwa najiuliza mambo mengi sana. Huwa nasema hivi kila siku kuna mgogoro Dar es Salaam, kila siku kuna migogoro ya Ardhi Dodoma na kila siku kuna mgogoro sijui Mbeya. Kwa nini tusitengeneze mikoa ya Majiji kama matano tukamaliza migogoro ya ardhi? Tukasema hii ni *pilot area* kwamba leo Dar es Salaam ni labda 90% tumefaulu na Dodoma 90% tumefaulu. Kwa nini miaka nenda rudi maeneo fulani hayaishi mgogoro? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, leo ukiitisha mgogoro wa ardhi hapa Dodoma ni balaa. Ukienda hata Bunda ukiitisha ni balaa? Kwa nini tusimalize migogoro ya ardhi? Kuna shida gani? Kuna shida gani ambayo hatumalizi wakati tuna vifaa vyote ikiwemo *GPS* na kila kitu? Kwa hiyo, niombe tujue hili jambo tukilitengeneza litakuwa zuri zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tuna vijiji vingapi vimepimwa, tuviwahi basi. Leo tunazungumza *squatter* ndani ya Dodoma, leo

tunazungumza *squatter* ndani ya Bunda, kila maeneo unaweza kukuta yako hivyohivyo. Tuwahi maeneo ambayo hayajapimwa yapimwe ili tuweze kuleta vipimo vya kutosha ili maeneo haya yawe safi tupunguze migogoro ya ardhi. Migogoro ya ardhi ni shida.

Mheshimiwa Spika, jambo la mwisho ambalo nataka kuchangia, huwa najiuliza, kuweka gharama kubwa ya ardhi mtu kununua kiwanja, mtu kupimiwa kiwanja hivi ni ubora? Hivi ni ufanisi? Hivi hakuna mikopo? Hivi si tuanze kwenye mikopo ya kukopesha watu basi? Mpime eneo, mkopeshe mwambie alipe pole pole kuna shida gani? Kuna shida gani mtu atoe hela nyingi kupima na hana? Kwa nini tusikopeshe watu sasa? Wewe bwana una eneo gani? Hili hapa, *ok* tunakupa eneo tunapima tunakwambia bwana lipa polepole utamaliza. Hivi kukaa na maeneo mengi ambayo hayajapimwa ni kupata hela? Hivi kuna nini? Hivi kwa nini tusitumie akili zetu za kawaida tukopeshe watu ardhi kama mtu anapima apime halafu alipe pole pole? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana, ya kwangu yalikuwa hayo. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Agnesta Lambert Kaiza atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Festo John Dugange, Mheshimiwa Geophrey Mizengo Pinda ajiandae.

**MHE. AGNESTA L. KAIZA:** Mheshimiwa Spika, nikushukuru kwa kunipa nafasi. Kabla ya kuchangia naomba nitumie nafasi hii kukupongeza wewe kwa kazi nzuri ambayo unaifanya hususan ya kutuwakilisha huko duniani. Hakika Mungu akubariki na sisi tunaendelea kukuombea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kabla ya kuendelea na mchango wangu naomba kwanza nianze na pongezi. Pongezi zangu za kwanza ni kwa Mheshimiwa Rais, Mama yetu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi nzuri sana ambayo anaifanya hususan katika eneo hili la ardhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tumekuwa tukisikiliza hotuba nyingi za Mheshimiwa Rais na mara nyingi tumeona na tumesikia jinsi ambavyo amekuwa akielekeza Wizara pamoja na wateule wake kuhakikisha wanasimamia haki kuhusiana na suala zima la ardhi ili kila mwananchi au kila Mtanzania apewe haki yake ya msingi pale linapokuja suala zima la ardhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niende pia kumpongeza Waziri mpya Mheshimiwa Jerry Silaa kwa kazi nzuri, kubwa na ngumu anayoifanya. Kuthibitisha kwamba Waziri huyu anafanya kazi nzuri, nakumbuka mnamo tarehe 13, Machi, Mheshimiwa Rais akiwa anawaapisha Waheshimiwa ma-*DC* na baadhi ya Wakuu wa Mikoa alisema wazi wazi jinsi ambavyo anafurahishwa na utendaji kazi wa hii Wizara ya Ardhi. Tutakuwa ni watu ambao basi tunajidanganya ikiwa Mheshimiwa Rais, atatambua kazi kubwa na nzuri ya Waziri pamoja na timu yake anayoifanya halafu sisi tukasimama hapa tukasema Waziri hufanyi kazi. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri Jerry nakupongeza, lakini niseme kwamba unazo changamoto nyingi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nasema hivyo kwa sababu unapoona hadi Rais wa nchi, anakupongeza ujue hiyo ni habari njema, lakini pia ni mtego. Ikiwa hutaenda kutimiza majukumu yako ipasavyo, basi ujue kuna siku ambayo atakwambia kwamba anachukizwa na hapendezwi na kazi yako njema. Sisi tunamwombea Waziri na tunamwamini. Binafsi namfahamu tangu kutokea huko, mimi natoka Jimbo la Segerea, yeye yuko Ukonga, utendaji wake wa kazi naufahamu vizuri na sina shaka naye.

Mheshimiwa Spika, kabla sijaenda moja kwa moja katika mchango nina ombi kwa Mheshimiwa Waziri. Nakumbuka niliwahi kwenda kwenye kiti chake hapo na nilimweleza jinsi ambavyo mimi natoka Jimbo la Segerea kwa maana naishi Segerea, kuna wakazi ambao wanaishi Segerea ila asili yao ni ya kutoka kule Jimbo la Chalinze kwa maana ya eneo la Mbara. Sasa nilimshirikisha Mheshimiwa Waziri, jinsi ambavyo wananchi hawa wana changamoto kubwa sana au wana mgogoro mkubwa kati ya wafugaji pamoja na wakulima. Nilimweleza Mheshimiwa Waziri kwamba hata wao kuhamia Segerea na wengine nafikiri wapo

Jimboni kwa kaka yangu Mheshimiwa Ridhiwani na maeneo mengine; wengi walihamia kule baada ya kuwa wamevutana sana kwa maana ya wafugaji na wakulima.

Mheshimiwa Spika, sasa walipoanza mambo ya kuvutana, kugombana na hata kutaka kutishana maisha, basi wengine wakaamua kujiepusha kutafuta maeneo mengine ili angalau maisha mengine yaendelee na ndiyo hivyo baadhi wakawa wamekuja katika Jimbo la Segerea. Nilimwambia Mheshimiwa Waziri na nilimpa vithibitisho kwamba ni zaidi ya wananchi 200 ambao wana huo mgogoro katika eneo la Mbara. Sasa nimwombe sana Mheshimiwa Jerry, tumeshuhudia jinsi ambavyo ametatua migogoro mikubwa kabisa kuzidi huo mgogoro wa Mbara. Tumemwona Mkoa wa Dar es Salaam, Mkoa wa Arusha na kule Ilemela ameweza kutatua migogoro mikubwa sana. Nimwombe Mheshimiwa Waziri kwa kuwa nilishamshirikisha jambo hili na akaniahidi kwamba atafika sehemu ile asikilize na baadaye atende haki.

Mheshimiwa Spika, atakapokuja hapa Mheshimiwa Waziri kwa nia njema kabisa na kwa sababu Watanzania hawa na wakazi hawa wa Segerea wanamsikiliza. Hivi ninavyochangia wananisikiliza na wanasubiri kusikia Waziri atajibu nini? Nimwombe Mheshimiwa Waziri, aniambie ni lini sasa ambapo ataweza kufika eneo hilo la Mbara ili angalau basi ijulikane ni wafugaji au ni hawa wakulima ambao wana haki ya kumiliki ile ardhi? Mheshimiwa Waziri, nitashukuru ikiwa atanipa majibu hayo na Wana-Segerea kwa kuwa wanakufuatilia, basi hakika watazidi kumwombea.

Mheshimiwa Spika, sasa niende katika machache ambayo nimejipanga kuchangia. Jambo la kwanza kabisa Mheshimiwa Jerry, wakati anawasilisha Hotuba ya Bajeti yako hapa nilimsikiliza kwa umakini mkubwa sana. Pia, nilisikiliza vipaumbele vyake na namna ambavyo amejipanga kwenda kutatua changamoto mbalimbali zinazohusu migogoro ya ardhi. Nimpongeze kwa maana vipaumbele vyake ni vizuri, lakini pia maelezo yake yamejitosheleza.

Mheshimiwa Spika, niseme pia kwa Mheshimiwa Jerry, Wizara hii kama ambavyo mzungumzaji ambaye amemaliza amesema ni zigo kubwa sana, lakini pia wewe ndiyo kwanza umeingia. Katika suala hili la ardhi Mheshimiwa Waziri Jerry, zipo changamoto nyingi au kuna migogoro ambayo kimsingi siyo migogoro ambayo tunapaswa kuisikia kila iitwapo leo.

Mheshimiwa Spika, nikienda katika suala zima la upimaji na umilikishwaji wa ardhi yapo mapungufu mengi sana. Pamoja na kazi nzuri inayofanywa na hii Wizara ya Ardhi, lakini yapo mapungufu makubwa sana katika upimaji na umilikishwaji wa ardhi. Nitataja baadhi kwa sababu ya muda.

Mheshimiwa Spika, kwanza kuna suala la Wizara kwenda kupima maeneo na kutoa viwanja katika maeneo ambayo hayana sifa ya kuwa makazi. Mheshimiwa Jerry ninachokwambia hapa, naongea kwa niaba ya Watanzania lakini pia naongea kwa niaba yangu mimi mwenyewe binafsi kwa sababu jambo hili limenitokea hapa hapa Dodoma.

Mheshimiwa Spika, mnamo mwaka 2019 nilinunua kiwanja kutokea Jiji. Baada ya kununua kiwanja kile na kukabidhiwa *document* zote niliweza kujenga nyumba pale kubwa tu yenye vyumba vitatu na nikajibana, nikaezeka kwa bati ya m-*south*. Baada ya kama miezi sita nikiwa Dar es Salaam, niliambiwa kwamba ile nyumba imebomolewa. Ni kwa nini imebomolewa? Nikarudi hapa Dodoma kufuatilia inakuwaje? Nimemilikishwa kihalali, nimejenga nyumba imekaa zaidi ya miezi sita halafu wanakuja wanabomoa kama hakuna chochote ambacho kilikuwa pale? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nilivyofika hapa nilienda moja kwa moja Jiji. Nilipofika nilichoambiwa ni ile kwamba makosa yamefanyika ni kwamba mifumo haikusomana kwamba kwa hiyo, alipewa mtu mwingine. Nimenunua mimi eneo, nimepewa *document* zote amekuja mwingine amenunua halafu huyu aliyeuziwa ndiyo anakuja kubomoa nyumba yangu. Kwa hiyo, nilichoambiwa kwamba sasa tutakupatia kiwanja kingine. Unajua wakati mwingine kama hujajua hizi Sheria za Ardhi unaweza

ukanyanyasika na *imagine* mimi napata majanga kama hayo? Mtanzania wa kawaida wa kule kijijini kabisa ambaye hajui lolote unaweza uka-*imagine*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, *to cut the story short,* nikaahidiwa kwamba ni makosa yalitokea, mifumo haikusomana. Sasa sijui haikusomana namna gani? Wizara inajua na wataalamu wanajua, nikaambiwa sasa nitapewa kiwanja kingine. Kile kiwanja kilikuwa kina *square meter* 1,870, nikaambiwa napewa kiwanja kingine. Mheshimiwa Waziri, nimekaa muda mrefu nafuatilia baadaye nikaambiwa njoo usaini hati, nikasaini *document* zote za hati bila kuoneshwa kiwanja. Nilihitaji nione kiwanja kabla ya kusaini ili niridhike kwamba je, kiwanja ninachopewa kinaendana na kile kitu ambacho nimepoteza?

Mheshimiwa Spika, sikuoneshwa kiwanja, baadaye nimekabidhiwa hati *the same day* ndiyo napelekwa kuoneshwa kiwanja. Ni maajabu, ni aibu hata kusema, lakini Mheshimiwa Jerry kile kiwanja kwamba pale kwanza hapapaswi kuwepo na kiwanja ni kwenye korongo ni kwenye mawe halafu kiwanja chenyewe *square meter* 450. Mimi nimevunjiwa nyumba, nimechukua kiwanja kikubwa halafu napewa kile kiwanja ambacho siyo kiwanja na siyo sehemu ya kukaa kiwanja ila nimeshikishwa hati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, *so* baada ya pale nilirudi jijini Mheshimiwa Jerry nikaambiwa nisubiri natafutiwa kiwanja kinachoendana na kiwanja cha kwangu. Kipindi kile alikuwepo Mkurugenzi mwingine ambaye ni Mafuru kama nakumbuka vizuri akaniambia nitapewa kiwanja kingine. Wakati yupo kwenye *process* zile akaondoka kabla hata sijapewa kile kiwanja na mpaka naongea na wewe sijapewa kiwanja ile hati ninayo siyo kiwanja ni korongo, ni mawe. Ukifika pale mwenyewe hata ukipewa bure kwamba hapa ujenge choo huwezi kukichukua kabisa.

Mheshimiwa Spika, sasa mpaka naongea hapa bado nilikuwa sijafika Ofisi ya Mkurugenzi mpya ndiyo leo sasa nakuja kuchangia. Natambua kwamba Mkurugenzi aliyepo anasikiliza watu na najua nikienda atanisikiliza. Nimeona niliseme hapa kwa

sababu yaliyonikuta najua yamewakumba watu wengine wengi ambao hawana hata sehemu ya kwenda wala kusikilizwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hilo lilikuwa ni pungufu moja wapo. Pungufu la pili na la mwisho kwa sababu kwenye mapungufu ni mengi na muda hautoshi. Pungufu la pili ni Wizara kwenda kupima maeneo ya wananchi bila kuwashirikisha. Mtu ana eneo lake na hapa Dodoma ndiyo *business* ya hali ya juu na mimi hilo limenikuta. Kwa sababu tumehamasishwa sana kuwekeza Dodoma si ndiyo? Kwa hiyo, watu tunawekeza Dodoma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nilinunua ardhi kule Msalato nina *document* zote. Nimekuja kushangaa naenda pale nakuta kote kumepangwa mawe halafu mawe yamepangwa ya kupimwa viwanja ni vidogo *square meter* 340, 350 na hatujui nani alipima. Ukiuliza unaambiwa kampuni fulani. Ukienda kwenye Kampuni unaambiwa hii Kampuni iliacha kazi imekuja nyingine, nyingine iko wapi? Haijulikani, haijulikani *and then we just give up,* hayo ni mapungufu.

Mheshimiwa Spika, jambo la mwisho, nimemwona Mheshimiwa Jerry *the way* anavyoshirikisha watu anapokuwa anakwenda kutatua migogoro. Amekuwa akishirikisha kuanzia viongozi wa Kiserikali na wataalam. Pamoja na kumpongeza Mheshimiwa Jerry, naomba nimwibie siri moja, anapokuwa anakwenda kutatua hii migogoro, sehemu nyingi viongozi wa Kiserikali ni sehemu ya hii migogoro. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, unakuta ma-*DC*, wakuu wa mikoa, nimesema baadhi, si wote, ni sehemu ya migogoro ambayo unakwenda kuitatua. Sasa, kama ni sehemu ya migogoro unayokwenda kuitatua unapokuwa nao tayari wanakuwa wameshakueleza wanayojua wao kwa sababu ya kuwa-*favour* wao, unapokwenda kwa wananchi ni ngumu sana kujua ukweli na kutambua ni nani hasa ambaye ni mhusika anapaswa kupewa haki kama hii. Hatimaye unakuta, kwa mfano maeneo ambayo kuna wawekezaji kama vile sheli na kadhalika, *always* viongozi wa

kiserikali wana-*base* upande wa huyu ambaye anaonekana ameshiba sana kuliko kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, ninafahamu na ninatambua kwamba zipo kanuni na taratibu za kutatua hii migogoro ya ardhi. Kwa hiyo ushauri wangu, hizo hatua pamoja na hawa viongozi wa kiserikali ambao tunawaheshimu na kutambua mchango wao, lakini kwa sababu maeneo mengi yamekuwa ni sehemu ya migogoro, basi utumie ule utaratibu na kanuni za utatuzi wa migogoro ya ardhi.

Mheshimiwa Spika, ninayasema haya kwa sababu, unakuta kuna mwekezaji amekuja kuwekeza kwenye eneo kubwa kabisa. Anachukua eneo la wananchi kwa hela ndogo au bila hata na fedha kabisa. Kiongozi wa mtaa au kijiji anapindisha pindisha mambo, hili eneo la Serikali, sijui lilikuwa eneo la wazi, ghafla unakuta amekuja mwekezaji. Anapokuja *DC* au mkuu wa mkoa ambao wamekaa kisiasa wanatoa matamko ya kuvunja moyo, na wote tunatambua. Naomba Mheshimiwa Jerry atambue kuwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan anategemea wapigakura wengi ambao ni wanyonge na wanaolia kwa ajili ya ardhi. Hatutaki mwaka 2025 Mama Samia anakwenda kuomba kura, wameshika mabango wakiwa wanadai ardhi.

Mheshimiwa Spika, ninamwomba sana asimamie kanuni. Wakuu wa mikoa, ma-*DC* awasikilize kama watawala wa eneo hilo, lakini wasiwe ni *final say* ya kumweleza ni nani yupo sahihi, nani ambaye hayupo sahihi. Aende chini kabisa kule awasikilize wananchi na hatimaye naomba akatende haki. Tumemwona akiwa anatenda haki, amesimama katika maeneo magumu ambako changamoto na migogoro ilishindikana kwa miaka mingi, lakini amesimama na ametatua. Ndiyo maana Mheshimiwa Rais anasema kwamba anafurahishwa na utendajikazi wake na Wizara yake. Kwa hiyo ninamwomba asimwangushe na asituangushe Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimalize kwa kusema kwamba nipo chini ya miguu yake, Wana-Segerea wanamsikiliza na wananisikiliza mimi pia, atuambie ni lini atakwenda pale Mbara kutatua ule mgogoro? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nikushukuru sana kwa kunipa nafasi. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana.

## MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Spika, ninachukua nafasi hii kuungana na Watanzania wenzangu wote kumshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kutujalia baraka zake katika nyanja mbalimbali za ustawi wa kijamii, kisiasa, kiuchumi, kidiplomasia na mshikamano wakati wote; kwa kweli ametuepusha na majanga mengi sana.

Mheshimiwa Spika, pia ninachukua nafasi hii kuungana na wananchi wa Jimbo langu la Mbulu Mjini kumpongeza sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali nzima ya Awamu ya Sita, kwa jinsi wanavyoiongoza na kutekeleza Ilani ya Chama Cha Mapinduzi ya mwaka 2020 - 2025. Hongereni sana na Mwenyezi Mungu awajaalie mshikamano wenu udumu.

Mheshimiwa Spika, ninampongeza sana Mheshimiwa Jerry William Silaa, Waziri wa Wizara hii muhimu sana kwa maendeleo ya Sekta ya Ardhi, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wote wa Wizara kwa jinsi walivyotekeleza majukumu yao ipasavyo kupitia taarifa ya Wizara iliyowasilishwa mbele ya Bunge letu hili, hongereni sana na Mwenyezi Mungu awabariki. Aidha, ninachukua nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati yetu ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi pamoja na wajumbe wake wote kupitia taarifa yao ambayo imefafanua vyema mafanikio na changamoto.

Mheshimiwa Spika, sasa naomba kutoa mchango wangu kupitia mapendekezo ya bajeti ya Wizara hii muhimu sana kwa maendeleo Sekta ya Ardhi. Kwanza tunaiomba Serikali iangalie upya utaratibu wa Mradi wa Kupanga, Kupima na Kumilikisha Ardhi (KKK). Kwa kweli huu ni mradi mzuri sana kwa ajili ya maendeleo ya Sekta ya Ardhi nchini.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo mradi huu unakabiliwa na changamoto nyingi sana zikiwemo ukosefu wa wataalamu wa ardhi, vitendea kazi na mkanganyiko wa mfumo wa ukusanyaji wa malipo ya viwanja katika halmashauri zote nchini ambazo tayari zimepokea fedha za mradi huu, hali inayosababisha fedha nyingi kutokusanywa kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo itakuwa vyema wakati wa Bunge la mwezi Septemba kuziita halmashauri zote zilizopokea fedha za K.K.K. mbele ya Kamati ya Ardhi na Kamati ya TAMISEMI ili kufanya tathmini ya maendeleo ya mradi pamoja na marejesho.

Mheshimiwa Spika, tunaiomba Serikali ijitahidi sana kutoa fedha za bajeti ya maendeleo ya Wizara hii muhimu sana katika mwaka huu wa bajeti. Pia tunaiomba Serikali iangalie uwezekano wa kuajiri wataalam wa ardhi katika halmashauri zote nchini ili kufanikisha malengo yaliyokusudiwa katika kila mwaka wa bajeti kwa kuwa tunashindwa kufanikisha malengo ya K.K.K.

Mheshimiwa Spika, Wizara iangalie utaratibu wa kuweka mfumo wa *sms* ili kumkumbusha mlipakodi ya pango la ardhi kila inapofika muda wa malipo, ujumbe ambao utakuwa na *control number* ili kurahisisha malipo badala ya kutafuta namba ya malipo hadi ofisini.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. OMARI M. KIGUA:** Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na watumishi wote wa Wizara kwa kazi nzuri wanayoifanya.

Mheshimiwa Spika, nimpongeze sana Mheshimiwa Rais kwa kutatua mgogoro wa mpaka kati ya Kilindi. Hoja yangu au rai yangu ni kwamba Serikali iweke alama za mpaka haraka iwezekanavyo ili wananchi wafanye shughuli za kimaendeleo. Aidha, bado utoaji wa hati unachukua muda mrefu sana, hivyo nimwombe Mheshimiwa Waziri jambo hili litafutiwe ufumbuzi.

Mheshimiwa Spika, Wana-Kilindi wamefarijika sana kupata mradi wa matumizi bora kwa vijiji 83.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE:** Mheshimiwa Spika, naomba nichukue nafasi hii kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kunijaalia afya.

Mheshimiwa Spika, naomba nimpongeze Mheshimiwa Rais kwa kazi nzuri anayoifanya katika kuwatumikia Watanzania. Pia naomba niungane na wenzangu kumpongeza Mheshimiwa Waziri na wasaidizi wake wote.

Mheshimiwa Spika, naomba niunge mkono hoja. Baada ya kuunga mkono hoja naomba nitoe mchango wangu katika baadhi ya maeneo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza ni kuhusu kubadilishwa mpaka kati ya Halmashauri ya Wilaya ya Kalambo na Halmashauri ya Manispaa ya Sumbawanga. Mpaka huu umebadilishwa kinyemela na kwa bahati mbaya bila kuwashirikisha wananchi wa pande mbili wanaofahamu vizuri mpaka pamoja na historia ya mpaka huu.

Mheshimiwa Spika, jambo la kushangaza zaidi ni pale ambapo serikali ya mkoa imefikia uamuzi huo bila kuwashirikisha Waheshimiwa Wabunge husika. Jambo hili halileti afya hata kidogo na huku ni kukuza mgogoro bila sababu kwani umekuzwa na uongozi wa Manispaa ya Sumbawanga kwa matazamio ya kuja kujenga uwanja mpya katika eneo la Kijiji cha Kisumba ambalo mimi binafsi nilikuwepo likiwekwa jiwe na msingi na aliyekuwa Makamu wa Rais, Mheshimiwa Dkt. Gharib Bilal. Ninaiomba Wizara iingilie kati baada ya uongozi wa mkoa kushindwa kutenda haki.

Mheshimiwa Spika, kuhusu upimaji na upangaji wa vijiji na miji midogo inayokua kwa kasi kubwa kuliko upimaji wa viwanja,

haina tija kwa dunia ya leo kuendelea kujenga bila kupima *(squatters)* hali ambayo inapunguza hata thamani ya majengo.

Mheshimiwa Spika, Mji Mdogo wa Matai ambao ni Makao Makuu ya Wilaya ya Kalambo kwa miaka ya nyuma uliwahi kusifiwa kuwa kati ya maeneo yaliyopangwa na kupangika vizuri, lakini kutokana na uchache wa rasilimali fedha kazi ya upimaji imepungua sana. Tuombe; kati ya halmashauri zinazotakiwa kusaidiwa kifedha basi na halmashauri yetu iwe miongoni kwani kasi ya kuendelea kujenga ni kubwa. Kasi hiyo itaongezeka zaidi pale barabara yenye kiwango cha lami kutoka Matai hadi *Kasesya Border* itakapokamilika.

Mheshimiwa Spika, kwa hayo mawili, naomba kuwasilisha.

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU:** Mheshimiwa Spika, ninaomba mchango wangu huu kwa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi uchukuliwe kwa uzito. Kwanza tunawapongeza kwa kazi kubwa inayofanywa na Wizara ya Ardhi nchini, bila kumsahau Rais wetu Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan.

Mheshimiwa Spika, naomba mchango wangu upokelewe kama ifutavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza kuongeza kasi ya upimaji na kuongeza mapato kutoka katika ardhi ni muhimu sana. Sasa tuongeze wigo wa walipakodi na kupunguza viwango kwa *square metre* kwa walipakodi ya ardhi, yaani *land rent* ili kodi iweze kulipika kirahisi na watu wengi na kwa wingi kuliko kuwa na madai makubwa yasiyolipika.

Mheshimiwa Spika, pili, viwango vya kodi kwa taasisi kama shule, itumike *flat rate* kutokana na maeneo ya majiji, manispaa au vijiji; kwa kuwa vipo viwango vya ardhi inayohitajika kwa ajili ya ujenzi wa shule. Kumekuwa na shida ya ulipaji wa hizi kodi za ardhi kwa taasisi kama shule kutokana na ukubwa wake unaohitajika, na umuhimu wake kwa wananchi. Huwezi kutumia *market price* ilhali hii ni *service,* lakini pia ina maeneo ambayo viwanja vya

michezo havitoshi na hivyo, inakuwa ni vigumu kwa wawekezaji hawa wa shule na taasisi nyingine za mtindo huo.

Mheshimiwa Spika, tatu, kuhusu viwango vya ulipaji wa kodi ya ardhi kwenye vijiji vinavyopandishwa hadhi kama miji wakati bado ni vijiji, tunaomba liangaliwe upya na sehemu hizo zichukuliwe kama vijiji kwa uhalisia wake. Kwa kuwa tuna vijiji ambavyo vipo mijini, hata sekta nyingine kama nishati, wameliweka na kutengeneza *peri-urban plan*.

Mheshimiwa Spika nne, viwango vya kodi za nyumba za *NHC* za Iringa Mjini vimekuwa ni mgogoro mkubwa. Tunaomba kodi iendane na kiwango cha bei ya soko kwa kuzingatia ubora wa nyumba hizo. Pia tunaomba ukarabati ufanyike kwenye majengo mengi yaliyochakaa ndani ya Manispaa ya Iringa. Tano, tunawaomba *NHC* waje wawekeze katika mji wetu katika maeneo ya utalii, kwenye makazi ya watu na hoteli.

**MHE. PROF. PATRICK A. NDAKIDEMI:** Mheshimiwa Spika, kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi Mheshimiwa Jerry Silaa na Naibu Waziri Mheshimiwa Geophrey Pinda, Katibu Mkuu Ndugu Anthony Damian Sanga pamoja na wataalamu wa Wizara kwa kazi nzuri wanazozifanya.

Mheshimiwa Spika, mchango wangu utahusu hatimiliki za mashamba ya ushirika Mkoani Kilimanjaro na mikoa mingine ambayo yalirithiwa baada ya kutaifishwa mwaka wa 1967 kutoka kwa wamiliki waliokuwa wana hatimiliki za miaka 33, 66 au 99.

Mheshimiwa Spika, mashamba niliyoyataja hapo juu yalikuwa na hatimiliki. Kifungu cha 32 cha Sheria ya Ardhi kinasema kuwa mtu anaweza kupewa hati bila kupewa chaguo la kupewa tena. Hii ina maana unapewa hati kwa muda maalum na muda huo ukiisha basi ardhi hiyo inakuwa si mali yako tena. Inapokuwa si mali yako tena ardhi hurudi mikononi mwa mamlaka za ardhi ambapo Waziri mwenye dhamana na Kamishna Mkuu wa Ardhi wanaweza kumpatia mtu mwingine ardhi hiyo akiwa kama mmiliki mpya.

Mheshimiwa Spika, ninaishauri Serikali ifanye utafiti wa kina ili kubainisha uhai wa hatimiliki za mashamba ya ushirika mkoani Kilimanjaro (penye mashamba mengi ya ushirika na uhaba mkubwa wa ardhi) na mikoa mingine. Maeneo haya yana migogoro kutokana na uwezo mdogo wa kuzilinda rasilimali ardhi hizi.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa tumeshuhudia matumizi mabaya sana yanayofanywa na wawekezaji katika mashamba hayo, na pia baadhi ya viongozi wa mashamba haya wameshindwa kuyaendeleza kabisa kwenye baadhi ya miradi ya uwekezaji mashambani, hata zile *Corporate Social Responsibility* hupatikana kwa shida. Ukweli ni kwamba wananchi hawaoni kabisa manufaa ya kiuchumi kutoka katika ardhi hizi za umma.

Mheshimiwa Spika, ninaishauri Serikali kuwa sasa ni wakati wa kupitia hati za umiliki wa mashamba haya na kubaini uhai wa hatimiliki za mashamba yote. Kwa zile zilizomaliza muda, ni wakati muafaka wa kubadilisha umiliki wa mashamba hayo na kuwapatia wazawa wa maeneo husika (hasa vijana wasio na ardhi) ili wasaidiwe na kuwa wawekezaji na kuondokana na mawazo ya kuwapatia ardhi yetu wawekezaji wa nje ya Tanzania. Kwa wale wanaotumia ardhi vibaya, mamlaka ya Rais ifute umiliki kisheria na kuwamilikisha vijana wa hayo maeneo ili washiriki kikamilifu kwenye miradi ya kitaifa ya uzalishaji kama *BBT*.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo yangu hapo juu, naunga mkono hoja.

**MHE. SANTIEL E. KIRUMBA:** Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa jinsi ambavyo amewekeza kwenye Sekta ya Ardhi.

Mheshimiwa Spika, kukosekana kwa Mfuko wa Fidia ambao ni takwa la kisheria kunasababisha fidia kutokulipwa kwa wakati na kuwa kero kubwa kwa waguswa (wananchi ambao ardhi zao zinatwaliwa kwa ajili ya miradi). Pia kwa sababu hakuna Mfuko wa Fidia, kumekosekana chombo ambacho kinaratibu fidia bila

upendeleo. Kwa sasa wanaotaka ardhi ndio wanaoamua fidia kiasi gani ilipwe na ilipwe wakati gani. Hiyo si sawa na inakiuka sheria ambayo inataka fidia ilipwe kupitia Mfuko wa Fidia kwa ukamilifu, kwa hali na kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, kuna suala pia la uzembe wa kukusanya maduhuli ya Serikali, hasa kodi ya pango la ardhi *(land rent)*. Hakuna juhudi za kudai, wamiliki wa viwanja wanasubiri hadi kipindi cha bajeti kikaribie ndipo waanze kusumbua wananchi kwa matangazo ya kutishia kupeleka watu mahakamani au kufuta umiliki wa viwanja. Kwenye hotuba haioneshi Wizara kuweka mkakati wowote juu ya namna ya kuongeza ukusanyaji wa maduhuli (mapato) yake.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la utatuzi wa migogoro ya ardhi linahitaji mkakati mahsusi zaidi ya kufanya ziara za viongozi maarufu kwa jina la Kliniki za Ardhi. Hizo kliniki kweli zinahamasisha watu kupeleka malalamiko, lakini mazingira ya usuluhishi hayana uhakika kama migogoro itakuwa imetatuliwa na maamuzi yataheshimika. Kuna mazoea ya wananchi kurudia kupeleka malalamiko kila uongozi mpya unapoanza. Waziri akibadilika walioshindwa watalalamika upya na huenda maamuzi yakabadilika na kuchochea tena migogoro.

**MHE. PRISCUS J. TARIMO:** Mheshimiwa Spika, mchango wangu ni kuhusu Benki ya Nyumba ya Taifa. Watanzania asilimia kubwa wanajenga nyumba kwa fedha taslimu, hali hii inasababisha rushwa makazini, kwenye biashara na jamii kwa ujumla. Nyumba ni hitaji muhimu na la lazima, lakini ni ulinzi pia kwa familia. Ni vyema kuhakikisha kuwepo kwa benki ya nyumba au mfumo wa kibenki wa kutatua suala hili. Hapa ushauri wangu si kwa kuwapa fedha bali ni kwa kuwakopesha wenye viwanja vifaa vya ujenzi; kwa kutumia nyumba na kiwanja hicho kama dhamana na iwe ya muda mrefu kuanzia miaka 10 hadi 30 kwa wananchi. Hii itasaidia kuwapa amani Watanzania, lakini pia itasaidia kuongeza urari mifukoni mwa wananchi na kuchochea ukuaji wa uchumi wa nchi.

**MHE. COSATO D. CHUMI:** Mheshimiwa Spika, kwanza napenda kuwapongeza kwa kazi nzuri sana na zaidi kwa ushirikishwaji. Kama mwakilishi wa wananchi napata ushirikiano mkubwa kuanzia ngazi ya watu wenu pale halmashauri hadi kwa Kamishna Msaidizi pale mkoani. Kwa kweli sina malalamiko, nawapongeza pia hata watendaji wa ardhi hapa Dodoma, Kamishna Msaidizi na wasaidizi wake wote wanafanya kazi vizuri sana, hata pale Jiji wanajitahidi sana, malalamiko yaliyopo naamini ni kutokana na kuzidiwa na kazi, lakini pili kutokana na ukweli kwamba ile kuwa wamerithi baadhi ya migogoro kutoka kwa iliyokuwa *CDA,* nitafafanua baadaye.

Mheshimiwa Spika, baada ya pongezi naomba kutoa ushauri na maombi nikianza na Baraza la Ardhi Mufindi; wananchi wa Mufindi wanalazimika kwenda Iringa kupata huduma za Baraza la Ardhi, mara ya mwisho niliambiwa kuwa wako katika hatua za mwisho kukamilisha suala hili, ninaomba watusaidie kukamilisha suala hili, Kamishna Msaidizi wa Ardhi wa Mkoa anaweza kuwapa picha kamili, *imagine* mwananchi anatoka Mgololo, Sadani, Malangali, Mtula, Kisada na kadhalika mpaka Iringa, kwanza lazima asafiri mpaka Mafinga alale, siku ya pili asafiri hadi Iringa, *is too costly,* nawaomba watusaidie jambo hili likamilike.

Mheshimiwa Spika, pili, ni kuhusu *revolving fund* kwa ajili ya kupima *industrial park;* wakati wa bajeti ya mwaka jana na wakati wa semina ya kutujengea uwezo wa mradi wa *LTIP,* niliwafahamisha kwamba Halmashauri ya Mji Mafinga tumetenga eneo la ekari 750 kwa ajili ya *Industrial Park* na nikaomba kama sehemu ya utekelezaji ya mradi huo, tupimiwe eneo hilo, lakini niliambiwa kwamba tutapewa fedha kupitia *revolving fund,* nafahamu changamoto ambazo wamezipata baadhi ya halmashauri kwa kubadilisha matumizi ya hizi fedha, ninaomba dhambi ya wengine isituumize sisi watu wa Mafinga, kwa hiyo ninaendelea kuomba kwa msisitizo watupe fedha hii, wataona maajabu. Mafinga na Mufindi kwa ujumla ina viwanda vya mazao ya misitu 35 na uhitaji bado mkubwa ingekuwa jambo jema sana kupima *industrial park.*

Mheshimiwa Spika, kuhusu kiliniki za ardhi; nawapongeza sana, mimi ni mnufaika wa kiliniki za ardhi kwa sababu mmeweza ku-*unlock* mambo mengi sana siyo ya kwangu binafsi, lakini ya baadhi ya wananchi, ndugu na jamaa, pamoja na kuwa watu wanasema Waziri utachoka.

Mheshimiwa Spika, ni kweli anachoka, lakini kilicho muhimu Mheshimiwa Waziri ameleta amshaamsha ambayo kwanza imeleta woga kwa matapeli wa ardhi, lakini pili imeleta matumaini kwamba kumbe haki inaweza tu kupotea kwa muda, lakini iko siku haki itarejea kwa mwenye haki. Hata hivyo, nina ushauri, walau Mheshimiwa Waziri siku moja moja uweke *clinic at village level* ambako nako kuna shida kama maeneo ya mjini.

Mheshimiwa Spika, kuhusu migogoro *Dodoma vs CDA vs* wataalam, mimi nina ushauri kwa Jiji la Dodoma *and I will be very honest* kwamba ile kurithi sheria *delicate* iliyokuwa ya *CDA* imeacha makovu mengi kwa pande zote kwa maana kwa upande wa wataalamu na kwa wananchi, kwa hiyo katika kupata suluhisho migogoro ya Dodoma inahitaji utulivu na umakini mkubwa sana, hapa Dodoma hata aje Malaika kama hatutaanzia kwa iliyokuwa *CDA,* tutaumiza watumishi, tutawapeleka TAKUKURU, tutawafukuza kazi, lakini nawaambia Dodoma ni *unique case,* kwa hiyo ushauri wangu wa kwanza Serikali ipime viwanja kwa mfano 1000, ikawa kama benki ndogo ya ardhi kama viwanja mbadala vya watu wenye migogoro ya ardhi, itasaidia.

Mheshimiwa Spika, la pili, migogoro ya kimakundi kwa mfano wale wananchi 562, hakikisheni migogoro ya aina hii maelekezo yakitoka yanatekelezwa, kwa sababu unakuta jambo linaenda, linarudi nyuma, linaenda linarudi nyuma, hii inaleta sura kwamba Dodoma ni ya migogoro, kumbe ni kwa sababu tu, migogoro haiishi.

Mheshimiwa Spika, kama Mbunge ambaye ninaishi hapa Dodoma kwa *almost 70%* ya muda wangu ninakutana na hizi kero mfano ikiwa ni huu mgogoro wa wananchi 562, maarufu kama Nala Shell Mbili. Tukiweza kumaliza migogoro ya makundi

tutawasaidia wananchi wa Dodoma na sura hii kwamba Dodoma ni ya migogoro tutaifuta.

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Dkt. Festo Dugange atafuatiwa na Mheshimiwa Geophrey Mizengo Pinda, mtoa hoja ajiandae.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa nafasi hii ili niweze kuchangia hoja ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi.

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kazi nzuri na kubwa anayoifanya ya kuliongoza Taifa letu, na pia kwa kazi kubwa ambayo anaifanya katika kuhakikisha kwamba Wizara ya Ardhi inaendelea kutenda haki kwa Watanzania, ili Watanzania wamiliki ardhi bila kuwa na migogoro ya aina yoyote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pili, nikupongeze sana wewe mwenyewe kwa kazi kubwa na nzuri iliyotukuka unayoifanya ya kuliongoza Bunge letu Tukufu. Sisi Wabunge tumekuwa mashuhuda kwamba unafanya kazi kubwa sana. Hongera sana na sisi tutaendelea kukuombea ili uendelee kufanya kazi kubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, migogoro ya ardhi inatokea katika maeneo ya vijiji, mitaa, kata na maeneo yote ambayo yapo chini ya Menejimenti ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI. Sisi Ofisi ya Rais, TAMISEMI kwa kushirikiana na Wizara ya Ardhi mara kwa mara tumekuwa tukifanya vikao vya pamoja ili kushauriana na kuona njia nzuri zaidi za kwenda kutatua migogoro hii katika maeneo ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa, ili kuhakikisha wananchi katika maeneo hayo wanaendelea kupata huduma bora za ardhi, kuendelea kupunguza migogoro na ikiwezekana kumaliza kabisa migogoro katika baadhi ya maeneo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, halmashauri ndiyo mamlaka za kupanga, kupima na kumilikisha ardhi kwa wananchi katika maeneo yao. Kwa hiyo, Ofisi ya Rais, TAMISEMI tumeendelea kusimamia hilo,

kusisitiza wakurugenzi, Waheshimiwa Wakuu wa Wilaya na Mikoa kuhakikisha kwamba wanasimamia kwa karibu kazi zote zinazohusiana na masuala ya ardhi, ili kupunguza na kuondoa migogoro hii na kuwezesha wananchi kustawi katika maeneo yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, migogoro ya ardhi kuna taratibu zake za kuitatua; na utaratibu rasmi zaidi ni wa Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya. Sasa, kwa sababu mabaraza haya yapo mbali na wananchi walio wengi, Serikali kwa mapenzi yaliyo mema iliona ni vyema tuanzishe utaratibu wa vyombo ambavyo vitatatua migogoro ya kawaida katika maeneo ya vijiji, mitaa na kata husika. Kwanza, kuwapunguzia umbali wananchi kwenda kutafuta suluhu ya migogoro hiyo katika mabaraza ya ardhi na nyumba ya wilaya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baadhi ya migogoro ni migogoro ambayo kwa kweli inaweza ikatatuliwa katika ngazi za kata. Hii inawezesha pia kupunguza msongamano wa migogoro ya kawaida sana kwenda kwenye Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya. Kwa kuzingatia hilo Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Kata. Kwa mujibu wa sheria Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Kata yanateuliwa na *Ward C* (Kamati za Maendeleo za Kata husika) na wajumbe wanakuwa ni wakazi wa eneo katika kata husika na wanawajibika kusikiliza migogoro yote inayotoka katika kata hiyo katika vijiji au mitaa ndani ya kata yao.

Mheshimiwa Spika, mpaka sasa tuna jumla ya Mabaraza ya Ardhi ya Kata 3,956 kote nchini. Mabaraza haya yanafanya kazi kwa mujibu wa sheria; lakini bado pamoja na kazi kubwa ambayo mabaraza haya yamekuwa yakifanya kumekuwa na changamoto za aina mbalimbali. Hapa Waheshimiwa Wabunge wametoa hoja na ushauri kwamba, bado ufanisi na kazi za mabaraza haujawa wa kutosha. Sisi kama Ofisi ya Rais, TAMISEMI tunakubaliana na Waheshimiwa Wabunge, ni kweli tuna Mabaraza ya Ardhi ya Kata, na yana majukumu yao ambayo yameelezwa, yanakuwa *specified* wanatakiwa kufanya nini kwa hatua ipi, lakini bado tunakubaliana kwamba kuna changamoto.

Mheshimiwa Spika, changamoto hizi zimetokana na sababu kadhaa. Sababu ya kwanza inatokana na wajumbe walio wengi kwa sababu wanapatikana katika vijiji na mitaa husika ndani ya kata husika, hawana utaalamu rasmi wa masuala ya kisheria na masuala ya ardhi. Kwa maana hiyo kumekuwa kuna maeneo baadhi ufanisi unakuwa si wa kutosha.

Mheshimiwa Spika, pili, kumekuwa na changamoto za kibajeti na ndiyo maana ili kutatua changamoto hiyo, Ofisi ya Rais, TAMISEMI tulitoa maelekezo mahsusi kwenda kwa Makatibu Tawala wa Mikoa pamoja na Wakurugenzi wa Halmashauri, kwamba kwanza wahakikishe mara wanapoteua wajumbe wa Mabaraza ya Ardhi ya Kata wapate mafunzo maalum katika maeneo yale, ili wajue taratibu na sheria za ardhi zinavyowataka namna ya kwenda kutatua migogoro. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, shughuli hizo zimekuwa zikifanyika mara kwa mara katika Mabaraza ya Ardhi ya Kata kwa kuwafanyia mafunzo na kuhakikisha kwamba angalau wanajua *a,b,c,d* za kutatua migogoro katika maeneo yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la pili ambalo tumesisitiza ni kwamba, halmashauri zote zihakikishe zinatenga fedha kwa ajili ya kuwezesha mabaraza ya kata kufanya majukumu yao ipasavyo. Ikiwemo kufanya vikao mara hoja zinapotakiwa kufanyika na pia kuhakikisha kwamba wanatenda haki kwa kuzingatia kukaa vikao vile kwa muda na kuwa na maamuzi ambayo yanazingatia taratibu hizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lengo la Serikali kupitia Ofisi ya Rais, TAMISEMI ni kuzuia migogoro na pale ambapo inakuwa haijazuiwa, basi tunakwenda na hatua za kutatua migogoro. Kwa kiasi kikubwa migogoro mingi ambayo inatokea katika maeneo ya vijiji mitaa na kata zetu, haya Mabaraza ya Ardhi ya Kata yamesaidia sana kutatua migogoro hiyo. Tumekuwa mashahidi kwamba mara nyingi migogoro mingi sana inakwisha ndani ya mabaraza ya kata. Hata hivyo kuna migogoro ambayo inakuwa ni migumu inahitaji hatua za kisheria za juu zaidi. Migogoro hiyo

inakuwa *referred* kwenda kwenye mabaraza ya ardhi na nyumba ya wilaya.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo naomba niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge kwamba Serikali inatambua sana umuhimu wa mabaraza ya ardhi katika ngazi za kata, na inaendelea kuyaimarisha mabaraza hayo ili yaweze kufanya kazi kwa ufanisi zaidi na yaweze kutatua migogoro ya wananchi kwa ufanisi mkubwa zaidi na kuweza kutenda haki pale ambapo kunakuwa na migongano ya hapa na pale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na taratibu hizi ambazo zimwekwa na hatua ambayo Serikali imechukua moja kubwa ni kuendelea kuwasisitiza Viongozi wa Mamlaka ya Serikali za Mitaa na Sekretarieti za Mikoa, kuendelea kutoa elimu kwa wananchi juu ya kuzingatia sheria za ardhi katika maeneo hayo na pia jinsi ya kuzingatia kanuni na taratibu za ardhi, ili kuepusha migogoro. Kwa sababu tunaamini njia pekee ya uhakika ni kutoa elimu kwa wananchi ili…

**MHE. TIMOTHEO P. MNZAVA:** Mheshimiwa Spika, Taarifa.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** …waweze kujua sheria, taratibu na kanuni za kuzuia migogoro ya ardhi katika vijiji na matawi pamoja na kata hizo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Timotheo Mnzava.

**TAARIFA**

**MHE. TIMOTHEO P. MNZAVA:** Mheshimiwa Spika, ninaomba nimpe taarifa mzungumzaji (mchangiaji) Mheshimiwa Naibu Waziri. Ni kweli Sheria ya Mabaraza ya Kata ipo, lakini ni vizuri TAMISEMI wakajua kwamba, kwa mujibu wa sheria ile mabaraza ya kata hayapo kwa ajili ya kesi za ardhi peke yake. Kwa hiyo, hata ile *composition* yake inavyokaa ni kwa sababu yanashughulika na mambo mengine nje ya mambo ya ardhi.

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba mabaraza yamekuwa na changamoto na ni muda sahihi sasa wa TAMISEMI kwamba, pamoja *composition* na sheria ile kuwepo, kuitafakari upya sheria ili iweze kutusaidia kutatua changamoto tulizonazo hasa mahususi kwenye eneo la upande wa sekta ya ardhi yenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Dugange unaipokea taarifa hiyo?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Ninaipokea taarifa hii ya Mheshimiwa Mbunge. Ni kweli, nimetangulia kusema kwamba tunatambua kuwa tuna mabaraza ya kata, kimsingi, mabaraza ya kata yanafanya shughuli nyingi zikiwemo shughuli za kusuluhisha migogoro ya ardhi, masuala ya ndoa na mambo mengine mengi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo na sisi tunaona umuhimu kwa sababu kwa sasa mwamko wa kumiliki ardhi umeongezeka miongoni mwa wananchi na hivyo migogoro imeendelea kuongezeka. Tunaona umuhimu sasa wa kuwa na baraza mahsusi ambalo linaweza likatatua migogoro hii kwa ufanisi mkubwa zaidi. Kwa hiyo tu kwamba niseme tunapokea maoni hayo na sisi Serikali tutakwenda kuyafanyia tathmini na kuona namna nzuri zaidi ya kuboresha ili ufanisi wa mabaraza ya ardhi ya kata uweze kuongezeka.

Mheshimiwa Spika, nitumie nafasi hii kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI kuwasisitiza viongozi, Waheshimiwa Wakuu wa Mikoa, Makatibu Tawala wa Mikoa na menejimenti za mikoa yote nchini, pia Wakuu wa Wilaya, Wakurugenzi na Wakuu wa Idara; kwanza kuhakikisha wanasimamia Mabaraza ya Ardhi ya Kata ili yaweze kutoa huduma ipasayo kwa kadiri ya sheria, maelekezo na taratibu ikiwemo kusimamia kuona kwamba yanafanya vikao mara kwa mara na pia kuhakikisha yanatenda haki. Pale ambapo yatahitaji kusaidiwa tuna Wakuu wa Idara, Wanasheria na Maafisa Ardhi katika halmashauri wanaweza

wakaingia na kusaidia kabla ya kufanya *reference* kwenda kwenye ngazi ya Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya.

Mheshimiwa Spika, pili nitumie nafasi hii kusisitiza halmashauri zetu kuendelea kutenga fedha kwa ajili ya kuwezesha kazi za mabaraza ya ardhi ya kata ili yaweze kutoa huduma vizuri zaidi na kuendelea kuondoa migogoro ya wananchi katika maeneo hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema haya, nakushukuru sana kwa nafasi hii. Niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge kuwa Ofisi ya Rais, TAMISEMI tutaendelea kuyasimamia Mabaraza ya Ardhi ya Kata, ili yaweze kutatua migogoro hii.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Geophrey Mizengo Pinda, mtoa hoja ajiandae.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, kwanza nianze kwa kusema kwamba, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kabla sijaanza kutoa mchango wangu nitoe pole kwa wananchi wa Jimbo la Kavuu, kata moja huko ambako ni wakulima maarufu wa zao la mpunga wakati wanafanya juhudi za kuondoa mpunga ule kwenye maji, ule mtumbwi waliokuwa wanautumia ulibeba wananchi kama 14, tumepoteza wananchi saba. Ilikuwa ni siku ya Ijumaa na leo ndiyo tumefunga hilo zoezi la kusaka miili mingine; lakini tumefanikiwa kupata miili minne.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo natoa pole sana kwa wananchi wangu hapo. Mungu akaziweke mahali pema peponi roho za marehemu wetu. Vilevile wale majeruhi waliopata msukosuko basi warejeshewe afya njema ili waweze kuendelea na shughuli zao.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili ambalo ningeanza nalo ni kumshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kuendelea kuniamini katika kusidia Wizara hii, kumsaidia Mheshimiwa Jerry katika kazi zake za Wizara hii. Vilevile kwa Mheshimiwa Rais kutuongezea uwezo Wizara katika utekelezaji wa majukumu ya kila siku ya Wizara yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimshukuru vilevile Makamu wa Rais, Mheshimiwa Waziri Mkuu na Naibu Waziri Mkuu kwa jinsi wanavyoendelea kutupa miongozo ya kutekeleza majukumu yetu katika sekta hii ambayo katika mazingira ya kawaida ni sekta muhimu sana katika nchi yetu. Kwa kweli kutokana na umuhimu wake; kitu chochote kilicho na umuhimu mara nyingi kinagubikwa na mambo mengi ambayo migogoro ni sehemu ya mambo yanayojitokeza katika jambo lililo jema.

Mheshimiwa Spika, nikushukuru wewe mwenyewe, Naibu Spika, pamoja na uongozi wa Bunge kwa miongozo mbalimbali ambayo mmeendelea kutusaidia.

Mheshimiwa Spika, nitajibu maeneo machache na mtoa hoja atakuja kujumuisha mambo yote. Nianze na Mpango wa Matumizi Bora ya Ardhi. Waheshimiwa Wabunge mbalimbali walichangia, ambao ni Mheshimiwa Edward Olelekaita, Mheshimiwa Ally Juma Makoa, Mheshimiwa Agnes Hokororo, Mheshimiwa Taska Restituta Mbogo, Mheshimiwa Hawa Subira Mwaifunga na Mheshimiwa Munira Mustapha, ambao kwa pamoja walizungumzia mambo mbalimbali yanayohusiana na tume, hasa kwenye suala la kuongezewa uwezo ili tume, iweze kutekeleza wajibu wake kwa ufanisi na kwa muda mfupi katika kupambania mazingira ya kuiweka nchi katika utambuzi wa matumizi bora ya ardhi.

Mheshimiwa Spika, hadi sasa vijiji ambavyo vimepimwa ni 10,000. Nataka kuweka tofauti kati ya kupimwa na kuboresha matumizi bora ya ardhi ya vijiji, isije ikawaletea *confusion.* Vijiji kati ya 12,318 sawa na 88% ya vijiji vyote hapa nchini. Kati ya vijiji hivyo vilivyoandaliwa matumizi bora ya ardhi ni vijiji 4,126 sawa na 33.5% ya vijiji vyote.

Mheshimiwa Spika, kwa kutambua umuhimu wa kukamilisha uandaaji wa mipango ya matumizi bora ya ardhi ya vijiji vilivyobaki, Serikali imeendelea kuongeza bajeti ya tume kwa ajili ya kazi hiyo. Katika mwaka wa fedha huu wa 2024/2025 bajeti imeongezeka kutoka bilioni 3.41 hadi bilioni 5.04. Wizara katika Mwaka wa Fedha 2024/2025 kupitia Mradi wa *LTIP* kiasi cha shilingi bilioni 15 kwa ajili ya kupanga vijiji 1,000 zimetengwa.

Mheshimiwa Spika, kuendelea kuhamasisha wadau ni njia nyingine ambayo tunaendelea kuitumia kwa ajili ya kupata fedha ambazo zinaweza zikasaidia, na hivyo katika mwaka 2024/2025 shilingi bilioni moja zitachangiwa na wadau. Hayo ni matarajio yetu makubwa kabisa. Wizara itaendelea kutenga fedha kila mwaka kwa ajili ya kuijengea uwezo tume

Mheshimiwa Spika, nataka niwape *comfort* Waheshimiwa Wabunge; jambo hili ni kubwa sana na hata Serikali imeliwekea umuhimu wa pekee. Kwa sasa tunaendelea na mazungumzo kati ya Wizara ya Fedha na Wizara yetu kuona kama tunaweza tukapata kile kiasi cha shilingi bilioni 120 ambalo ndilo kadirio la mwisho ambalo fedha hizi zikipatikana zitakamilisha nchi nzima kupimwa kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, tayari mawasiliano ya kiofisi yanaendelea; tumwombe Mwenyezi Mungu awajalie watu wa Wizara ya Fedha wawezeshwe na Mwenyezi Mungu, tushushiwe hizo fedha ambazo katika mazingira ya kawaida tume inaweza ikafanya kazi katika muda mfupi sana. Kwa sababu ni ukweli usiopingika kwamba zoezi hili la kuweka mipango ya matumizi bora ya ardhi limetoa matokeo makubwa sana katika kutatua migogoro mbalimbali katika maeneo mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, *once* wanapopima wakimaliza hata ile migogoro iliyokuwepo inakuwa ndiyo mwisho wa safari ya mgogoro ule. Hayo tumeyabainisha katika maeneo mbalimbali na ambayo katika mazingira ya kawaida yameonesha mafanikio makubwa sana. Kwa hiyo, niwaombe Waheshimiwa Wabunge tuendelee kuwa watulivu katika kipindi hiki ambacho Serikali

inapambania kupata fedha, ili ziweze kwenda kutuletea matokeo ambayo ni matarajio ya Watanzania wote.

Mheshimiwa Spika, sambamba na eneo hili Waheshimiwa Wabunge wengi wamezungumzia kuhusu elimu inayotolewa wakati wa zoezi zima la kwenda kufanya maboresho kwenye maeneo ya vijiji. Kuna hatua kama saba ambazo tunazipitia. Kwanza, ni kuhakikisha tu kwamba tunapofika kwenye vijiji wale wanavijiji wanakuwa ni watu wanaotangulizwa mbele katika kuandaliwa kupokea ule mradi. Kwa hiyo elimu inatolewa na kamati zinazokwenda kusimamia utambuzi wa yale maeneo ni kamati za wanakijiji wenyewe, tunaunda timu maalum ambayo kwa wale ambao bahati mbaya sana siyo rahisi kuwabeba Waheshimiwa Wabunge wote kwenda kwenye maeneo haya, lakini tumeipeleka Kamati maeneo mbalimbali, wameshuhudia kwamba tafsiri ya kutambua matumizi ya ardhi katika vile vijiji haitolewi na afisa ardhi.

Wale wameshibishwa kuelewa jinsi tutakavyokwenda kutumia lile eneo lao na wao ndiyo wana-*own*, wanabeba ule uzito wa kutambua matumizi bora ili waweze kuwa ni sehemu ya walinzi wa ile miradi. Kwa hiyo, ikitokea kuna maeneo ambayo Maafisa Ardhi wanaenda kulazimisha, ninaomba sana Waheshimiwa Wabunge tupewe taarifa haraka kwa sababu *ownership* ya usimamizi wa mradi ule inafanywa na wananchi wenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sisi tunakuwa tu kama wataalamu na hata ukienda kule wao ndiyo wanaojua kabisa kijiji chao kinapakana na hiki, mtaa huu nani anapakana na nani na kule tuna Kamati ambayo haiishii tu kwenye kipindi kile cha zoezi, inaendelea na shughuli hizo katika muda mrefu sana.

Mheshimiwa Spika, maeneo yale kwenye vijiji, nimemsikia Mheshimiwa Getere, ninadhani hata Mheshimiwa Olelekaita; masuala ya kulazimisha *WMA* kwenye maeneo ambayo tunakwenda kutambua, itambuliwe kwamba, Sheria ya *WMA* iko chini ya vijiji vyenyewe. Wala ile siyo ardhi inayosimamiwa na

Maliasili wala siyo ardhi inayosimamiwa na mamlaka nyingine yoyote.

Mheshimiwa Spika, uamuzi wa kulinda msitu ule ulioachwa kwenye eneo lile la kijiji kile ni wa wananchi wenyewe na unapitia kwenye vikao vyao vya wazi na hata hiyo *WMA* kwa sababu inaweza ikawa inaleta matokeo, hata uongozi wa *WMA* ni wa wananchi wenyewe. Wala hakuna kiongozi mwingine wa Serikali anayeweza kusimamia lile eneo.

Mheshimiwa Spika, niwape tu mfano, kwangu kuna *WMA* ambayo inasimamiwa na wananchi wenyewe kwa kuchaguana wao wenyewe. Kwa hiyo, kama haya yako kwenye maeneo yetu huko tunakotoka, ninaomba tu wananchi waelewe kwamba mpango wa matumizi bora ya ardhi na mkaacha na eneo la *reserve*, maamuzi juu ya mnalitumiaje lile eneo kawaida linafanyiwa maamuzi yake na wananchi wenyewe.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ninaomba tu, kama kuna mashinikizo yanatolewa, basi hayo mashinikizo siyo sahihi, wanatakiwa viongozi wote ambao wanasimamia zoezi hili cha kwanza waanzie kwenye elimu. Waweze kutoa elimu ya kutosha juu ya wanachokifikiria wananchi wale kukitenga kwa ajili ya matumizi yao ya baadaye na maeneo mengine wanagongana kwa sababu wanataka kutenga eneo la kufugia, lakini *at a same time* wanajikuta wana maeneo ambayo wangetaka kuhifadhi. Kwa hiyo, haya ni maamuzi ambayo kijiji kinaweza kikaamua kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, urejeshwaji wa fedha za miradi ya kupanga, kupima na kumilikisha; Waheshimiwa Wabunge, Wizara itaendelea kushirikiana na TAMISEMI zile fedha ambazo zimeenda kule kwa ajili ya mikopo na kwa kweli ninatumia Bunge lako Tukufu kuwahamasisha Wakurugenzi wa halmashauri mbalimbali nchini kurejesha fedha hizi ambazo kimkakati Serikali ililenga kutuwezesha sisi watu wa Wizara ya Ardhi kupima maeneo ya nchi yetu, hasa kwenye miji inayochipukia kama halmashauri hizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, halmashauri zingine usimamizi wa zile fedha umekuwa ni hafifu sana na wanashindwa kurejesha kwa wakati ili na wenzao waweze kuzipata. Ninaamini wazi wananchi wamesikia kilio cha Wabunge ambao hawajafikiwa na miradi hii lakini sisi kama Wizara tunaendela kujipanga kuona namna nzuri ya kuendelea kuhamasisha halmashauri kurejesha zile fedha.

Mheshimiwa Spika, hata kwenye miradi mingine sasa hivi tumebaini, ni lazima sisi wenyewe tuzisimamie zile fedha kwa sababu tumeshapima uaminifu wa halmashauri una kasoro kasoro, basi hata kama halmashauri itapata, usimamizi wa matumizi ya ile fedha katika miradi wanayopanga halmashauri itasimamiwa na Wizara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo Waheshimiwa kwa namna mbalimbali wameweza kulizungumzia ni suala la utatuzi wa migogoro ya ardhi katika vijiji 975. Baraza chini ya ile Kamati ya Mawaziri Nane ilishatoa ufafanuzi wa majibu mbalimbali katika namna ya kutekeleza maeneo mbalimbali yanayopitiwa na mradi huu.

Mheshimiwa Spika, tumechukua lile la Mheshimiwa Kawawa ambalo alisema kwenye kijiji chake kuna watu wana uasili, lakini mazingatio makubwa kwa sababu hata haya maamuzi ya Kamati ya Mawaziri Nane ilipita huko na kujiridhisha juu ya maelezo ya msingi ambayo yalisababisha maamuzi hayo yakatokea. Bado milango iko wazi, Wizara hii ndiyo Mwenyekiti wa Kamati ile ya Mawaziri Nane, kama kuna hoja zingine za msingi ambazo tunaweza tukazipokea na tukakaa kwenye kiti kimoja tukazungumza, *then* tuone, lakini maamuzi ya Baraza la Mawaziri lile ambalo lilitumwa na Mheshimiwa Rais, kimsingi tumetumia lile kama mwongozo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mchakato wa kupitia Sera ya Ardhi, Mheshimiwa Waziri atalieleza vizuri na sababu za msingi kwa nini tumeleta sera mpya. Mheshimiwa Waziri ana maelezo ya ndani kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mabaraza ya Ardhi; ninampongeza sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa mchango wake kuhusu Mabaraza haya ya Kata. Tuliyaondolea uwezo wa kuwa wanatoa hukumu kwa sababu hawana Vyombo vya Kisheria. Mwenyekiti ni mwananchi mwenzao, hana elimu ya sheria ambayo inaweza ikamsaidia kutoa uamuzi wenye haki kwa sababu, vigezo vya sheria vinampeleka mtu darasani. Lazima asome ajue miiko, hapa mmeamua nini na hapa mmeamua nini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ninadhani Serikali ilipoyapitia yale maamuzi mbalimbali yaliyofanywa na Mabaraza ya Kata, iliona ni muhimu waishie kwenye usuluhishi, upatanishi ili kujenga misingi mizuri ya mahusiano katika kile kijiji au katika ile migogoro. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tukija kwenye Mabaraza ya Wilaya, haya ni kweli Wabunge wamesema wanabaini yana changamoto. Siyo kwamba wamebaini wao tu, toka tumeingia na Mheshimiwa Waziri hapa, jambo la kwanza tunaendelea kuangalia uwezekano wa kufanya maboresho. Hapa hapa nina sauti mbili katika Mabaraza haya, moja ni ile *process* ya Serikali kuyahamisha Mabaraza haya kurudi Mahakamani, lakini yale hata yakichelewa hayajatuzuia sisi kuendelea kutengeneza mpango mzuri wa kuhakikisha Mabaraza haya yanatoa haki iliyo sawa. Kwenye Mabaraza huko hakuna *prosecution* hakuna nini, nako kuna vitu ambavyo kama Wizara tumeanza kuviangalia ili tuviweke vizuri ili baadaye huko tuweze kuona namna ambavyo tunaweza, wale Wenyeviti wakatoa haki zinazolingana na uhalisia wenyewe.

Mheshimiwa Spika, kwenye eneo hili la Mabaraza, vilevile, hatujafungua Mabaraza nchi nzima kwa maana kwamba hatujateua wale Wenyeviti. *Process* yake ni kwamba tumebakiza Wenyeviti kama 35 katika halmashauri zote na hili limeshafikia kwenye mchakato. Tuliona hatuwezi kumleta mtu ambaye hana hata *experience* ya kufanya kazi. Kwa hiyo, Serikali tulikubaliana kwamba tuchukue wanasheria ambao tayari wako kazini tuwahamishie kwetu ili hata wanapokwenda kukalia meza za maamuzi angalau wawe na *reference* mbalimbali. Maana sheria

inataka vilevile uwe na uwezo wa utangulizi, *experience* na vitu vingine katika kuamua jambo ambalo linahusisha haki za watu.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, hili tunaendelea na mchakato na niwape *comfort* tu Waheshimiwa Wabunge, tunakwenda kukamilisha zoezi hili la kuwaletea Wenyeviti wa Mabaraza haya. Nia yetu ni kwa wilaya zote hapa nchini ziweze kuwa na uwakilishi wa hawa Wenyeviti ili kuwapunguzia adha wale wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa mfano Kiteto, Mwenyekiti wa Baraza anatoka Dodoma, mbali sana na hapa pana mrundikano wa kesi nyingi sana. Kwa hiyo, ile *jam* haimpi nafasi ya kuhudumu kwenye maeneo mengine kwa uhuru wa kutosha. Kwa hiyo, haya yote haya tumeyaona na kuna maeneo mengine ni mbali sana. Ni mbali mno kutoka wilaya moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaomba nimalizie, la kumalizia ni kwamba yale yote ambayo Waheshimiwa Wabunge wametoa kwetu ni maelekezo, ushauri, kwa kweli leo ninapata nguvu ya kutosha kabisa. Wabunge watakumbuka ndiyo nilikuwa ninaingia kwenye Bajeti ya mwaka jana, ile presha ilisababisha maradhi ya kutumia vidonge, lakini ninawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge kwa sababu, kwa kweli kwa mwenendo huu wa kuendelea kutuamini tunakwenda kufanya kazi ambayo wataiona. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninamshukuru sana Mheshimiwa Waziri wangu toka ameingia, katika mazingira ya kawaida lazima ujifunze kutoka kwa aliye juu yako. Ninajifunza vitu vingi sana kutoka kwa kaka yangu hapa Mheshimiwa Jerry, ni mtu ambaye anasimama kwenye sheria na Wabunge wameona wote hapa nchini shughuli tunayokwenda kuifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, siwezi kukaa ofisini wakati Waziri wangu yuko kazini, kwa hiyo kwa mwendo wake ule ule na bahati nzuri mimi msaidizi wake ni mwanajeshi. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Kengele ya pili imeshagonga Mheshimiwa. Kengele ya pili imeshagonga.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, kwa hiyo ninamsaidia kwenda mahali popote ambapo kiatu chake hakifiki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimalizie tu kwa kusema nitaendelea kumpa ushirikiano Mheshimiwa Waziri, nitamshauri kwa hekima na kwa wakati wote, anitumie kadiri atakavyoweza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kuyasema haya, ninaunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, sasa nimwite Mheshimiwa Jerry William Silaa, Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi ili aje ahitimishe hoja ya Wizara yake.

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, ninaomba nikushukuru wewe kwa kunipa nafasi ya kuja hapa kuhitimisha hoja yangu, lakini niruhusu niwashukuru kidhati Waheshimiwa Wabunge kwa michango yao mizuri sana, ninawashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jumla ya Wabunge 45 wamechangia, Wabunge 40 wamechangia hapa Bungeni na Wabunge watano kwa maandishi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaomba uniruhusu nitumie fursa hii kumshukuru kidhati Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuniamini nimsaidie kazi. Ninamwahidi nitafanya kazi kwa uaminifu na kwa moyo na kwa nguvu zangu zote na nitaishi kiapo changu wakati wote kumshauri kwa hekima na uaminifu. Ninamshukuru kwa maagizo na maelekezo na miongozo anayotupatia Wizara ya Ardhi, hasa falsafa yake ya *4Rs* na sisi tumejikita zaidi kwenye zile *R* mbili za mwisho za *Reforms and Rebuilding*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niruhusu nimshukuru Mheshimiwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango kwa miongozo yake anayoendelea kutupatia na usimamizi. Ninaomba tena unipe fursa nimshukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu, Mheshimiwa Dkt. Doto Mashaka Biteko kwa miongozo na usimamizi wao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaomba nitumie fursa hii kuishukuru Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii. Kipekee ninamshukuru Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Timotheo Mnzava (Mbunge), Mheshimiwa Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Najma Murtaza Giga na Wajumbe wote. Tunawashukuru sana kwa usimamizi wao, ushauri na maelekezo yao. Ninahakika tutazingatia katika utendaji wa kazi zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Bunge lako mwaka 1995 lilitunga Sheria, Sura Na. 398, Sheria hii imeainisha, kiongozi ni kiongozi mwenyewe, mke au mume wake na watoto chini ya miaka 18. Niruhusu nitumie fursa hii kuishukuru sana familia yangu hasa mke wangu Bi. Mariam Bakar Silaa kwa matunzo yake. Kazi hii inachukua muda mrefu, kule nyumbani hatuonekani, bibi huyu wa Kitanga hodari. Malezi ya mtoto simba yako vizuri, utulivu wa Waziri uko vizuri, mambo ya huduma zote yako sawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kazi ya ardhi ni ngumu, utoke kwenye mgogoro wa ardhi usiku saa tano ukutane na mgogoro wa mwanamke nyumbani, utatembea unaongea mwenyewe kama chizi. Ninaomba nitumie fursa hii kumshukuru sana na Mwenyezi Mungu amjalie na aendelee kuniombea dua njema. *(kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninakishukuru Chama changu Cha Mapinduzi, kwani kimenilea toka ngazi ya tawi, Jumuiya ya Umoja wa Vijana, leo nimesimama hapa kama zao la chama hiki. Ninaomba nitumie fursa hii niwashukuru wapigakura wangu wa Jimbo la Ukonga na leo baadhi yao wako hapa, kwa kunivumilia

katika kipindi ambacho ninatumikia Serikali na kuendelea kuniunga mkono kule jimboni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninampongeza Katibu wangu Ndugu Ayubu Msalika na wenzake pale kwenye ofisi ya jimbo kwa kazi kubwa anayoifanya ya kuendelea kuwahudumia wananchi.

Mheshimiwa Spika, kipekee ninaomba nikupongeze wewe binafsi, kwanza kwa kuchaguliwa kuwa Rais wa Mabunge ya *IPU*. Uchaguzi wako mimi sikupata shaka, sisi tunaofahamu sifa zako tulijua unastahili na unafanya vizuri, Mwenyezi Mungu akubariki sana. Aidha, ninaendelea kukupongeza wewe pamoja na Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu, Naibu Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kuendelea kuongoza na kusimamia kwa umahiri shughuli za Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile, ninawapongeza Mheshimiwa Dkt. Joseph Kizito Mhagama na Mheshimiwa Deodatus Phillip Mwanyika, kwa kuteuliwa kuwa Wenyeviti wa Bunge. Tunawaombea Mungu aendelee kuwasimamia katika kazi zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Wabunge wengi waliochangia wamenipongeza. Upo msemo wa Kiswahili unasema; "Usimsifie mwenye mbio, msifie anayemkimbiza." Kazi tunazofanya Wizarani sifanyi peke yangu, ipo timu pale Wizarani, ninaomba nitumie fursa hii, kwanza kumshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Geophrey Mizengo Pinda, Naibu Waziri wa Ardhi na Mbunge wa Kavuu. Ninatumia fursa hii vivevile kumpa pole kwa kupoteza wananchi wake saba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, unaweza ukamwona Mheshimiwa Pinda ni mkimya, kwanza amepita jeshini na wewe unafahamu ndiyo Mjeshi wa Bunge hili, lakini la pili, ana uzoefu mkubwa wa utumishi wa umma. Pale Wizarani anatusaidia sana hasa sisi katika kuona jinsi gani ya kuenenda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninamshukuru *Engineer* Anthony Sanga, Katibu Mkuu wa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya

Makazi. Pale Wizarani tunamwita Baba Paroko, Mtendaji huyu ana sifa zote za utendaji wa umma. Ni mtu mpole, msikivu na Waheshimiwa Wabunge wengi hapa ni mashahidi jinsi anavyoendesha Wizara yetu ya Ardhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninamshukurui Bi. Lucy Kabyemela, Naibu Katibu Mkuu ambaye pale kwetu kwenye Uongozi wa Wizara ndiyo *practitioner* wa Wizara. Amekuwa akitushauri na kutusaidia vizuri na amekuwa kiungo kizuri baina yetu sisi viongozi wakuu wa Wizara na watumishi wenzake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Ndugu Nathaniel M. Nhonge, Kamishna; Evelyne Mugasha, *Chief Valuer;* Mkurugenzi wa Upimaji na Ramani na watendaji wote wa Menejimenti, lakini watumishi wote wa Ardhi ngazi za mikoa na wilaya ambao wanatekeleza majukumu yao ya kila siku, tunawashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninawashukuru viongozi wa dini hasa kiongozi wangu wa kiroho Baba Askofu Alex Gehaz Malasusa kwa malezi ya kiroho. Ninawashukuru pia viongozi jimboni, Ijumaa walikuja hapa Mashekhe na leo amekuja *Prophet* Nicholaus Suguye, yuko hapa katikati yetu, wameendelea kutuombea na kutusaidia kiroho. Tunaendelea kuwaomba waombee Taifa letu, wamwombee Rais wetu na waendelee kutuombea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimejifunza mengi kwa marehemu baba yangu *Captain* William John Silaa lakini nitasema mambo mawili. Baba yangu alinifundisha mambo mengi, lakini makubwa mawili; la kwanza ni kuheshimu kazi. Wale waliowahi kufanya kazi na mzee yule Mheshimiwa Tabasamu anafahamu, alikuwa ni mtu mwenye kuheshimu kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la pili, alinifundisha ukiamka asubuhi lazima uandike *to-do list,* uandike orodha ya shughuli utakazozifanya na jioni ufanye tathmini ya yale uliyoyafanya, ni yapi umefanikiwa na ni yapi hujafanikiwa ili uyahamishie siku nyingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mafunzo hayo yamenifanya na mimi nije na miongozo mitano ambayo nimewapa watendaji wa Wizara wawe wanayazingatia katika utendaji wao wa kazi. La kwanza ni *sense of urgency*, lazima tunavyofanya kazi ya umma tuweke *seriousness* na kuwa na uharaka wakati wote kwa sababu wananchi tunaowahudumia wanahitaji matokeo ya kwenda kufanya shughuli zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, msingi wa pili ni *sense of care*, lazima tuwajali Watanzania, lazima tuwahudumie kwa upendo, lazima tuwajibu kama sisi tukijibiwa hivyo tutajisikiaje ndani ya mioyo yetu. Ndiyo maana pale Wizarani nimekataza kuacha kusaidia Watanzania na tuanze kuwahudumia kwa sababu ni haki yao kupata huduma kwenye Serikali yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la tatu ni *discipline* (nidhamu), lazima tukisema saa mbili ni saa mbili, lazima tukisema saa nne ni saa nne, lazima tuheshimu watu na lazima tuheshimiane. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la nne ni *attentiveness*, lazima tuwe tunasikiliza na kuelewa, siyo unaambiwa kitu leo unamwambia mwananchi akija kesho hukumbuki alikwambia nini. Lazima uzingatie; pale Wizarani tuna wataalamu, sisi ni viongozi, ukimsikiliza mwananchi msikilize kwa makini, umwelewe ili uweze kumtatulia shida yake.

Mheshimiwa Spika, la tano ni *result orientation*, lazima tuwe na majawabu ya matatizo ya Watanzania. Hatuwezi kuwa watu ambao tumekaa na majibu, aliniambia Mheshimiwa Yahya Nawanda, ninafikiri Mkuu wa Mkoa wa Simiyu rafiki yangu; tuwe na majawabu, majibu ni njoo kesho, majibu nashughulikia, majawabu Mheshimiwa Janejelly ni shahidi, tumeweka kliniki pale ya Bunge, amepata hati zake tano, nyingine alikuwa anashughulikia kuanzia 2010, amezipata hapa leo, alikosa tu muda wa kuchangia. Lazima tuwe na majawabu, ndiyo ile *to do list* aliyonifundisha baba yangu, uweke malengo yako, uweke matokeo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, haya matano yanatumika kwenye *corporate world*, humu kwenye Serikali tumeongeza la sita la *integrity*, lazima tufanye kazi yetu kwa uadilifu. Maneno matakatifu ya Mungu, kutoka kitabu cha Kutoka, mlango wa 23, mstari wa nane, neno la Mungu linasema: "Kwani hiyo rushwa hupofusha macho hao waonao na kuyapotoa maneno ya wenye haki." Ukifanya kazi hii hasa ya ardhi, sina nia ya ku-*discourage sector* nyingine, ukifanya bila *integrity* utapofuka macho na ukipofuka macho maneno ya wenye haki utayapotoa, utajikuta unayoyasikia wewe huwezi kupata tena ule uwezo wa kusikia kwani macho yako yamepofushwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nilithibitishie Bunge lako, tumedhamiria kufanya kazi. Wizara ya Ardhi tumedhamiria kufanya kazi, Waheshimiwa Wabunge hapa wamesema wengi kwamba ardhi ni rasilimali muhimu sana, kilimo kinafanyika kwenye ardhi, mifugo kwenye ardhi, maliasili ni ardhi, maji na vyanzo vyake ni ardhi, mazingira ni ardhi, madini ni ardhi, miundombinu na nishati zote zinapita kwenye ardhi. Waheshimiwa Wabunge wameshauri sana kwamba Wizara hii ni sekta mtambuka na tufanye kazi kwa kushirikiana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nilithibitishie Bunge lako Tukufu tunashirikiana sana ndani ya Serikali, Wizara zote zinazohusiana na ardhi tunashirikiana na kama mlisikiliza hotuba ya Mheshimiwa Bashe hapa, ndani ya bajeti ya Kilimo ametenga shilingi bilioni tano kwa ajili ya upimaji wa ardhi za mashamba na tutaendelea kufanya kazi kwa karibu na Mheshimiwa Abdallah Ulega, Waziri wa Mifugo, Mheshimiwa Antony Mavunde, Waziri wa Madini, Mheshimiwa Angellah Kairuki na Mawaziri wengine wote tukiratibiwa vizuri sana na Mheshimiwa Waziri Mkuu wetu Kassim Majaliwa Majaliwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Condester Michael Sichalwe, ametukumbusha maneno ya msingi sana ambayo Baba wa Taifa aliyasema mwaka 1958 ni maneno marefu sina haja yakuyarudia lakini yapo kwenye *Hansard*. Baada ya uhuru, Mwalimu Nyerere aliamua kidhati kabisa kuondosha umiliki wa ardhi kwa utaratibu wa *free hold*, akaleta umiliki wa ardhi kwa

utaratibu wa *lease hold* mwaka 1963 lakini kama haitoshi mwaka 1969 akaweka utaratibu wa *rights of occupancy*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kuliarifu Bunge lako bado misingi aliyotuwekea Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere ipo pale pale. Ardhi yetu yote nchi hii kilometa za mraba 948,132 zinamilikiwa kwa pamoja na umma wote wa Watanzania milioni 61.7 na wale wenzangu na mimi tunapata haki ya ku-*occupy rights of occupancy*. Tunapata haki ya ku-*occupy* ardhi ambayo inamilikiwa na Watanzania wote na mdhamini wa ardhi hii ni Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ardhi yetu imegawanyika kwenye makundi matatu, alisema Mheshimiwa Olelekaita akichangia, ipo ardhi ya jumla kwa sasa ni 10%, ipo ardhi ya vijiji kwa sasa ni 57% na ipo ardhi ya hifadhi na sasa ni 33%. Bunge hili limetunga sheria 13 ambazo zinasimamia sekta ya ardhi. Kwa kuwa wote tunaotumia ardhi, tunatumia ardhi ya Watanzania ndiyo maana tunapaswa kulipia Kodi ya Pango la Ardhi. Kodi hii tunawalipa Watanzania, kodi hii tunawalipa wamiliki wa ardhi kwa sisi kutupangisha kuitumia.

Mheshimiwa Spika, nilisema kwenye hotuba yangu, tumeanzisha kampeni ya ulipaji wa Kodi ya Ardhi. Yupo Mbunge amechangia leo aliomba sana tukianza oparesheni tuanze na watu wakubwa wakubwa tusianze na watu wadogo. Kampeni hii imeitikiwa vizuri sana, wakati nakuja ku *wind up* hoja yangu hapa nimeletewa orodha ya viongozi.

Mheshimiwa Spika, nikupongeze umelipia kodi ya pango la ardhi, ungeniweka katika wakati mgumu sana tunapoanza zoezi. Nikuthibitishie Wabunge wa Bunge lako mpaka leo ninavyozungumza na muda bado upo, 96% wamelipia Kodi ya Pango la Ardhi. Niwaombe Waheshimiwa Wabunge ambao hawajalipa, walipie Kodi ya Pango la Ardhi, hawanilipi mimi wala hawalipi Wizara ya Ardhi, wanawalipa Watanzania ambao ndiyo wamiliki wa kodi ya ardhi na fedha hii wataitumia kwenye huduma zao za jamii ambazo zipo majimboni mwenu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mdogo wangu Diamond Platnumz alikuwa amesafiri na alijua nimepania kuanza na yeye, leo ameenda kulipa kodi zake za pango la ardhi. Maana niliwaelekeza wataalamu wangu tukianza tuanze kama Bunge lilivyoshauri, tuanze na wale watu ambao jamii inawaangalia ili watu wajue kwamba sheria ni msumeno. Nitumie Bunge lako Tukufu kuwaomba wananchi wa Tanzania kulipa Kodi ya Pango la Ardhi, kuwalipa Watanzania ambao ndiyo wamiliki wa ardhi yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge wamechangia kwenye maeneo mengi na yote ni muhimu, nitaanza na yale ya jumla na baadaye nitaenda kwenye yale maeneo moja moja. Maelekezo ya Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, ametupa maelekezo twende tukatende haki ya Watanzania kwenye ardhi. Naomba nimnukuu Mheshimiwa Rais, alituelekeza; "Simamieni haki za watu kwenye ardhi ndiyo msingi wa kila kitu, ardhi ndiyo utajiri wa wananchi na kila kitu ni ardhi." Hayo ni maneno ya Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la haki ni jambo la Mwenyezi Mungu, maandiko matakatifu kutoka Kitabu cha Yeremia, mlango wa 22, mstari wa tatu, neno la Mungu linatueleza; "Bwana asema hivi, fanyeni hukumu na haki, mwokoeni mkononi mwa mdhulumu yeye aliyeibiwa." Kitabu cha Isaya, mlango wa 32, mstari wa 17 kinasema; "Matunda ya haki yatakuwa amani na matokeo ya haki yatakuwa utulivu na matumaini milele." *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, maelekezo ya Dkt. Samia Suluhu Hassan ya kwenda kuwatendea Watanzania haki yanalenga kuingiza matumaini kwenye mioyo ya Watanzania, yanalenga kudumisha amani na utulivu kwenye Taifa letu hasa kwenye rasilimali hii muhimu ya haki. Kila siku asubuhi tukiingia hapa Bungeni tunaomba dua kwa Mwenyezi Mungu na kwenye dua lile yapo maneno yanasema; "Ee Mwenyezi Mungu Mtukufu, Muumba wa Mbingu na Dunia, umeweka katika dunia Serikali za wanadamu na Mabunge ya Mataifa ili haki yako itendeke." Suala la haki ni

suala la Kimungu na Serikali inapaswa kusimamia haki za watu na Bunge hili linapaswa kusimamia haki za watu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niwapongeze Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia, wote wamezungumza haki ya wananchi wao, haki za mipaka, haki za vijiji, haki za wakulima, haki za wafugaji na haki za mijini. Niahidi katika kipindi chote nitakachotumika kwenye Wizara hii nitasimamia haki bila kumwonea mtu yeyote na tutafanya hivyo kwa maelekezo ya Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan lakini kwa maelekezo ya Mwenyezi Mungu ambaye si tu tutaishi hapa duniani lakini mbele za haki tutaenda kukuta hesabu yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kazi kubwa imefanyika kwenye sekta ya ardhi, Serikali imefanya kazi kubwa, nimeeleza hatua mbalimbali toka kipindi cha uhuru wa nchi yetu, hatua za Baba wa Taifa, Serikali ya Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, nimeeleza hatua na wengi hapa wamechangia. Serikali za Hayati Alhaji Ali Hassan Mwinyi ambaye ndiyo baba wa mageuzi ya kiuchumi na kisiasa nchini kwetu. Yeye ndiyo aliyeleta Sera ya Ardhi na imechangiwa vizuri hapa leo. Serikali ya Mzee Benjamini William Mkapa, ndiyo iliyokuja na Sheria ya Ardhi Namba Nne na Namba Tano. Serikali ya Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, Serikali ya Dkt. John Pombe Magufuli na sasa Serikali ya Awamu ya Sita. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, bado kuna matatizo lazima tukiri. Ipo migogoro, migogoro ya mipaka, migogoro ya mirathi, migogoro ya dhuluma, migogoro ya uvamizi, wapo watu wenye nguvu wanavamia wanyonge, lakini wakati mwingine wapo hata wananchi na wenyewe wanavamia maeneo mbalimbali yaliyopimwa. Ipo migogoro inayosababishwa na viongozi, Wenyeviti wa Mitaa, Wenyeviti wa Vijiji na viongozi wengine wa kisiasa. Limezungumzwa hapa suala la *double allocation*, ipo migogoro inayosababishwa na watumishi wa sekta ya ardhi. Wapo watumishi wengi sana waadilifu, wengi sana waadilifu lakini lazima tukiri wapo watumishi wachache ambao nao wanasababisha migogoro. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Conchesta alieleza vizuri hapa na Mheshimiwa Chumi ameelezea historia ya hapa Dodoma. Zipo historia za utawala wa ardhi hapa Dodoma toka enzi ya *CDA* na sasa halmashauri ya Jiji. Mheshimiwa Rwamlaza amezungumza hapa, lakini naomba kusema, matatizo aliyoyapata yeye na Mheshimiwa Agnesta, hapa Halmashauri ya Jiji la Dodoma amewasemea wengi humu ndani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, huwezi kuamini, sasa umekaa kwenye kiti, wewe mwenyewe ni mhanga wa vitendo vya baadhi ya watumishi wa Jiji la Dodoma kwenye sekta ya ardhi. Yupo Mheshimiwa Waziri mmoja hapa na yeye ni muhanga, wapo Manaibu Waziri sita nao ni wahanga, wapo Wabunge zaidi ya 30 nina taarifa na wenyewe wamepata madhara. Mheshimiwa Waziri Mkuu aliunda Tume, Tume ya kuchunguza utendaji wa sekta ya ardhi na Mheshimiwa Waziri Mkuu alitupa maagizo Wizara ya Ardhi, twende tukatafute njia bora zaidi ya kufanya *land administration* kwenye Jiji la Dodoma ambalo ndiyo Makao Makuu ya Nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kuliarifu Bunge lako Tukufu inatosha, wananchi wengi wanapata madhara, mtu anapewa kiwanja leo anaanza kulipia akija mtu akikipenda anapewa *invoice* ya siku za nyuma, analipishwa hicho kiwanja, yule mwananchi akija anakuta mwingine ametengenezewa hati. Tumeamua rasmi ndani ya Wizara kufunga masjala ya ardhi pale kwenye Halmashauri ya Jiji la Dodoma.

Mheshimiwa Spika, pale Dar es Salaam tulichelewa, vitendo vya *double allocation* vilitokea sana Dar es Salaam na mpaka leo tunaishi navyo, lakini mwaka 2018 Waziri wa Ardhi Mheshimiwa William Vangimembe Lukuvi, ambaye bado ni Mwalimu wetu sisi alifunga pale Masjala ya Halmashauri ya Jiji. Leo tunafanya *administration* ya ardhi pale Ofisi ya Kamishna Msaidizi na shida zote zimepungua. Waheshimiwa Wabunge wameona mfumo tulioufunga Dar es Salaam, leo wapo hapa Dodoma na wamepata hati zenu hapa kwenye Viwanja vya Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kesho asubuhi saa moja Katibu Mkuu namwelekeza, tutaamkia pale Ofisi ya Kamishna Msaidizi wa Ardhi Mkoa wa Dodoma na watumishi wote wanaohudumu kwenye Wizara hii ya Ardhi pale Halmashauri ya Jiji kufikia saa moja na nusu muwe mmeripoti kwa Kamishna Msaidizi wa Ardhi Mkoa wa Dodoma. Hapa Dodoma tutakuwa na Masijala moja, Halmashauri ya Jiji kwa mujibu wa Sheria za Mipango Miji itabaki na mamlaka yake kama *planning authority* na sisi Wizara tutaisaidia kutekeleza majukumu yake lakini *land administration* itafanywa kwenye Masjala moja na tutaanzisha uchunguzi wa kuhakikisha wale wote waliyoathirika wanapata nafuu ya athari zao ili kero hii iweze kwisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tumejipanga Wizarani, tunayo mikakati ya muda mfupi, tunayo mikakati ya muda wa kati na tunayo mikakati ya muda mrefu. Mikakati ya muda mfupi ndiyo kliniki za ardhi tunazozifanya maeneo mbalimbali. Mheshimiwa Dkt. Mollel angesimama hapa angesema na nyinyi ni mashahidi, kliniki za afya zinafanyika kwenye magonjwa ambayo yamezidi, magonjwa madogo madogo kama homa na nini unaenda kwenye hospitali ya kawaida, lakini magonjwa ya moyo, magonjwa ya sukari yanawekewa kliniki maalum. Sasa kazi ya migogoro ya ardhi imekithiri na ndiyo maana tumekuja na kliniki za ardhi. Kwa hiyo tutaendelea na kliniki hizi kama mikakati ya muda mfupi.

Mheshimiwa Spika, dhuluma na matapeli kwenye ardhi wamekithiri na lazima twende tukawasikilize wananchi wetu, lazima twende tukawasikilize tuwatatulie matatizo yao. Alichangia hapa Mheshimiwa Kunambi na akaelezea Mhimili wa Mahakama, Katiba inavyotaka kufanya kazi ya kusimamia haki. Nikuthibitishie Serikali inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, inaheshimu Katiba na inaheshimu Mahakama. Serikali hii, Bunge hili la kwako na Mahakama kote kuna binadamu na hakuna binadamu aliyekamilika. Hata mimi Waziri wa Ardhi kuna wakati nitafanya maamuzi mtu mwingine ana haki ya kuyaangalia akasema maamuzi haya Mheshimiwa Waziri, hayakuwa sahihi. Mahakama yetu inafanya kazi nzuri sana, sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pale Kariakoo, Mtaa wa Kongo kuna kesi maarufu ya familia ya Pazi imekwisha na wamepata haki yao na mliona tumeenda kuwakabidhi jengo lao lakini kesi ile imechukua miaka 26. Miaka 26 familia ile inapambana kupata haki yake ambayo hata Waheshimiwa Wabunge hapa ambao hawajasoma sheria ukiwaonesha shauri lile watakwambia haki yao wangeiona miaka 26 iliyopita. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wewe ni daktari wa sheria, *civil procedure code* inatuelekeza kwenye *order forty-three rule* namba mbili, kwamba maombi yote Mahakamani yatawasilishwa kwa *chamber summons* na *affidavit.* Haya hapa Mheshimiwa Mbunge umsimamishe akuandikie *chamber summons* na *affidavit*, hivi ile familia ya Mwananyamala waliyoiona kwenye kipindi cha Maimartha cha *ICU* kuna mtu pale wa kuandika *chamber summons* na *affidavit*? Inabidi atafute wakili. Mawakili nao ni binadamu, wapo Mawakili wenzetu wengi waadilifu wanaofanya kazi nzuri ya kutetea wateja wao, lakini wapo mawakili wanaoingiza wateja wao kwenye matatizo na kukosa haki zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, *there is a legal maxim* inasema; "*those who come into justice, should come with clean hands.*" Leo Mheshimiwa Kanyasu amesema hapa, sheria inataka watu wanaokwenda Mahakamani kutafuta haki waende na mikono misafi, lakini wapo matapeli wanaoghushi nyaraka, wanafungua mashauri. Amesema hapa Mheshimiwa Kanyasu yupo mtu anachukua ramani ya kughushi anapeleka Mahakamani na anaipelekea Mahakama hii inayotenda haki impe haki kwa kutegemea nyaraka zile ambazo siyo sahihi na yule mwananchi mnyonge anayeenda kumpora haki yake hana taarifa kuna kesi, hana uwezo wa kujitetea. Tutasimamia haki za wananchi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, *Civil Procedure Code Order 37* inaelezea vigezo vya kutoa *interlocutory orders* na inaelezea vizuri kabisa, Waheshimiwa Wabunge wanapata fursa ya kwenda kusoma lakini tumeona watu wenye nguvu wanaenda na ile *interlocutory orders* inasababu zake kubwa kupunguza hasara mtu asivunjiwe

nyumba, mnada usifanyike na imesema pale kwamba Serikali haitazuiwa kutekeleza majukumu yake lakini watu wenye nguvu, wenye ufundi wa kisheria wakati mwingine wanakwenda Mahakamani kuzuia haki ya mwananchi mwenye nyaraka halali kabisa za umiliki wa ardhi ili asipate haki yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tutasimamia haki na tupo tayari wakati mwingine kutofautiana na baadhi ya maamuzi kwa sababu tunasimamia haki bila kumwonea mtu yeyote. Kuna kesi moja imefanyika pale Dar es Salaam, yupo tapeli mmoja wa ardhi alichukua hati ya Mzee mmoja anaitwa Mwinyimvua pale *Mbezi Beach*, amekaa na ile hati zaidi ya miaka 10, yule mzee amepambania hati yake mpaka amefariki dunia. Wamebaki warithi wake (wanaye) wanapambania hati yao, akaja kwetu, tukampatia *notice* yule tapeli hakurejesha hati. Tukawapatia wale warithi *duplicate title* wakaendelea wakapata wateja wao wakawauzia, yule tapeli akaenda Mahakamani kufungua shauri.

*Mheshimiwa Spika, Jaji aliyesikiliza kesi ile mwaka 2015, ndiyo aliyekuwa Wakili ali-attest document za Mzee Mwinyimvua kwenda kuvunja nguvu ya Kisheria Power of Attorney ya tapeli yule aliyefanya kwa forgery na akakutwa na forensic ya Jeshi la Polisi kwamba ame-forge na akapelekwa Mahakamani na huyo huyo tapeli akashinda na ame-forge nyaraka.* **[Maneno Haya Siyo Sehemu ya Taarifa Rasmi za Bunge]**

*Mheshimiwa Spika, Jaji aliyekuwa Wakili aliye-attest nyaraka za Mzee Mwinyimvua kwenda kuondoa utapeli ule, kaja kuwa Jaji anasikiliza kesi ya tapeli anataka kwenda kuwaonea wale yatima, wale warithi wa yule mzee marehemu wa watu.* **[Maneno Haya Siyo Sehemu ya Taarifa Rasmi za Bunge]**

Mheshimiwa Spika, tumeshafungua mimi binafsi maana mwisho ameanza kuwaita watumishi wa ardhi ambao Sheria na Mwanasheria Mkuu wa Serikali yupo hapa, inataka mtumiShi wa Serikali akifanya kazi, afanye kazi kwa kuitetea Serikali na atatetewa na Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Jaji anaita watumishi kwa majina yao anawa-*harass* wale watumishi.

Mheshimiwa Spika, hii vita nimeinunua mimi mwenyewe, nimeandika barua kwa Waziri wa Katiba na Sheria, hakuna mtu nchi hii yupo juu ya Sheria. Majaji nao wanayo kanuni zao za maadili tunataka tuone kama kilichofanyika ndiyo maadili ya utaratibu wa sheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimpongeze Mheshimiwa Waziri Mkuu, alikuja kutufungulia kliniki ya ardhi na alitoa maelekezo kupitia Mheshimiwa Jenista Mhagama, kwamba masuala ya utapeli wa ardhi una jinai ndani yake. Ambacho tumefanya marekebisho kwenye Sera ya Ardhi ni pale tu kuongeza ile *trespass of land* kuja kuwa *criminal.*

Mheshimiwa Spika, *Penal Code,* Sura ya 60, ukisoma Kifungu cha 333 *forgery* (kughushi nyaraka) ni kosa la jinai. Ukisoma Kifungu cha 302 kujipatia pesa kwa njia ya udanganyifu *false pretense* ni kosa la jinai. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunamshukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa maelekezo yake, lakini tunamshukuru sana Inspekta Jenerali wa Polisi, Camillus Wambura, anaunga mkono jitihada hizi, mmeona matapeli papa pale Dar es Salaam, wameanza kwenda mbele ya vyombo vya sheria, hatutachoka mpaka haki za wananchi zipatikane. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Bunge hili limetunga Sheria Sura 113, moja ya njia za kupata ardhi haikuorodheshwa kwenye Sheria ile ambayo Bunge hili Tukufu limetunga kwamba, unaweza kupata ardhi kwa kupata *ex-parte judgment* ya nyaraka za kughushi eti ukaleta kwa Msajili wa Hati ukapata ardhi, tutaendelea kufanya kazi ndani ya Serikali na kushirikiana na wenzetu wa Mhimili wa Mahakama kuhakikisha wananchi wanapata haki zao, nilitaarifu Bunge lako kwamba tutaendelea na kliniki hizi mpaka ugonjwa huu wa migogoro ya ardhi utapopungua na kwisha kabisa kwa maelekezo ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunaendelea kuwashukuru na kuwapongeza Waheshimiwa Wakuu wa Mikoa, Waheshimiwa Wakuu wa Wilaya, tunaendelea kuwaomba waendelee

kutekeleza maagizo ya Mheshimiwa Rais, waendelee kushirikiana na Makamishna Wasaidizi wa Ardhi wa Mikoa yote ya Tanzania Bara na waendelee kushirikiana na Maafisa Maendeleo ya Ardhi wa Wilaya zote kufanya kliniki.

Mheshimiwa Spika, Wizara wa Ardhi, tutaendelea na ile kliniki kubwa ambayo sisi Viongozi wa Wizara wenyewe tunahudhuria, safari hii tulikuwa tumefanya kidogo yale waliyokuwa wanayaona Mheshimiwa Cosato, itabidi aongeze *bundle* ile ilikuwa ni 10% tu anayoiona, tulikuwa tunaogopa kidogo tunaweza kuja hapa kwa Wawakilishi wa Watanzania labda wamelipokea vibaya. Pongezi zao zimetuongezea nguvu kwamba, wanayoyasema ni pongezi za Watanzania, tunaenda kuongeza kasi na sasa kliniki hii itaenda kila mahali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kliniki hii sasa itakuwa ni kliniki rasmi na itajulikana kama Samia *Ardhi Clinic*, tutakwenda, Waziri atakwenda, Naibu Waziri atakwenda, tutakwenda kusikiliza Watanzania na tutakwenda kuwafuta machozi Watanzania wote waliodhulumiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wito wangu ni kwa Mtanzania yeyote ambaye anajua amemdhulumu mtu ardhi, mtu ana hati yake wewe umeingia tu kwa sababu una nguvu, arejeshe mapema kabla hatujaja. Tutakuja na niwathibitishie kampeni hii ni maelekezo ya Mheshimiwa Rais, tutakuja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna maeneo tukiri tumekosea wapo watu tumefanya kazi hii *in camera* hamjayaona na wapo watu tumewaagiza kistaarabu wengi wao wametoka wametusema, wameona kama hatujawatendea haki, safari hii tutaenda kufanya kama yale mengine wanayoyaona. Tutaenda na kipira wa mung'anda wataenda mung'anda hatua za kisheria zitachukuliwa kila mtu atapata haki yake, wale wote wenye jinai Sheria itachukua mkondo wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, alisema hapa Mheshimiwa Kanyasu, kliniki hii vilevile ni elimu, ni darasa kwa watumishi wetu wa ngazi za Mikoa na ngazi za Wilaya ili yale tunayoyafanya Viongozi

Wakuu wa Wizara, tukiondoka na wao waendelee kuyafanya ili kazi hii iwe endelevu. Katika hatua za muda mfupi tumeunda Mikoa Maalum ya Ardhi. Pale Dar es Salaam tumeunda Mkoa Maalum wa Ardhi Kinondoni, Ilala, Ubungo, Temeke na Kigamboni, kuunga mkono jitihada za Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan za uwekezaji tumeunda Mkoa wa Uwekezaji. Kwenye Majiji makubwa Mbeya, Mwanza, kote tumeunda Mikoa.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Muharami, amesimama hapa Pwani ya Kaskazini tumeunda Mkoa Maalum na Pwani ya Kusini, pia tumeendelea kufanya kazi ya kuboresha utendaji na kama nilivyosema hapa Dodoma na pale Dar es Salaam, tunaongeza uwezo wa Ofisi ya Waziri ya kufanya kazi ili kuwapunguzia wananchi mzigo.

Mheshimiwa Spika, mwananchi wa Dar es Salaam anapomfuata Waziri Dodoma na wataalamu amewaacha Dar es Salaam hawezi kupata suluhu ya tatizo lake. Kwa pale Dar es Salaam wananchi wapata huduma wakati wote na hapa Dodoma wapata wakati wowote na maeneo mengine tumeendelea kuwasihi wananchi watumie Ofisi za Makamishna Wasaidizi wa Mikoa kama maeneo ya kupata huduma.

Mheshimiwa Spika, tuliagiza tarehe 13 Aprili, kwamba watumishi wote Mikoani watekeleze majukumu yao. Hatuwezi kuwa na Maafisa Ardhi, Maafisa Mipango Miji na Wapima, wamerudikana Ofisini na Miji yetu inaendelea kuharibika lazima watoke. Tumeelekeza wakae Ofisini siku ya Jumatatu na Ijumaa lakini siku ya Jumanne, Jumatano na Alhamisi waende wakafanye kazi zao za kitaalam, nimeelekeza kwenye ziara zetu viongozi tutakagua *log books* zao watuambie wamefanya kazi gani katika kipindi ambacho tumetoa maelekezo haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, yapo masuala ya migogoro ya mipaka yamechangiwa na Mheshimiwa Makoa, Mheshimiwa Olelekaita, Mheshimiwa Kakunda, Mheshimiwa Francis Isack na Mheshimiwa Genzabuke. Tutaendelea kushirikiana na mamlaka zingine ikiwa ni pamoja na Ofisi ya Rais, TAMISEMI katika kuondoa migogoro hii ya mipaka ya kiutawala. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vipo vijiji vingi vina migogoro ya mipaka, zipo Wilaya nyingi zina migogoro ya mipaka, lazima tukiri kwamba, vipo vijiji vimesajiliwa ndani ya hifadhi, vipo vijiji vimesajiliwa na vime-*overlap* upimaji wake. Tutaendelea kushirikiana na kwa kuwa tutafanya ziara nchi nzima, tutafanya kazi ya kujitahidi kutatua matatizo hayo. Naliahidi Bunge lako tutafanya kazi hiyo kwa uadilifu wa hali ya juu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi imefanya marejeo ya Sera ya Ardhi ya mwaka 1995, Toleo la mwaka 2023. Natumia fursa hii kumtoa hofu Mheshimiwa Simai, hatujafuta Sera ya Ardhi ya mwaka 1995, tumeifanyia maboresho. Wakati anazungumza nilimwona Daktari wa Falsafa Mheshimiwa Balozi Dkt. Bashiru Ally Kakurwa akipiga makofi, nimejua alikuwa na shaka ya mchakato wa maboresho ya Sera hii. Sera ya Ardhi ipo palepale tumeongeza matamko toka matamko 46, mpaka matamko 67, tumeongeza malengo makuu toka malengo makuu nane mpaka malengo makuu 16. Misingi ya Sera ile ikiwemo lile tulilolisema hapa la ardhi yetu kumilikiwa na umma wa Watanzania bado ipo palepale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kuliambia Bunge lako katika Sera hii ambayo imepitishwa mwaka 2023 na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, haki za wanawake zimeenda kulindwa. Sera ya Ardhi ya mwaka 1995, ilitambua haki za wanawake hasa kwenye mirathi, lakini iliongeza maneno mila na desturi zitazingatiwa. Watu wanapotaka kumdhulumu mwanamke nchi hii, watu wanapotaka kumdhulumu mjane mirathi yake ndiyo mila na desturi zao watazikumbuka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, leo nilikuwa naongea na Mheshimiwa Profesa Ndakidemi, ana Shahada ya Uzamivu, ana watoto sita mwenye elimu ya chini ana *Degree* ya Uzamili. Mmoja kaoa Mhehe, unaenda kumiliki ardhi Mikocheni, Dar es Salaam, unamiliki ardhi Kisasa halafu unataka mirathi yako ifuate mila na desturi. Ukitaka mila na desturi ungebaki kule Kibosho ukae na kiamba chako uishi maisha ya kijijini na maisha ya kimila ili ukitaka mambo ya mila na desturi tukuelewe. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, Sera ya Ardhi Mapitio ya 2023, inaenda kulinda maslahi na haki za wanawake ambao wamekuwa wakidhulumiwa kwenye mirathi kwa kisingizio cha mila na desturi wakati ni dhahiri maisha tunayoishi si maisha ya mila na desturi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kazi hii ni kazi ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. Mimi ninaomba Waheshimiwa Wabunge, muendelee kutuunga mkono. Tumetoa maelekezo wasimamizi wa mirathi ni marufuku kuuza mali za warithi. Nimeelekeza Wasajili wote wa Ardhi nchi nzima, kazi ya msimamizi wa mirathi ni kupeleka majina ya warithi ili Msajili awaingize kwenye usajili wa ardhi ili wakitaka kuuza wauze ardhi yao wao wenyewe. *(Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ukisoma hati ya jina la msimamizi wa mirathi imeandikwa kabisa *as legal representative* wa marehemu, lakini imekuwa ni desturi ya watu kuuza mali za marehemu kwa kisingizio cha usimamizi wa mirathi. Ipo hukumu moja ya Mahakama ya Rufaa pale Tabora imeondosha kile kilichokuwa kinaitwa *beneficiary consent* maana ilikuwa msimamizi akiuza lazima warithi waridhie. Hukumu ya Mahakama ya Rufaa, imewaondoa warithi kutoa ridhaa ya kuuza, tukienda hivi yatima watadhulumiwa kwenye nchi hii na watu waliopewa kazi ya kusimamia mirathi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu uvamizi, tutaendelea kulinda haki za ardhi na haki halali za ardhi, kila mwenye hati yake tutailinda na tutahakikisha tunaendelea kupiga vita uvamizi ili kila mtu apate haki ya ardhi. Mheshimiwa Mkenge, nitakuja Bagamoyo na Waheshimiwa wote waliomba hapa kufanya ziara kote tutafika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunafanya marekebisho ya Tangazo la Serikali Namba Saba la Mwaka 2021, kwa zile nyaraka za mauziano ya ardhi. Nilipiga marufuku Wenyeviti wa Mitaa, kushiriki mauzo ya ardhi. Maana Wenyeviti wa Mitaa wamejigeuza Makamishna wa Viapo, wanafanya kazi ya Mawakili. Mawakili wana utaratibu wao wa kazi, Wakili akishuhudia utiaji saini anashuhudia biashara ya watu wawili, Mwenyekiti wa Mtaa siyo

Wakili. Tunaenda kurekebisha nyaraka za mauzo ya ardhi mitaani ili Mwenyekiti wa Mtaa akishuhudia yale mauzo ashuhudie kwamba, anamfahamu muuzaji na anathibitisha ardhi ile ni ya muuzaji ili siku yule mnunuzi akiona ametapeliwa na Mwenyekiti wa Mtaa huyu awe ni mmoja atakayeshirikiana na muuzaji katika kwenda kupata mkono wa sheria. *(Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lazima tuokoe Watanzania wetu wanyonge wanaotafuta riziki yao kwa taabu wanaishia kwenda kuuziwa ardhi. Hii *double allocation* ya Dodoma inayofanyika na kwenye mitaa inafanyika. Hili litaenda pamoja na Wenyeviti wa Vijiji, Sheria namba tano Kifungu cha 8(5) kinatoa mamlaka ya ardhi ya vijiji kwa Mkutano Mkuu wa Kijiji na si kwa Mwenyekiti wa Kijiji. Mwenyekiti wa Kijiji hana mamlaka ya kuuza ardhi, kama kuna mtu kanunua ardhi kwa Mwenyekiti wa Kijiji tukimkuta atakuwa ametapeliwa. Tunaenda kufanya marekebisho ya Sheria, Sera ya Ardhi ilishakamilika kwenda kuingiza Kamishna ili aangalie maslahi ya wananchi wa Tanzania kwenye ardhi ya Kijiji na kuepusha Wenyeviti wa Vijiji ambao wanauza ardhi ya wanakijiji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ile hoja ya Mheshimiwa Condester Michael Sichalwe, ya wanakijiji ama Viongozi wa Vijiji kuuza ardhi na wananchi Watanzania. Kwa hotuba ile ya Mwalimu Nyerere tusipokuwa *serious* tutatengeneza Taifa la watu ambao watawatumikia wengine wenye ardhi kubwa na wao kukosa ardhi. *(Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa haraka haraka mambo ya muda wa kati, cha kwanza, ni mfumo wa TEHAMA. Mheshimiwa Kunambi, alichangia hapa na alisema Mfumo wa *ILMIS*. Mheshimiwa Kunambi, ni Mwanasheria mwenzangu ila mimi *degree* ya kwanza inaitwa *Bachelor of Science and Electronic Science and Communication,* ndiyo Shahada pekee ya mifumo ambayo *computer* inashughulikiwa kwa mbele kwenye *software*, inashughulikiwa kwa nyuma kwenye *hardware* na kwenye mawasiliano. *(Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, anavyosema Mheshimiwa Kunambi, *ILMIS* ni kama kusema Toyota ni aina ya gari. Tunaenda kuunda mfumo wa kisasa kabisa utaofanya *management* ya ardhi nchi hii na tayari timu ya vijana ipo pale Arusha na ni kazi ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan na ni maelekeo yake kuhakikisha Sekta ya Ardhi inatawaliwa vizuri. *(Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kupanga, kupima na kumilikisha (KKK) yamesemwa vizuri sana hapa na Naibu Waziri amesema, kupanga matumizi bora ya ardhi vijijini, kupanga maeneo wataalamu wetu wafanye kazi pa kupanga wapange, pa kupima wapime na pa *demarcation* wafanye *demarcation.* Kuna upimaji mwingine hauhitaji hata vifaa wafanye kazi hiyo.

Mheshimiwa Spika, nimpongeze Mheshimiwa Bashe ametenga fedha, lakini tumefanya marekebisho ya Kanuni *GN*. No. 91, kwa kufanya mabadiliko ya maeneo ya wazi Waheshimiwa Wabunge wamesema hapa. Tumeongeza mchakato mkutano wa mtaa utahusika na Kamati za Usalama za Wilaya zitahusika, tunataka maeneo ya wazi yalindwe, tunataka mabadiliko ya matumizi yasimamiwe, hatuwezi kuwa na Taifa ambalo kila mtu akiamka akitaka kubadilisha matumzi anabadilisha matumizi. *(Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Deodatus Mwanyika, aliwahi kuuliza swali hapa Bungeni na Mheshimiwa Bashe nimesema tunashirikiana tunafanya marekebisho ya *GN. No*. 93 ili wananchi wanaolima kwenye maeneo ya Miji waweze kulima kwa furaha na kile kikomo cha eka tatu tumekiondoa. *(Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nimepokea hoja ya Jiji la Mbeya, nikuahidi Jiji lile tutalifanyia kazi kupitia Mradi wa *LTIP* Mheshimiwa Suma amesema vizuri. Tutahakikisha na nikuahidi, bajeti hii ikimaliza kupita eneo tutaanza nalo tutaanza na Jiji la Mbeya. Tutaanza na Jiji la Mbeya kwa heshima kubwa ambayo dunia imekupa wewe pia kwa heshima kubwa ambayo Waheshimiwa Wabunge wa Bunge hili wanayo kwako. Tunataka tutengeneze sura nzuri ya Jiji lile maeneo yote *ring road* yapangwe, yapimwe tuwe na Jiji la kisasa, ubaki na *legacy* katika miaka yako 20, 30, 40,

50 utayokuwa Mheshimiwa Mbunge wa Mbeya Mjini, uache Jiji la kisasa na kazi hii tunaahidi tutaifanya. *(Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hoja ya mashamba. Pamoja tutaendelea kulinda haki za kumiliki lakini hatutaruhusu Watanzania wazawa na wageni kumiliki maeneo makubwa ya ardhi kwa kisingizio cha umiliki na wasiyatumie na waishie kuwakodisha Watanzania na kuwageuza wao *feudalism* ndani ya ardhi yao. *(Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tunashirikiana na Wizara ya Kilimo, tutakagua mashamba mwenye haki yake atapata haki yake na pale ambapo hakuna uzalishaji hatutasita kubatilisha matumizi na kuwapa wenye uwezo ili ardhi ile iweze kuzalisha na wananchi waweze kufanya kazi. *(Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hii inaenda sambamba na hoja ya dada yangu Mheshimiwa Halima James Mdee, Mheshimiwa Halima amezungumzia Shamba la *DDC,* Mheshimiwa Halima tutakwenda kuwasikiliza wananchi wale. Hatuwezi kuwa Serikali ambayo tunakubali kuna haki ya karatasi, lakini lazima tusikilize na haki nyingine tutumie busara. *(Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Halima amezungumzia hekima, Mheshimiwa Tauhida, ameniomba nimwombe Mwenyezi Mungu hekima na Mheshimiwa Hokororo, ameelezea suala la hekima, lazima tunapofanya kazi za kutenda haki hasa ya watu wengi Mheshimiwa Rais, ametuelekeza wananchi wasipate taharuki tutumie hekima na busara kutafsiri Sheria. Tusitumie busara kuvunja Sheria bali tutafsiri sheria kwa hekima na busara. *(Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hoja ni nyingi kuna hoja ya uthamini tumetoa waraka namba moja wa mwaka 2024, tutakuwa wakali Wizara ya Ardhi, kwa mtu yeyote ndani ya Serikali anayetaka kuwa na mradi ahakikishe kabla ya kutwaa maeneo ya wananchi anazo fedha za kulipa fidia. Unakuta kule mkoani au wilayani, Afisa tu wa Serikali ameamua kuwe na mradi anatwaa maeneo ya watu. Hata Mkoani hawajui, Wizara yake haijui mpaka ije kujua

ni miaka mitatu, minne, waje kuomba fedha hapa mpaka zitengewe miaka mitano, sita wananchi wanateseka. *(Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tumetoa Waraka Na.1 wa Mwaka 2024 kulinda wananchi wetu, Katiba yetu Ibara ya 24(2) inataka wananchi wamiliki mali na tulinde umiliki wao, hoja hiyo amezungumzia Mheshimiwa ya Magessa, ya *surface right versus mining right,* tunafanya kazi na Mheshimiwa Mavunde, kuweza kuhakikisha jambo hili na lenyewe linafanyiwa kazi. *(Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nikikaribia kumalizia naomba niliambie Bunge lako, sifa na pongezi mlizotupa niwaahidi hazitotulevya wala hatuwezi kuzichukulia poa. Sifa na pongezi tulizopewa na Waheshimiwa Wabunge tumezichukua kama deni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naahidi dawa ya deni ni kulipa na usiku wa deni haukawii kukucha. Tutahakikisha tunalipa sifa hizi kwa kuwafanyia kazi Waheshimiwa Wabunge na wananchi wa Tanzania kwa kutekeleza maelekezo ya Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan. Mheshimiwa Kanyasu tutakwenda kwenye jimbo lake, Mheshimiwa Agnesta amesema kule Mkoa wa Pwani tutakwenda kwa wale wananchi wa Segerea, Mheshimiwa Condester kwenye lile shamba tutakwenda na maeneo mengine yote. Niwaambie Waheshimiwa Wabunge hizi suti tutavaa hapa Bungeni, tukimaliza bajeti tutavaa buti na *jeans* tutakwenda kule wananchi wanakopata shida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Wizara hii Mheshimiwa Rais sio Wizara ya kwenda Nje ya Nchi. Kwenda Nje ya Nchi ni kazi ya Wizara ya Mambo ya Nje, sisi Wizara yetu tutakwenda kule wananchi walipo. Hli ndiyo dhamana Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan ametupa Wizara ya Ardhi na wala hatutochoka. Tutakuja na itakuwa ndiyo malipo ya deni hili ambalo wametukopesha kwa kutupa sifa hizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niendelee kushukuru vyombo vyote vya Serikali na Serikali nzima. Mheshimiwa Waziri Mkuu yuko hapa, Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu na Mawaziri wote wamekuwa

wakitupa *support*. Nimeeleza hapa Mheshimiwa *IGP* amekuwa akitu-*support*. Niwathibitishie tutafanya kazi hii.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Lusinde aliongelea suala la ulinzi. Zaburi ya 127:1-2 neno la Mungu linasema, "Bwana asipoulinda mji, yeye aulindae akesha bure." Niwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote waliotuombea Baraka za Mungu, niwahakikishie vilio na machozi ya Watanzania tunayoyafuta ndiyo ulinzi mkubwa kwa Mwenyezi Mungu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nikuthibitishie yuko mtu mmoja aliandika kwenye mtandao hii nchi sio ya kuchukuliana poa. Msituone Kariakoo tunazurura, siyo kila mtu pale ni machinga wengine wako kazini, jichanganye utaona nguvu ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. Pale napo vijana wa Kizimkazi wapo na hapa ipo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nikuthibitishie kazi tuliyoifanya lakini naomba niwaahidi Wabunge wote waliochangia, hoja zote tutazijibu kwa maandishi. Waheshimiwa Wabunge niwaombe sana zile hoja ambazo hatujazijibu tumeziheshimu sana, tutatoa majibu kwa maandishi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa naomba kuomba fedha. Jumla ya fedha zinazoombwa kuidhinishwa na Bunge lako Tukufu kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 kwa mafungu yote mawili (Fungu la 48 na Fungu Na. 3) ni jumla ya shilingi 169,628,415,000. Fedha hizo kwa Fungu 48 ni shilingi 157,455,085,000 na kwa Fungu Na. 3 ni shilingi 12,173,330,000.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono, ahsanteni sana. *(Makofi)*

Sasa kwa sababu vitabu ambavyo Mheshimiwa Waziri alikuwa amewasilisha hoja yake jana vilikuwa na hesabu ambayo wakati wa majumuisho kwa maana ya Fungu 48 na Fungu Na.3 viliandikwa sawasawa isipokuwa kwenye jumla kuu iliyoandikwa baadaye ilikuwa imeongezeka kwa kiasi cha 1,744,093,000.

Kwa hivyo, fedha halisi ambayo anaiomba Mheshimiwa Waziri ni ile ambayo imetajwa sasa wakati akihitimisha hoja. Kwa hiyo, wale ambao wanavyo vile vitabu unaweza kurekebisha ile sehemu. Pia, kwa maelezo haya upande wa Katibu wa Bunge pia afanye marekebisho kwenye vile vitabu ili Taarifa Rasmi za Bunge zikae sawasawa.

Baada ya kusema hayo, Waheshimiwa Wabunge tunaendelea na utaratibu wetu.

Katibu.

**NDG. EMMANUEL MPANDA – KATIBU MEZANI:** Kamati ya Matumizi.

**SPIKA:** Kamati ya Matumizi.

**KAMATI YA MATUMIZI**

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tukae.

Katibu.

**NDG. MICHAEL CHIKOKOTO, *ndc* – KATIBU MEZANI:**

**KITABU CHA PILI - MATUMIZI YA KAWAIDA**

**Fungu 48 – Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi**

Kifungu 1001 - *Administration and Human Resources Management*...................................Sh. 11,356,722,000

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, kifungu hiki kina mshahara wa Waziri. Ninayo majina hapa ya Wabunge ambao wanahitaji ufafanuzi wa jambo ambalo ni la kisera. Mheshimiwa Condester Michael Sichalwe.

**MHE. CONDESTER M. SICHWALWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa nafasi. Kwanza nikiri kwamba nimeridhishwa na ufafanuzi wa Mheshimiwa Waziri. Maelezo yake yameonesha kuleta matumaini kwa Watanzania wengi ambao wamemsikia leo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina ombi moja tu, atoe *commitment* kwenye lile tabaka ambalo Baba wa Taifa alisema, kwenye lile kundi ambalo wapo Watanzania ambao wamejitwalia maeneo makubwa na kuwafanya wenzao kuwa watwana kinyume na utaratibu. Ni upi mkakati wa haraka wa Wizara kuwafanya kundi hilo la watwana lisiwepo na hao Watanzania wabaki na maeneo ya kawaida. Mfano mtu ana ekari 2,000 au 1,000 kwenye kijiji cha watu 200,000 na watu hawana maeneo. *Commitment* tu ya Mheshimiwa Waziri katika hili lakini nimeridhishwa na ufafanuzi wake. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Sasa Mheshimiwa Sichalwe unanipa wakati mgumu sana kumnyanyua Waziri. Umeanza na umeridhika, umemalizia na umeridhika. Sasa anasimama kusema nini wakati umeridhika sana? Mheshimiwa Waziri naona umejiandaa kusimama. *(Makofi)*

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba kuliarifu Bunge lako kwamba Wizara itaendelea kuunga mkono jitihada za Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kuhamasisha uwekezaji na niseme kwenye uwekezaji ardhi ni msingi muhimu. Tutaendelea kutoa ardhi za uwekezaji kwa ukubwa wa aina ya uwekezaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mkakati aliouomba Mheshimiwa Mbunge, Mheshimiwa Rais kama mmesikiliza maelekezo yake na mimi nimekuwa nikiyarejea ipo haki haramu na ipo haki halali.

Yupo mtu kama nilisikia mchango wake vizuri, anapata eneo kijiji A kwa *approval* ya Kijiji B. Yupo mtu anapata eneo kwa kupewa na Mwenyekiti wa Kijiji wakati Sheria, Sura ya 114 inataka mkutano mkuu wa kijiji; ile ni haki haramu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunachokifanya, tutafanya ukaguzi na ukaguzi huu wenzetu wa kilimo tutashirikiana nao. Huyu mtu ana hekta 2,000 ana hekta 5,000 wenzetu wa kilimo watatuambia hekta 5,000 inatakiwa kuzalisha mazao kiasi gani ili atuoneshe uzalishaji wake ukoje na mchango wake ukoje. Ili kama tukithibitisha kwenye masharti ya umiliki hajaendeleza hatua zitachukuliwa ikiwemo kubatilisha umiliki wake na ardhi hii itatumiwa na watu wengine wenye uhitaji. Hiyo ndiyo *commitment* ya Wizara na naomba nimuahidi tutafanya kwa moyo na kwa uadilifu mkubwa. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, Mheshimiwa Jafari Wambura Chege.

**MHE. JAFARI W. CHEGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi. Kimsingi sijakusudia kushika shilingi ya Mheshimiwa Waziri kwa kazi kubwa nzuri ambayo ameendelea kuifanya, lakini nilitaka nipate ufafanuzi juu ya jambo moja la malimbikizo ya kodi kwa Mashirika ya Umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye Taarifa ya Mheshimiwa Waziri amezungumza kodi inayodaiwa kwa Mashirika ya Umma zaidi ya shilingi bilioni 136 lakini wakati Mheshimiwa Waziri akijibu hoja hii alitoa mfano kwa wananchi hawa wadogowadogo na akatoa mfano kwako pamoja na Diamond. Sikusikia akizungumzia haya Mashirika ya Umma ambayo kimsingi nadhani yanadaiwa fedha nyingi kuliko hata ambayo ameenda kuilipa leo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwa kutokuitaja napata kidogo mashaka kwamba tunai-*handle* vipi. Tukumbuke madeni haya ndiyo yale Mheshimiwa Rais alisamehe riba hivi karibuni baada ya kuwa yamelimbikizwa kwa miaka nenda rudi. Haya Mashirika ya Umma ni taasisi za Serikali na Wakurugenzi ni wateule wa Mheshimiwa Rais. Kutokulipa kodi hizi kunasababisha

malimbikizo makubwa sana kwa Wizara na wakati mwingine wanasababisha fedha hizi kutokwenda kwenye huduma za kijamii. Kwa hiyo nilitaka nipate *commitment* ya Waziri; nini mpango waliojipangia kuhakikisha kodi hizi zinalipwa kwa wakati?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri ufafanuzi.

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilieleza pale awali msingi wa umiliki wa ardhi yetu nchini ni ardhi ya umma na sheria inawapa watu upangaji *(right of occupancy)* na kila mwenye kutumia ardhi anapaswa kuwalipa Watanzania kodi ya pango la ardhi. Kwa sababu ya muda nilitolea mfano wa watu binafsi na viongozi lakini zipo Taasisi za Umma na Binafsi na zenyewe zinadaiwa kodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kutumia Bunge lako niendelee kusema kwamba tangazo ama ile Ilani ya Wizara niliyoitoa inagusa watu wote. Zipo jitihada ndani ya Serikali ya kuhakikisha taasisi za Serikali zinalipa kodi. Tutaendelea kushirikiana na wenzetu ndani ya Serikali kuendelea kuhamasisha ulipaji wa kodi ya ardhi na hatutosita kuchukua hatua kwa taasisi ambazo zitathibitika zina uwezo wa kulipa kodi, lakini wanakalia ardhi ya Watanzania bila kulipia kodi na hivyo wanakwamisha maendeleo kwa sekta za huduma za jamii na Sekta ya Ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hiyo ndiyo *commitment* ya Wizara na nimwombe Mheshimiwa Chege ambaye ni *practitioner* wa sekta ya ardhi aridhie maelezo haya na aridhie kupitisha na kuunga mkono bajeti yetu. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**NDG. MICHAEL CHIKOKOTO, *ndc* – KATIBU MEZANI:**

Kifungu 1002 - *Finance and Accounts Unit*..............Sh. 1,333,814,000
Kifungu 1003 - *Policy and Planning Department*....Sh. 1,289,657,000

**MWENYEKITI:** Kuna mtu amepiga meza? Mheshimiwa Waziri vipi bwana mbona unaniangusha? Ukipiga meza kwenye ngazi hii maana yake una jambo la kusema. Tupo kwenye Kamati ya Matumizi, ukipiga meza maana yake una jambo unataka kusema.

Hapana siyo Waziri wewe, aliyepiga meza maana naona Waziri wa Ardhi alihisi yeye ndiyo amepiga meza.

**NDG. MICHAEL CHIKOKOTO, *ndc* – KATIBU MEZANI:**

Kifungu1004 - *Management Information System Unit*......................Sh. 1,666,764,000
Kifungu 1005 - *Internal Audit Unit*................................Sh. 602,626,000
Kifungu 1006 - *Procurement Management Unit*........Sh. 673,416,000
Kifungu 1007 - *Government Communication Unit*....Sh. 593,565,000
Kifungu 1008 - *Legal Services Unit*...............................Sh. 661,464,000
Kifungu 1009 - *Monitoring and Evaluation Unit*………Sh. 300,000,000
Kifungu 2001 - *Land Management and Development Department*....................................Sh. 15,314,840,000
Kifungu 2002 - *Surveys and Mapping Department*………………Sh. 10,958,306,000
Kifungu 2003 - *Registration of Titles Unit*....................Sh. 1,327,040,000
Kifungu 2004 - *Valuation Department*......................Sh. 5,178,912,000
Kifungu 2005 - *Dar es Salaam Land Office*...............Sh. 1,374,779,000
Kifungu 2007 - *Dodoma Land Office*..........................Sh. 920,000,000
Kifungu 2008 - *Tabora Land Office*............................ Sh. 670,000,000
Kifungu 2009 - *Mwanza Land Office*..........................Sh. 900,000,000
Kifungu 2010 - *Kilimanjaro Land Office*.......................Sh. 700,000,000
Kifungu 2011 - *Mtwara Land Office*............................Sh. 590,000,000
Kifungu *2012 - Mbeya Land Office*............................Sh. 810,828,000
Kifungu 2013 - *Simiyu Land Office*..............................Sh. 580,361,000
Kifungu 2014 - *Arusha Land Office*..............................Sh. 710,716,000
Kifungu 2015 - *Geita Land Office*.................................Sh. 600,000,000
Kifungu 2016 - *Njombe Land Office*............................Sh. 600,000,000

Kifungu 2017 - *Katavi Land Office*................................Sh. 600,000,000
Kifungu 2018 - *Coastal Land Office*.............................Sh. 720,023,000
Kifungu 2019 - *Iringa Land Office*.................................Sh. 520,493,000
Kifungu 2020 - *Kigoma Land Office*.............................Sh. 618,544,000
Kifungu 2021 - *Lindi Land Office*...................................Sh. 600,000,000
Kifungu 2022 - *Mara Land Office*..................................Sh. 715,000,000
Kifungu 2023 - *Morogoro Land Office*..........................Sh. 860,000,000
Kifungu 2024 - *Ruvuma Land Office*.............................Sh. 640,000,000
Kifungu 2025 - *Shinyanga Land Office*..........................Sh. 620,000,000
Kifungu 2026 - *Singida Land Office*..............................Sh. 594,000,000
Kifungu 2027 - *Tanga Land Office*.............................. Sh. 800,000,000
Kifungu 2028 - *Kagera Land Office*.............................Sh. 670,000,000
Kifungu 2029 - *Rukwa Land Office*...............................Sh. 550,000,000
Kifungu 2030 - *Songwe Land Office*.............................Sh. 550,000,000
Kifungu 2031 - *Manyara Land Office*.......................... Sh. 595,403,000
Kifungu 3001 - *Human Settlement Development Department*......................................Sh. 10,261,821,000
Kifungu 3002 - *Real Estate Unit*.......................................Sh. 453,908,000
Kifungu 3003 - *District Land and Housing Tribunal Unit*..........................Sh. 6,715,373,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 03 – Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi**

Kifungu 1001 - *Directorate of Corporate Services*...Sh. 2,872,973,500
Kifungu 1003 - *Procurement and Management Unit*.................................Sh. 206,498,000
Kifungu 1004 - *Internal Audit Unit*..................................Sh. 170,360,000
Kifungu 1005 - *Legal Services Unit*...............................Sh. 393,430,000
Kifungu 2001 – *Directorate of Land Use Planning, Management & Coordination Division*...................................................Sh. 929,718,000
Kifungu 2002 - *Directorate of Research, Compliance & Information*............................................ Sh. 780,390,500
Kifungu 2003 - *Zonal Offices*....................................Sh. 1,778,728,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**KITABU CHA NNE - MIPANGO YA MAENDELEO**

**Fungu 48 – Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi**

Kifungu 1001 - *Administration and Human Resources Management*......................................Sh. 696,687,000
Kifungu 1003 - *Policy and Planning Department*..........................Sh. 0
Kifungu 1004 - *Management Information System Unit*.................Sh. 0
Kifungu 1005 - *Internal Audit Unit*..................................Sh. 300,000,000
Kifungu 1009 – *Monitoring and Evaluation Unit*..........Sh. 350,000,000
Kifungu 2001 - *Land Management and Development Department*.....................................Sh. 59,408,985,000
Kifungu 2002 - *Surveys and Mapping Department*.......................................Sh. 9,638,538,000
Kifungu 3001 – *Human Settlement Development Department*..........................................Sh. 262,300,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 03 – Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi**

Kifungu 1001 - *Directorate of Corporate Services*......Sh. 252,000,000
Kifungu 2001 – *Directorate of Land Use Planning, Management & Coordination Division*.....................Sh. 4,666,732,000
Kifungu 2002 - *Directorate of Research, Compliance & Information*..................................Sh. 122,500,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**NDG. MICHAEL CHIKOKOTO, *ndc* – KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa taarifa kwamba Kamati ya Matumizi imekamilisha kazi yake.

**MWENYEKITI:** Bunge linarejea.

*(Bunge Lilirejea)*

**SPIKA:** Waheshimiwa, tuketi. Mtoa hoja, taarifa.

**T A A R I F A**

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, Bunge lako limekaa kama Kamati ya Matumizi na limekamilisha kazi yake. Naomba Taarifa ya Kamati ya Matumizi ikubaliwe na Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono. Sasa nitawahoji Waheshimiwa Wabunge kuhusiana na hoja ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa mwaka wa fedha 2024/2025. Wote mmeafiki.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kuwahoji na ninyi kusema ndiyo, ni kwamba sasa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa mwaka wa fedha 2024/2025, yamepitishwa rasmi na Bunge. *(Makofi)*

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 Yalipitishwa na Bunge)*

**SPIKA:** Nitumie fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu na watendaji wote ambao mnafanya nao kazi kwenye Wizara hii. Nawapongeza kwa hotuba yenu ambayo Waheshimiwa Wabunge wameona kwamba inafaa kupitishwa na kwa hivyo yale ambayo mmeyaomba kwao wamewapitishia leo. Kwa hiyo

tunawapongeza sana na vivyo hivyo tunawatakia kila la kheri katika kutekeleza yale mliyoyaahidi jana wakati mkiwasilisha hotuba na mengine ambayo mmeyaahidi baada ya kusikia michango ya Waheshimiwa Wabunge. Tunawatakia kila la kheri kwenye utekelezaji wa hayo yote. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, namshukuru sana pia Mheshimiwa Mwenyekiti wetu wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii, Makamu Mwenyekiti na Wajumbe wote wa Kamati hii kwa kuendelea kuisimamia Wizara hii vizuri kwa niaba ya Bunge. Tunawashukuru sana kwa kazi hiyo nzuri ambayo mmeifanya.

Waheshimiwa Wabunge wote ambao mmepata nafasi ya kuchangia pia kama mlivyomsikia Mheshimiwa Waziri alivyohitimisha hoja hapa, bila shaka michango yenu itaiongezea Wizara hii nguvu zaidi katika kutekeleza ama kuboresha yale ambayo walikusudia kuyafanya. Kwa hiyo tunawashukuru ninyi nyote. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo kuna mambo matatu hapa; jambo la kwanza ni la ufafanuzi. Wakati Mheshimiwa Waziri akihitimisha hoja yake hapa, sikutaka kumkatisha, amezungumza mambo mengi yanayohusu Mhimili wa Mahakama. Ameeleza kuhusu kesi ya tapeli ambaye huyo tapeli amefanya mambo ambayo pengine hayafai ndiyo maana anaitwa tapeli, lakini sasa kesi imepelekwa kwa Jaji ambaye huko nyuma aliwahi kuwa wakili na alihusika kwenye jambo hili akiwa wakili na sasa amekuwa sehemu ya Mahakama. *(Makofi)*

Sasa kwa utaratibu wetu ule wa hii mihimili kuheshimiana, kama liko jambo ambalo haliko sawa kwa huyu Jaji kusimamia kesi hii si kazi ya sisi Waheshimiwa Wabunge kusema kama anafaa au hafai. Kwa sababu utaratibu upo kule Mahakamani wa namna ya kumwondoa huyu Jaji ambaye anasimamia kesi ambayo ana maslahi nayo. *(Makofi)*

Kwa hiyo, wao wana utaratibu na kwa mawakili, huwa inajulikana nini cha kufanya ili huyo Jaji ajiondoe kwenye kesi

yake. Kwa hiyo, si hoja ya Bunge hapa. Kwa hiyo natoa huo ufafanuzi kwa maana ya kwamba maneno aliyoyaeleza Mheshimiwa Waziri hapa yanaweza yakaleta picha fulani kwa upande wa Mahakama, kwamba watumishi wao ama majaji wanajadiliwa humu ndani. Jambo ambalo halitaleta picha nzuri kwa sababu ya ile heshima ambayo Katiba yetu imeiweka.

Waheshimiwa Wabunge, hivyo kwenye jambo hili hata siwezi kusema kama lipo kweli Mahakama ifanye hivi, si utaratibu wa kawaida. Ila kwa namna Mheshimiwa Waziri alivyolisema hapa ndani na kuhusu kughushi nyaraka maana yake amelisema kwa sura ambayo ni tuhuma; na kwa sababu ni tuhuma sasa anayetuhumiwa ni Jaji na utaratibu wa kumtuhumu Jaji uko kwa sura nyingine. Basi kwa sura hiyo maelezo aliyoyatoa Mheshimiwa Waziri ili isionekane hizi tuhuma kumhusu huyo Jaji zilitolewa Bungeni, basi hayo maneno yanaondoka kwenye Taarifa Rasmi za Bunge. *(Makofi)*

Sasa ninavyosema yanaondoka, yanaondoka yale yote ambayo yalihusu eneo hilo, ikiwa ni pamoja na maelezo ya kusema kwamba majaji wana chombo chao cha kuangalia maadili, ni kweli lakini siyo kazi ya sisi humu ndani kulizungumzia hilo kwa sababu wao wanao utaratibu, ikiwa mtu ambaye anaona hajatendewa haki na huyo Jaji kwa kusimamia kesi yake au kwa namna nyingine yoyote ile kwa sababu wanaweza kufanya hivyo. Ili sasa tukae vizuri, basi hayo yatakaa kwa namna hiyo. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Waziri ameeleza pia kuhusu Kliniki za Ardhi; nadhani ametoa ufafanuzi wa kutosha hapa na ninyi Waheshimiwa Wabunge mmesema namna ambavyo mnaona hizi Kliniki zinawasaidia wananchi kwenye kutatua changamoto zao. Jambo ambalo Bunge linaweza kusema kwa ujumla wake kwa sababu yale mengine ni Waheshimiwa Wabunge tulikuwa tunasema kila mmoja wetu; ni kwamba katika yote hayo yanayofanyika, lazima utaratibu wa kisheria ufuatwe. Wakati huo utaratibu unafuatwa lazima kuangalia mipaka iliyowekwa kati ya utendaji wa Serikali na utendaji wa Mahakama kwa muktadha wa Katiba yetu ya

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Nalisema hili ili isije ikaonekana Serikali inafanya shughuli za Mahakama ama Mahakama inaofanya shughuli za Serikali, ama Bunge linafanya shughuli za Mahakama. Kwa hiyo mihimili hii imewekewa ile misingi ili kuondoa huo mvurugano. Hilo lilikuwa jambo la kwanza nililoona kwamba linahitaji ufafanuzi. *(Makofi)*

Jambo la pili ni tangazo la wageni. Yupo mgeni wa Mheshimiwa Festo Sanga ambaye jina lake halijawekwa hapa lakini nimeambiwa ni mzee maarufu wa Kijiji cha Ihanga kutoka Makete. Ahsante sana mzee wetu. Karibu sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, ahsante sana, huyu mzee ni bingwa sana huyu, amejua kwamba Waheshimiwa Wabunge walikuwa wanamaanisha hawajamwona vizuri; sasa nadhani wamemwona. Ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge, jambo la mwisho linahusu taarifa ya Mheshimiwa Spika, chini ya Kanuni ya 39(2) na Kanuni ya 144 ya Kanuni za Kudumu za Bunge.

Waheshimiwa Wabunge, tarehe 14 Februari, 2024 nilipokea barua kutoka katika Kanisa la Efatha ikiwasilisha utetezi wake kuhusu mchango alioutoa Mheshimiwa Deus Clement Sangu dhidi ya Efatha. Mchango huo ulihusu mgogoro wa ardhi kati ya wawekezaji kwenye Shamba la Malonje na vijiji vinavyolizunguka shamba hilo kikiwemo Kijiji cha Sikaungu katika Jimbo la Kwela.

Kwa kuzingatia maombi ya Kanisa la Efatha kukutana na Kamati ya Bunge inayohusika, nililipeleka suala hilo kwenye Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii ili lifanyiwe kazi.

Waheshimiwa Wabunge, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii ilikutana na viongozi wa Kanisa la Efatha, Mbunge na wawakilishi wa Kijiji cha Sikaungu. Tarehe 9 Mei, 2024 Kamati hiyo iliwasilisha kwangu taarifa kuhusu matokeo ya kikao hicho. Katika taarifa hiyo Kamati ili ilibainisha yafuatayo:-

(a) Mgogoro wa Shamba la Malonje ni wa muda mrefu na kwamba umekuwa ukizungumzwa Bungeni na Waheshimiwa Wabunge mbalimbali kwa nyakati tofauti kabla ya Mheshimiwa Deus Clement Sangu hajaingia humu ndani;

(b) Licha ya kuwepo kwa kumbukumbu za mawasiliano kati ya Mheshimiwa Waziri wa Ardhi na wawekezaji wa shamba hilo zinazoonesha mgogoro umekwisha, kiuhalisia mgogoro huo bado upo na umedumu kwa miaka 13 ukiwa na madhara makubwa kwa pande zinazohusika;

(c) Hatua zilizochukuliwa na Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Mkazi katika kutatua mgogoro huo tarehe 17 na tarehe 23 Novemba, 2023 haziendani na kumbukumbu zilizopo Bungeni kuanzia mwaka 2014 hadi 2015 zilizohusu majibu ya Serikali kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge wakiwemo Mheshimiwa Ignas Aloyce Malocha na Mheshimiwa Khalfan Hilaly Aeshi; na

(d) Wananchi wa vijiji vinavyozunguka Shamba la Malonje hawaridhiki na namna Wizara inavyoshughulikia mgogoro huko.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kupitia barua ya Kanisa la Efatha, Taarifa ya Kamati ya Ardhi, Maliasili na Utalii pamoja na Taarifa Rasmi za Bunge *(Hansard)*, nimeamua kuunda Kamati Maalum chini ya Kanuni ya 144 ya Kanuni za Kudumu za Bunge. Kamati hiyo itaongozwa na hadidu za rejea zifuatazo:-

(a) Kubaini eneo la Shamba la Malonje lilipoanzia;

(b) Kubaini mipaka halisi ya Shamba la Malonje na vijiji vinavyolizunguka;

(c) Kubaini iwapo taratibu za uongezaji wa eneo zilifuatwa katika ongezeko la ukubwa wa Shamba la Malonje;

(d) Kubaini iwapo kuna dalili za vitendo vya uvunjifu wa haki za binadamu vinavyodaiwa kufanywa na walinzi wa Shamba la Malonje na iwapo vitendo hivyo vinatokana na miongozo ya wamiliki wa shamba hilo; na

(e) Kubaini jambo lingine lolote linalohusiana na mgogoro huo.

Waheshimiwa Wabunge, kwa kuzingatia hadidu za rejea hapo juu, nawateua Waheshimiwa Wabunge wafuatao kuunda Kamati hiyo. Wajumbe hao ni:-

(i) Mheshimiwa Dkt. Hamisi Andrea Kigwangalla;
(ii) Mheshimiwa Lucy Thomas Mayenga;
(iii) Mheshimiwa Mhandisi Stella Martin Manyanya;
(iv) Mheshimiwa Innocent Sebba Bilakwate;
(v) Mheshimiwa Festo Richard Sanga;
(vi) Mheshimiwa Asia Abdukarimu Halamga;
(vii) Mheshimiwa Eric James Shigongo;
(viii) Mheshimiwa Ester Amos Bulaya;
(ix) Mheshimiwa Joseph Anania Tadayo;
(x) Mheshimiwa Tauhida Gallos Cassian; na
(xi) Mheshimiwa Profesa Shukrani Elisha Manya. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, Kamati hii itaongozwa na Mheshimiwa Profesa Manya na itafanya kazi kuanzia tarehe 15 hadi tarehe 28 Julai, 2024. Aidha, Kamati Maalum itapaswa kukabidhi taarifa kwangu kabla ya tarehe 2 Agosti, 2024 kufuatana na masharti ya Kanuni ya 144(5) ya Kanuni za Kudumu za Bunge. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya hili jambo la tatu, tumefika mwisho wa siku yetu ya leo na kwa hivyo naahirisha Shughuli za Bunge mpaka kesho saa 3.00 asubuhi. *(Makofi)*

*(Saa 1.15 Usiku Bunge Liliahirishwa hadi Siku ya Jumanne, Tarehe 28 Mei, 2024 Saa Tatu Asubuhi)*